**6 APRILI, 2023**

**BUNGE LA TANZANIA**

---

# MAJADILIANO YA BUNGE

---

## MKUTANO WA KUMI NA MOJA

### Kikao cha Tatu – Tarehe 6 Aprili, 2023

*(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Spika (Mhe. Dkt. Tulia Ackson) Alisoma Dua*

**SPIKA:** Waheshimiwa tukae. Katibu.

**NDG. EMMANUEL MPANDA – KATIBU MEZANI:**

**HATI ZA KUWASILISHA MEZANI**

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na:-

**WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:**

Mheshimiwa Spika, naomba kuweka mezani Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa Mwaka wa Fedha ulioishia tarehe 30, Juni 2022 pamoja na ukaguzi mwingine.

(a) Ripoti ya Mwaka ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ya Ukaguzi wa Serikali Kuu kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022 *(The Annual General Report of the Controller and Auditor General on the Audit of Central Government for the Financial Year 2021/2022)*

(b) Ripoti ya Mwaka ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ya Ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022 *(The Annual General Report of the Controller and Auditor General on the Audit of Development Projects for the Financial Year 2021/2022)*

(c) Ripoti ya Mwaka ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ya Ukaguzi wa Mashirika ya Umma kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022 *(The Annual General Report of the Controller and Auditor General on the Audit of Public Authorities and Other Bodies for the Financial Year 2021/2022)*

(d) Ripoti ya Jumla ya Mwaka ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ya Ukaguzi wa Ufanisi kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022 *(The Annual General Report of the Controller and Auditor General on the Performance Audit for the Financial Year 2021/2022)*

(e) Taarifa ya Ukaguzi wa Ufanisi kuhusu Utekelezaji wa Malengo ya Maendeleo endelevu nchini *(Performance Audit Report on the Implementation of Sustainable Development Goals)*

(f) Taarifa ya Ukaguzi wa Ufanisi kuhusu Usimamizi wa Uondoshaji wa Magari ya Serikali *(Performance Audit on the Management of Disposal of Government Vehicles)*

(g) Ripoti ya Ufuatiliaji wa Utekelezaji wa Mapendekezo ya Kaguzi za Ufanisi zilizofanyika na kuwasilishwa Bungeni Mwezi Aprili ,2018 na 2019 *(Follow – Up Report on the Implementation of the Controller and Auditor General's Recommendations for the Performance Audit Reports issued and tabled before the Parliament in April 2018 and 2019)*

(h) Taarifa ya Ukaguzi wa Ufanisi kuhusu Usimamizi wa Uwekezaji wa Mali za Serikali zisizohamishika unaosimamiwa na Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma *(PSSSF)* na Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii *(NSSF) (Performance Audit Report on the Management of Property Investment as Implemented by PSSSF and NSSF)*

(i) Ripoti Kuu ya Mwaka ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ya Ukaguzi wa Tawala za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022 *(The Annual General Report of the Controller and Auditor General on the Audit of Regional Administration and Local Government Authorities for the Financial Year 2021/22)*

(j) Ripoti ya Mwaka ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kuhusu Ukaguzi wa Mifumo ya TEHAMA kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022 *(The Annual General Report of the Controller and Auditor General on the Audit of Information Systems for the Financial Year 2021/2022)*

(k) Taarifa ya Ukaguzi wa Ufanisi kuhusu Usimamizi wa Mipango na Ujenzi wa Mifumo ya TEHAMA Serikalini *(Performance Audit Report on the Management of Planning and Acquisition of ICT Systems in the Government)*

(l) Taarifa ya Ukaguzi wa Ufanisi kuhusu Utekelezaji wa Mpango wa Kunusuru Kaya Maskini wa Awamu ya Kwanza *(Performance Audit Report on the Management of Productive Social Safety Net One)*

(m) Taarifa ya Ukaguzi wa Ufanisi kuhusu Usimamizi wa Viumbe Vamizi katika Mazingira ya Nchi kavu *(Performance Audit Report on the Management of Invasive Alien Species in Terrestrial Environment)*

(n) Taarifa ya Ukaguzi wa Ufanisi kuhusu Udhibiti wa Vyanzo vya Mionzi *(Performance Audit Report on the Control of Radiation Sources)*

(o) Taarifa ya Ukaguzi wa Ufanisi kuhusu Usimamizi wa shughuli za Utafiti na Ubunifu *(Performance Audit Report on the Management of Research and Innovation)*

(p) Taarifa ya Ukaguzi wa Ufanisi kuhusu Usimamizi wa Urasimishaji wa Makazi yasiyopangwa *(Performance Audit Report on the Management of Regularization of Unplanned Settlements)*

(q) Taarifa ya Ukaguzi wa Ufanisi kuhusu Usimamizi wa Usindikaji na Uongezaji wa Thamani wa Mazao ya Kilimo *(Performance Audit Report on the Management of Agro-Processing and Value Addition of Crops)*

(r) Taarifa ya Ukaguzi wa Ufanisi katika Udhibiti wa Utoaji wa Huduma za Afya kwenye Vituo Binafsi na vya Hiari *(Performance Audit Report on the Regulation of Private and Voluntary Healthcare Facilities)*

(s) Taarifa ya Ukaguzi wa Ufanisi kuhusu Udhibiti wa Malipo yaliyofanywa na Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya *(NHIF)* kwa Vituo vya Huduma za Afya *(Performance Audit Report on the Controls of Payments made by NHIF to Accredited Healthcare Facilities)*

(t) Taarifa ya Ukaguzi wa Ufanisi katika Usimamizi wa Hatua za Kutokomeza Ukatili dhidi ya Wanawake na Watoto nchini *(Performance Audit Report on the Management of Measures for Eliminating Violence against Women and Children in Tanzania)*

(u) Taarifa ya Ukaguzi wa Ufanisi kuhusu Uendeshaji na Matengenezo ya Miradi ya Usambazaji wa Maji *(Performance Audit Report on the Operation and Maintenance of Water Supply Schemes)*

(v) Taarifa ya Ukaguzi wa Ufanisi kuhusu Utekelezaji wa Mpango wa Umeme Vijijini *(Performance Audit Report on the Implementation of the Rural Electrification Programme)*.

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Waziri kwa uwasilishaji wa taarifa hizi muhimu. Tunaendelea, Katibu!

**NDG. EMMANUEL MPANDA – KATIBU MEZANI:**

**MASWALI NA MAJIBU**

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, maswali tutaanza na Ofisi ya Rais TAMISEMI, Mheshimiwa Mheshimiwa Deo Kasenyenda Sanga, Mbunge wa Makambako sasa aulize swali lake.

Na. 31

**Serikali kuangalia upya mipaka ya kiutawala**

**MHE. DEO K. SANGA** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itaangalia upya mipaka ya kiutawala ikiwemo na Halmashauri ya Mji wa Makambako?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI)** alijibu:-

Mheshimiwa spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, ninaomba kujibu

swali la Mheshimiwa Deo Kasenyenda Sanga, Mbunge wa Jimbo la Makambako, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali imekuwa ikizingatia suala la maendeleo ya mipaka ya maeneo ya utawala ili kuongeza ufanisi katika utendaji kazi na kusogeza huduma karibu na wananchi.

Mheshimiwa Spika, mabadiliko ya mipaka ya maeneo ya utawala kwa mujibu wa mwongozo wa uanzishaji wa maeneo ya utawala katika mamlaka za Serikali za Mitaa wa mwaka 2014 huanza na kusudio ambalo hupaswa kujadiliwa katika vikao vya Ngazi ya Halmashauri, Wilaya na Mkoa. Kusudio hilo huwasilishwa Ofisi ya Rais, TAMISEMI kupitia Katibu Tawala wa Mkoa.

Mheshimiwa Spika, Ofisi ya Rais, TAMISEMI bado haijapokea kusudio la kubadili mipaka kutoka Halmashauri ya Mji wa Makambako. Hivyo, endapo kuna uhitaji wa kubadili mipaka, inashauriwa kuanzisha kusudio na kuliwasilisha katika vikao vya Kamati ya Fedha, Uongozi na Mipango, Baraza la Madiwani, Kamati ya Ushauri ya Wilaya *(DCC)* na hatimaye katika Kamati ya Ushauri ya Mkoa *(RCC)*.

**SPIKA:** Mheshimiwa Deo Kasenyenda Sanga swali la nyongeza.

**MHE. DEO K. SANGA:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Serikali, nina maswali mawili ya nyongeza.

(a) Kwa kuwa, Serikali inakubaliana na mawazo ambayo wananchi wa Kijiji cha Mtewele na ndiyo wanahitaji kupata huduma Makambako kwa sababu kutoka Makambako kwenda kwenye Kijiji hicho ni kilometa nne tu na kutoka kwenye Kijiji kwenda kwenye Halmashauri yao ni kilometa 72. Je, Serikali inatuagiza nini ili tuweze

kufanikisha wananchi hawa kwa sababu wako tayari kurudi Makambako?

(b) Swali la pili. Kwa kuwa Kata ya Kivavi ni kata kubwa sana na kwa sababu Serikali inania ya kuwahudumia wananchi jirani na maeneo wanakokaa. Je, Serikali itakuwa tayari tuanzishe mpango wa kugawa Kata hiyo ya Kivavi?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI):** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Sanga kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kuhusu Kijiji hiki cha Mtewele kuwa kilometa Nne bado utaratibu ni uleule. Ni wao wenyewe kuanzisha mchakato sasa hapa inahusisha Halmashauri Mbili, kwa maana ya Wanging'ombe wakae kuridhia hili kwenye vikao vyao kama nilivyoeleza kwenye majibu yangu ya msingi na vilevile Halmashauri ya Mji wa Makambako nao waweze kupitia katika vikao vyao na waweze kuleta katika Ofisi ya Rais TAMISEMI ili mchakato huo uweze kuanza.

Mheshimiwa Spika, nikienda kwenye swali lake la pili nalo vilevile linafanana. Kata hii ya Kivavi kuigawa lakini nataka niongeze tu kidogo hapo. Kwa sasa Serikali imeweka kipaumbele katika kuendeleza maeneo yale ambayo yaligawiwa hivi karibuni na tumeona jitihada kubwa ya Serikali ninyi Wabunge ni mashahidi. Mheshimiwa Rais wetu Dkt. Samia Suluhu Hassan ametoa fedha nyingi sana kuhakikisha tunakamilisha majengo ya halmashauri, tunajenga nyumba za watumishi, tunajenga ofisi za Wakuu wa Wilaya. Kwa hiyo, kwa sasa kwanza kipaumbele kikubwa cha Serikali ni kuhakikisha tunaimarisha miundombinu kwenye maeneo ambayo yapo kwa sasa.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

**SPIKA:** Mheshimiwa Priscus Tarimo swali la nyongeza.

**MHE. PRISCUS J. TARIMO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. Naomba kuiuliza Serikali. Ni lini wataukwamua mchakato wa kuupanua Mji wa Moshi ambao ulishapita ngazi zote alizozitaja ikiwa ni pamoja na kupata *GN* Na. 19 ya tarehe 15 Julai, 2016?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI):** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Priscus Tarimo, Mbunge wa Moshi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kama ambavyo nilimalizia kusema hapa, kwa sasa kipaumbele cha Serikali kwanza ni kuhakikisha tunakamilisha ujenzi wa miundombinu mbalimbali ya maeneo ambayo yalikuwa yamekwisha megwa kupeleka huduma karibu ya wananchi. Baada ya hapo sasa tutaangalia mchakato huo mwingine wa kuweza kuendeleza maeneo kama ambavyo Mheshimiwa Tarimo amezungumza.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mwita Boniphace Getere swali la nyongeza.

**MHE. BONIPHACE M. GETERE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru.

Mheshimiwa Spika, Halmashauri ya Bunda iko Mwibara kilometa 72 kutoka kwenye Jimbo langu. Mwaka mmoja uliopita alikuja Mheshimiwa Rais pale tukamwomba majengo yaliyokuwa wazi Halmashauri ya Bunda yabaki kwenye Jimbo la Bunda ambalo huwa tunatembea umbali mrefu.

Je, ni lini Serikali sasa itateua Mkurugenzi kwenda kwenye majengo ambayo yako wazi ya Bunda ili kuwapa nafuu wananchi wa Jimbo la Bunda?

**SPIKA:** Mheshimiwa Mwita Getere nadhani swali lako lina mambo mengi. Ni kwamba hiyo Halmashauri ipo, lakini ngoja kwanza ili nielewe nijue Mheshimiwa Naibu Waziri anajibu nini. Halmashauri kwenye hilo Jimbo lako ipo ila Mkurugenzi hajateuliwa?

**MHE. BONIPHACE M. GETERE:** Mheshimiwa Spika, majengo yaliyokuwa Halmashauri ya Bunda yalihamishwa kwenda Mwibara Halmashauri mpya. Sasa kutoka Jimbo langu kwenda Mwibara ambako halmashauri mpya inaenda kujengwa ni kilometa 72 na majengo ya Bunda yaliyokuwa yametoka Halmashauri ya zamani yako wazi. Kwa hiyo, swala la msingi ni Serikali kuyaenzi yale majengo kwa kuteua Mkurugenzi mpya na Halmashauri kukendelea kuwepo hapo badala ya wananchi kwenda umbali ule.

**SPIKA:** Mheshimiwa sasa kama unaongelea uteuzi wa Mkurugenzi maana yake hayupo. Maana yake Mkurugenzi ateuliwe mwingine kwa ajili ya majengo. Kwa hiyo, majengo yasababishe Mkurugenzi mwingine ateuliwe?

Mheshimiwa Mwita nakupa nafasi uliza swali la nyongeza kwenye swali la msingi.

**MHE. BONIPHACE M. GETERE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru.

Je, ni lini Serikali kwa kuwa mchakato wa kupata Halmashauri ya Bunda ulishatekelezwa na tulishaandika, sasa ni lini Halmashauri ya Jimbo la Bunda itapata Halmashauri kutokana na umbali wa kutoka kwenye Jimbo langu kwenda kwenye Jimbo lingine?

**SPIKA:** Sasa ndiyo umeuliza swali. Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI):** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mwita Getere, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, michakato kufika TAMISEMI yote tunaikusanya na kama nilivyoeleza hapo awali bado kwa sasa kipaumbele kikubwa cha Serikali ni kuhakikisha tunakamilisha miundombinu katika Halmashauri ambazo zilikuwa ni mpya na Wilaya ambazo ni mpya, baada ya hapo sasa tutaanza kuangalia tena haya maeneo mengine ambayo Mikoa imepitisha na kuleta kwa Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais TAMISEMI.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge. Tunaendelea na Wizara ya Afya Mheshimiwa Felista Deogratius Njau, Mbunge wa Viti Maalum sasa aulize swali laki.

Na. 32

**Ajira kwa wanaojitolea katika hospitali nchini**

**MHE. FELISTA D. NJAU** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itawaajiri Wataalam wanaojitolea kwa muda mrefu kufanya kazi katika Hospitali mbalimbali nchini?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Afya naomba kujibu swali la Mheshimiwa Felista Deogratius Njau, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwenye hospitali zetu kumekuwa na watumishi wanaojitolea. Wizara imetoa Mwongozo wa kuwalipa nusu mshahara kwa mapato ya ndani. Hata hivyo hospitali zetu za Mikoa, Kanda na Taifa zimeweza kuwalipa hadi asilimia 40 ya watumishi wote wanaojitolea mshahara kamili kwa kutumia mapato ya ndani.

Mheshimiwa Spika, Wizara itashirikiana na Wizara ya Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora ili kuona namna bora ya kuwapa kipaumbele kwenye ajira watumishi ambao wamekuwa wakijitolea kwenye vituo vya huduma za Afya kuliko walioko nje wakisubiri ajira.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

**SPIKA:** Mheshimiwa Felista Njau swali la nyongeza.

**MHE. FELISTA D. NJAU:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Pamoja na majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri, nina maswali mawili madogo ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, mahitaji ya watumishi wa afya nchi nzima ni 336,453; waliopo ni 114,582 sawa na asilimia 34 tu na pungufu ni 221,946 upungufu huu ni mkubwa. Je, Serikali haioni umuhimu wa kuajiri watumishi hawa ili kunusuru afya za Watanzania?

Swali la pili, Serikali haioni umuhimu wa kutengeneza *database* ili kutambua wahudumu wote wanaojitolea ili wakati wa ajira waweze kupewa kipaumbele? Ahsante sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Swali la pili: Serikali haioni umuhimu wa kutengeneza *database* ili kutambua wahudumu wote wanaojitolea ili wakati wa ajira waweze kupewa kipaumbele? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa Mbunge, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza ni upungufu. Ni kweli tuna upungufu kwenye Sekta ya Afya na unachangiwa na mambo mengi. Wakati mwingine katika Hospitali ya Wilaya tumeweka idadi ya watumishi, Hospitali ya Mkoa tumeweka idadi ya watumishi, na Hospitali ya Kanda hivyo hivyo. Pamoja na hivyo, utakuta kwa mfano Hospitali ya Mawenzi wana watumishi 400 lakini pale Mwananyamala hospitali, wanaona wagonjwa 500 kwa siku; ukienda pale Mnazi Mmoja Dar es Salaam ambayo ni ya Wilaya wana watumishi 170 wanaona wagonjwa 700 mpaka 800 kwa siku. Maana yake ni nini?

Mheshimiwa Spika, tukienda kwenye eneo la kuangalia ni watu wangapi hospitali husika inaona wagonjwa kwa siku na tukaweza kupeleka watumishi kulingana na mzigo ulioko kwenye eneo, hata huo upungufu anaousema Mheshimiwa Mbunge haupo.

Mheshimiwa Spika, tulikwenda Wilaya moja kule Shinyanga wakasema wana upungufu katika Hospitali ya Wilaya. Nilipowauliza, wakasema tuko 37. Ni kweli ukiwasikia Hospitali ya Wilaya wako 37, utasema kwamba ni wachache sana, lakini nikawauliza mnaona wagonjwa wangapi kwa siku? Wakaniambia tunaona wagonjwa 13. Unaweza ukaona kwamba kuna umuhimu wa kufikiria. Hilo moja, ni kwamba linatakiwa lifanyiwe kazi, kuangalia hali halisi na kupeleka watumishi kulingana na mzigo.

Mheshimiwa Spika, la pili, lile la kuweka *database,* ndicho nilichokisema hapa, tutashirikiana na wenzetu wa Utumishi kuona namna nzuri tutakayofanya na kuweka *database* kama alivyoshauri Mheshimiwa Mbunge ili tuweze kuwatambua wakati wa ajira wapewe kipaumbele. Hilo ni wazo zuri sana, tunalichukua na tunakupongeza Mheshimiwa Mbunge.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, tunakushukuru kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge. Mheshimiwa Waziri wa Afya na Waziri wa TAMISEMI nafikiri kuna haja ya kukaa na Ofisi ya Rais, Utumishi na Utawala Bora, kwa sababu watumishi wa afya wanaojitolea na waalimu wanaojitolea kwa Shule za Msingi na Sekondari, huwa haipendezi sana yaani kwamba wao ndio huwa hawana sifa za ajira! Yaani kwa sababu ajira zikitangazwa, wale wote wanaojitolea unakuta kwenye eneo lako hakuna hata mmoja aliyepata. Sasa huwa tunajiuliza, kama wale wanaojitolea huwa hawana sifa, waliokaa nyumbani wanaomba kazi ndio wana sifa kuwazidi hao wengine! *(Makofi)*

Nafikiri mtengeneze utaratibu mzuri uli kila mwaka muwe mnapata taarifa za wale wanaojitolea, ili ajira zinapopatikana mzitumie taarifa hizo kuwapa wao kipaumbele. Nafikiri hilo litatupunguzia changamoto hasa kipindi hiki ambacho majengo mengi yanajengwa kwenye afya na elimu, ni muhimu sana wale wanaojitolea kupewa kipaumbele. *(Makofi)*

Kwa kusema hayo, tunaendelea na Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Mheshimiwa Justin Lazaro Nyamoga, Mbunge wa Kilolo, sasa aulize swali lake.

Na. 33

**Kufuta hati ya umiliki shamba lililotelekezwa – Kilolo**

**MHE. JUSTIN L. NYAMOGA** aliuliza:-

Je, kuna mpango gani wa kufuta Hati ya Umiliki wa Shamba la Mwekezaji katika Kijiji cha Mawalla - Kilolo ambalo limetelekezwa?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Mheshimiwa Pinda, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Justin Lazaro Nyamoga, Mbunge wa Kilolo, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, shamba lililotelekezwa katika Kijiji cha Mawalla, ni shamba lenye Hati Na.16633 lenye ukubwa wa ekari 639 ambalo linamilikiwa na Ndugu Mbaraka Mazrui. Mmiliki wa shamba hili alitelekeza shamba tangu mwaka 1980. Halmashauri ya Wilaya ya Kilolo kwa kushirikiana na Ofisi ya Kamishna wa Ardhi Msaidizi wa Mkoa wa Iringa, imelitambua shamba hili kama shamba lililotelekezwa.

Mheshimiwa Spika, kufuatia hali hiyo, Serikali imeanza hatua za awali za ubatilishaji wa shamba husika na pindi hatua hizo zitakapokamilika, mapendekezo yatawasilishwa kwa mamlaka husika kwa ajili ya ubatilishaji.

**SPIKA:** Mheshimiwa Justin Lazoro Nyamoga, swali la nyongeza.

**MHE. JUSTIN L. NYAMOGA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru. Pamoja na majibu mazuri ya Serikali, nina maswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza: Serikali haioni haja ya kufanya tathmini ya mashamba yote yaliyotelekezwa na kupata orodha yake ili taratibu za kubatilisha ziweze kufanyika katika Wilaya ya Kilolo?

Mheshimiwa Spika, swali la pili, hili shamba limetelekezwa tangu mwaka 1980, lakini hadi sasa halijaweza kubatilishwa: Je, Serikali haioni umuhimu wa kulibatilisha kwa haraka ili liweze kukabidhiwa kwa Halmashauri na kupangiwa matumizi mengine ili wananchi waweze kunufaika? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI** Mheshimiwa Spika, ahsante. Naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Justin Lazaro Nyamoga, Mbunge wa Kilolo, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, mashamba ambayo yametelekezwa kwa muda mrefu ni mamlaka za Halmashauri kubaini hayo maeneo na kuyaanzia michakato ya kuomba yabatilishwe. Hivyo, nitoe wito kwenye Halmashauri zote hapa nchini, kupitia maeneo ambayo yamesahauliwa na wale ambao walimilikishwa huko nyuma ili sasa hii michakato ya haraka iweze kufanyika na kubadili yale matumizi ya maeneo kupitia hizi mamlaka za juu.

Mheshimiwa Spika, nikijibu swali la pili, kwa kuwa jambo hili lilichukua muda mrefu, kama nilivyosema mwanzo, inawezekana Halmashauri ilikuwa haijabainisha na kuanza ile michakato, lakini kwa sasa kwa hatua tulipofikia, hili jambo linakwenda kukamilika kwa sababu mwenye maamuzi ya mwisho katika ubatilishaji wa maeneo haya ya ardhi ni Mheshimiwa Rais. Kwa hiyo, tutakapomfikishia, tunaamini

wazi kwamba atalitolea maamuzi ya haraka kadri inavyowezekana, ahsante.

**SPIKA:** Ahsante sana, Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Wizara ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara Mheshimiwa Kavejuru Eliadory Felix, Mbunge wa Buhigwe, sasa aulize swali lake.

Na. 34

**Viwanda vya kuchakata mazao ya uvuvi Ziwa Victoria na Tanganyika**

**MHE. KAVEJURU E. FELIX** aliuliza:-

Je, Serikali ina mkakati gani wa kuongeza viwanda vya kuchakata mazao ya uvuvi katika Ziwa Victoria na Tanganyika?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Uwekezaji, Viwanda na Biashara, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UWEKEZAJI, VIWANDA NA BIASHARA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Kwa niaba ya Waziri wa Uwekezaji, Viwanda na Biashara, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Kavejuru Eliadory Felix, Mbunge wa Jimbo la Buhigwe, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali ina Mkakati wa Kuendeleza Sekta ya Uvuvi 2022/2023 – 2025/2026, pia Mkakati wa Taifa wa Kuendeleza Ukuzaji Viumbe kwenye Maji 2018 – 2025, na Mpango Kabambe wa Sekta ya Uvuvi 2021/2022 –2036/2037 ambayo imelenga kuongeza viwanda vya kuchakata mazao

ya uvuvi kupitia Mkakati Jumuishi wa Kuendeleza Viwanda Nchini.

Mheshimiwa Spika, kupitia mikakati hiyo, Serikali imeendelea kuboresha miundombinu ya uvuvi na viwanda na uboreshaji wa mazingira ya ufanyaji biashara na uwekezaji ambayo utekelezaji wake utaendelea kuvutia uwekezaji wa viwanda vya kuchakata mazao ya uvuvi nchini ikiwa ni pamoja na eneo la Ziwa Victoria na Tanganyika.

**SPIKA:** Mheshimiwa Kavejuru, swali la nyongeza.

**MHE. KAVEJURU E. FELIX:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Serikali, nina maswali mawili ya nyongeza.

Moja, kwa kuwa upatikanaji wa malighafi kwa ajili ya viwanda vya kuchakata na kusindika mazao ya uvuvi vimepungua; mazao hayo ya uvuvi na malighafi yanapungua, hayakidhi mahitaji ya viwanda: Je, Serikali ina mpango gani wa kuboresha vyombo na zana za uvuvi ili kuongeza ufanisi na tija? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, swali la pili, kwa kuwa kuna upotevu mkubwa wa mazao ya uvuvi baada ya kuvunwa: Je, Serikali itasaidiaje kusambaza teknolojia rahisi za usindikaji wa mazao ya uvuvi ili kuyaongezea thamani kwa wavuvi wadogo wadogo? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UWEKEZAJI, VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Kavejuru Eliadory Felix, Mbunge wa Jimbo la Buhigwe, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli moja ya changamoto tuliyonayo katika sekta ya viwanda ni ukosefu wa malighafi

ambazo zinahitajika katika viwanda ambavyo vimepelekea baadhi ya viwanda kufungwa. Moja ya mikakati ya Serikali ambayo inatekelezwa kwenye mipango hii niliyoitaja ni kuwawezesha wavuvi na wenye viwanda kutumia teknolojia nzuri ya kisasa ambayo itapelekea kuvuna Samaki wanaohitajika katika viwanda badala ya kuvuna na wale madogo kwa maana ya makokoro ambayo yanatumika kuvuna hata mazalia.

Mheshimiwa Spika, pili, tuna mikopo mbalimbali, moja ni hii ya Halmashauri na pia kupitia taasisi zetu kama *SIDO* ambayo inawawezesha wavuvi kupata mikopo hiyo ili waweze kupata teknolojia za kisasa za kuvuna au kuvua samaki katika maeneo hayo. Kwa hiyo, Serikali inaendelea kuwawezesha wavunaji au wavuvi ili waweze kupata teknolojia za kisasa kupitia mikopo.

Mheshimiwa Spika, pili, kwenye upotevu; ni kweli moja ya changamoto iliyopo ni upotevu wa mazao yanayotokana na uvuvi baada ya kuvunwa. Mara baada ya kuvua Samaki wanapotea au wanaoza. Moja ya maeneo, tunajenga *industrial pack* au kongani ambazo zitasaidia kuwa na maeneo maalum ya kutunzia Samaki ikiwa pamoja na kuvutia wawekezaji wa viwanda ili kuhakikisha mavuno yanayotoka baharini au kwenye maziwa yanaenda moja kwa moja kwenye viwanda ili kuchakatwa kabla ya kuharibika.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru.

**SPIKA:** Mheshimiwa Saashisha Mafuwe, swali la nyongeza.

**MHE. SAASHISHA E. MAFUWE:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi. Kwa kuwa Miwanda cha *Kilimanjaro Machine tools* kimeshaanza kufanya kazi na **mashine** imeshakamilika: Je, Serikali ina mpango gani sasa kuagiza

taasisi zake zianze kununua vyuma pale na vipuri mbalimbali ili kuimarisha kiwanda hicho?

**SPIKA:** Mheshimiwa Saashisha, hicho kiwanda kinatengeneza pia vifaa kwa ajili ya uvuvi ili niweze kulihusisha swali lako na swali la msingi?

**MHE. SAASHISHA E. MAFUWE:** Mheshimiwa Spika, linatengeneza vipuri vya kila aina pamoja na vya uvuvi.

**SPIKA:** Naona Mheshimiwa Naibu Waziri ametikisa kichwa kuashiria swali lako liende kama swali la msingi. Mheshimiwa Abubakar Asenga, swali la nyongeza.

**MHE. ABUBAKAR D. ASENGA:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Kama ilivyokuwa *machine tools* ya kwao, Mheshimiwa Waziri alitembelea Kiwanda cha *Mang'ula Machine Tools* cha Kilombero, nacho akaahidi kwamba kitafufuliwa hivi karibuni ili kiendelee kutengeneza *spare* za viwanda mbalimbali: Je, ni lini ufufuaji wa kiwanda cha *Mang'ula Machine Tools* utaanza ili iwasaidie na wavuvi? *(Makofi)*

**SPIKA:** Haya, nawe utapeleka swali la msingi au lolote litakalowahi mmoja wenu atauliza swali la nyongeza. Mheshimiwa Ester Bulaya, swali la nyongeza.

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Jimbo la Bunda Mjini, limetenga eneo la Kata ya Mgeta kwa ajili ya Ukanda wa Uwekezaji, mpaka sasa hivi hawajawekeza; na Bunda pia tunavua: Kwa nini sasa Wizara isione kwamba kuna haja ya kujenga kiwanda kwa ajili ya vifaa vya uvuvi? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ujenzi wa Kiwanda cha Vifaa vya Uvuvi. *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA UWEKEZAJI, VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Kwa niaba ya Waziri wa Uwekezaji, Viwanda na Biashara, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Ester Bulaya, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli, kama nilivyosema kwenye jibu la msingi moja juu ya changamoto tulizonaao: Kwanza, ni mazao yenyewe yanayotokana na uvuvi kupungua; pili, kukosekana kwa viwanda ambavyo vinazalisha vifaa vya uvuvi ambavyo ndiyo teknolojia mahususi ambayo itapelekea kuvua kwa ubora zaidi mazao ya samaki.

Mheshimiwa Spika, katika mikakati ambayo tunaendelea nayo ni kuvutia wawekezaji kujenga viwanda vya kuchakata, lakini pia naamini tukifanikiwa hilo, hatua inayofuata nadhani ni kuweka sasa viwanda ambavyo vinazalisha vipuri vitakavyoweza kuzalisha zana za kuvuali Samaki katika sekta hii ya uvuvi. Kwa hiyo, nachukua hili kama sehemu ya changamoto na juhudi zetu kama Serikali, kuvutia zaidi wawekezaji katika viwanda vya kuzalisha vifaa vya kuvulia samaki katika maeneo mbalimbali hapa nchini. Nakushukuru.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri ahsante sana kwa majibu yako kwa Waheshimiwa Wabunge.

Wizara ya Fedha na Mipango, Mheshimiwa Innocent Edward Kalogeris, Mbunge wa Morogoro Kusini sasa aulize swali lake.

Na. 35

**Kuruhusu Mabenki kuwa Wakala wa Bima**

**MHE. INNOCENT E. KALOGERIS** aliuliza:-

Je, kuruhusu Benki kuwa Wakala wa Bima Serikali haioni kuwa Mawakala wengine watafunga biashara kwa kukosa wateja?

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango, majibu.

**WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Innocent Edward Kalogeris, Mbunge wa Morogoro Kusini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Mamlaka ya Usimamizi wa Bima Tanzania *(TIRA)* pamoja na wadau wa bima ilianzisha BenkiWakala wa Bima ili kuongeza wigo wa usambazaji na upatikanaji wa huduma za bima kwa wananchi. Idadi ya Mawakala wa Bima wa Kawaida imekuwa ikiongezeka sambamba na BenkiWakala wa Bima kwa sababu hali hii imechochea ushindani, ubunifu na kutegemeana. Takwimu zinaonesha BenkiWakala waliosajiliwa kwa mwaka 2020 wako 14; mwaka 2021 wako 23; mwaka 2022 wako 27; na hadi 30 Machi, 2023 walishafika 30. Aidha, Mawakala wa Bima wa Kawaida waliosajiliwa kwa mwaka 2020 walikuwa 745; mwaka 2021 walikuwa 789; mwaka 2022 walikuwa 910; na kwa mwaka 2023 hadi Machi, 2023 wameshafika 960.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa takwimu hizi, ni dhahiri kuwa Mfumo wa BenkiWakala wa Bima umesaidia kukuza biashara ya Bima hapa nchini.

**SPIKA:** Mheshimiwa Innocent Edward Kalogeris, swali la nyongeza.

**MHE. INNOCENT E. KALOGERIS:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Serikali, nina maswali mawili ya

nyongeza. Kiuhalisia, ongezeko la Mawakala wa Bima linatokana na vijana wengi waliomaliza elimu ya fani ya bima nchini kuamua kujiajiri wenyewe baada ya kukosa kazi Serikalini:-

Mheshimiwa Spika, je, ni utafiti gani wa kina ambao umefanyika na Serikali hadi kujua kwamba ongezeko hilo linatokana na mfumo wa biashara ya bima kukua?

Mheshimiwa Spika, je, ni utafiti gani ambao mmeufanya katika kujua mawakala vijana ambao wamefunga biashara baada ya kushindwa biashara kutokana na ushindani mkubwa wa biashara ya bima ambao umevamiwa na benki pamoja na kampuni za simu? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Spika, namshukuru na kumpongeza Mheshimiwa Mbunge kwa maswali mazuri. Moja, hivi tunavyoongea mpaka sasa, upande wa masuala haya ya bima hapa nchini ziko takribani asilimia 16 tu, ndiyo tunapata ushiriki wa vijana ambao wako chini ya umri wa miaka 18 na utafiti huo uliofanywa na *Finscope* ulionesha hivyo. Sasa katika nchi ambazo zimeendelea na kule tunakoelekea tunatamani angalau tufike asilimia 84 au zaidi ya hapo.

Mheshimiwa Spika, kuhusu utafiti wa mawakala, taarifa ambazo zilikusanywa kwa miaka kadhaa kama nilivyotoa pale mwanzo, zinaonesha kwa mwaka 2020 walikuwa zaidi ya 700, lakini kwa sasa tumeshazidi 930. Kama tumeshazidi 930 hii inaonesha kwamba bado pana fursa ambapo vijana wote wanaweza wakashiriki na bado mafanikio yakapatikana bila wao kuzuiliwa kwa sababu ya uwepo wa BenkiWakala.

Mheshimiwa Spika, hivyo hivyo, *TIRA* ilishatoa mwongozo ambao unaweka mipaka ambayo inaonesha ni namna gani italinda BenkiWakala zisilete athari kwa Mawakala hawa wa kawaida ambao wanaendesha shughuli hizo. Tunaamini kwamba biashara hiyo itaendelea kusambaa zaidi kwa wananchi walio wengi zaidi. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Waheshimiwa Wabunge, sasa tunajielekeza katika Wizara ya Kilimo, na swali hili ni la Mheshimiwa Reuben Nhamanilo Kwagilwa. Nimeletewa taarifa hapa mbele kwamba inabidi lijibiwe na Wizara ya Maji badala ya Wizara ya Kilimo. Swali namba 36 la Mheshimiwa Reuben Nhamanilo Kwagilwa litapelekwa Wizara ya Maji. Inaonekana baada ya kufanya huo uhariri imelifanya swali lipelekwe kwenye Wizara ambayo haihusiki na swali hilo.

Inaonekana katika uhariri baada ya kufanya huo uhariri imelifanya swali lipelekwe kwenye Wizara ambayo haihusiki na swali hilo la Mheshimiwa Mbunge. Kwa hivyo kuliko kuyasikiliza majibu halafu yakaonekana hayajajibu lile swali alilokuwa ameliuliza Mheshimiwa Mbunge hilo swali litapangiwa katika ratiba zinazofuata ili lipelekwe Wizara ya Maji, halafu Wizara ya Maji wawezi kuleta majibu kwa kadri ya swali linavyotaka kwa muktadha huo swali la 36 leo litaondolewa kwenye orodha ya maswali yaliyoulizwa. *(Makofi)*

*(Hapa Swali Na. 36 liliondolewa kwenye Orodha ya Maswali)*

**SPIKA:** Tunaelekea Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi Mheshimiwa Neema William Mgaya Mbunge wa Viti Maalum sasa aulize swali lake.

Na. 37

**Ujenzi wa Barabara ya Njombe – Ludewa – Itoni - Manda**

**MHE. NEEMA W. MGAYA** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itakamilisha Ujenzi wa Barabara ya Njombe – Ludewa – Itoni hadi Manda kwa kiwango cha lami?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI NA (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Neema William Mgaya, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali inaendelea na ujenzi kwa kiwango cha zege wa Barabara ya Itoni - Ludewa hadi Manda yenye urefu wa kilomita 211.42. Ujenzi kwa kiwango cha zege wa sehemu ya Lusitu – Mawengi kilomita 50 umekamilika na ujenzi wa sehemu ya Itoni – Lusitu kilomita 50 unaendelea.

Mheshimiwa Spika, ujenzi wa sehemu zilizobaki utaendelea kwa awamu kulingana na upatikanaji wa fedha, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Neema William Mgaya, swali la nyongeza.

**MHE. NEEMA W. MGAYA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi kuweza kuuliza swali la nyongeza. Barabara ya Njombe – Itoni, watu bado hawajalipwa *compensations* nilipenda kujua lini watalipwa fidia wakazi

hao? Lakini kibaya zaidi Mawengi – Mlangali tayari barabara imejengwa lakini kuna baadhi ya watu bado hawajalipwa fidia lini watalipwa? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, swali langu la pili naomba kujua barabara ya Makete – Mbeya mkandarasi ameisha saini mkataba lakini mpaka hivi sasa tunavyozungumza hajafika *site* lini atafika *site* na ujenzi wa barabara hii ukaendelea? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Neema William Mgaya Mbunge kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, nataka nimuhakikishie Mheshimiwa Mbunge na wananchi ambao ameuliza kwamba hawajalipwa fidia kwa eneo la Mawengi – Mlangali nataka nimuhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali imeisha andaa na kukamilisha Jedwali la malipo ya hao watu wenye fidia wa Mawengi pamoja na hawa wa Itoni – Lusitu na zoezi la kuwalipa nataka nimuhakikishie Mheshimiwa Mbunge litafanyika muda si mrefu.

Mheshimiwa Spika, nakuhusu suala la barabara ya Makete – Isyonje mkandarasi alishapatikana ameisha onyeshwa *site* lakini kinachosumbua kwasasa kuanza yupo kwenye *mobilizations* ni hali halisi ya hewa kwa maana ya mvua nyingi inayoendelea lakini tayari mkandarasi ameishapatikana na ameisha kabidhiwa *site,* ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Stanslaus Shing'oma Mabula swali la nyongeza.

**MHE. STANSLAUS S. MABULA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Kwa kuwa usanifu wa ujenzi wa barabara ya Kenyatta kutoka Mwanza Mjini kwenda Buhongwa – Usagara na *Airport* – Nyanguge zimeishakamilika ni lini ujenzi huu utaanza mara moja?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mabula Mbunge wa Nyamagana kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli Serikali hazma yake ni kuijenga hii barabara na kuipanua lakini tayari tumeisha kamilisha usanifu na sasa hivi tunaendelea kutafuta fedha. Nimuombe Mheshimiwa Mbunge avute subira kwa sababu ndiyo tunaelekea kwenye bajeti tuone Serikali imepanga nini kwenye hiyo barabara, ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa David Kihenzile swali la nyongeza.

**MHE. DAVID M. KIHENZILE:** Mheshimiwa Spika, ahsante, pamoja na kupitisha kwenye bajeti hii inayoendelea lakini bado barabara ya Mafinga – Mgololo na Mgololo – Mtwango hazijaanza kujengwa. Je, ni lini sasa Serikali itaanza ujenzi wa barabara hizi?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa David Kihenzile Mbunge wa Mufindi Kusini kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, barabara hii ilipangiwa bajeti. Nataka nimuhakikishie Mheshimiwa Mbunge pamoja na wananchi wa Jimbo la Mufindi Kusini kwamba tayari mkandarasi alishapatikana na kinachomsumbua pia kuanza hii kazi ni kwa sababu tu ya hali ya hewa na Mheshimiwa Mbunge nilishamuhakikishia yeye mwenyewe kwamba tayari tumeisha mpata mkandarasi na tayari ameishaandaa vifaa lakini hawezi kuanza kwa kweli ujenzi kwa mazingira ya Jimbo lake lina mvua nyingi sana lakini mara tu mvua itakapokatika mkandarasi ataanza kujenga kwa kiwango cha lami kwa bajeti ambayo tulikuwa tumeipanga kwa mwaka huu unaoendelea, ahsante sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Iddi Kassim Iddi

**MHE. IDDI K. IDDI:** Mheshimiwa spika, ahasante sana, kwa kuwa marudio ya upembuzi yakinifu wa barabara inayotoka Bulyanhulu kwenda Kahama umekamilika, vikao vya tathimini vimekamilika, vikao vya Kata zote vimekamilika, fedha zipo *cash*.

**SPIKA:** swali, swali.

**MHE. IDDI K. IDDI:** Ni lini sasa Wizara itaanza ujenzi wa barabara hiyo?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Idd Kassim Mbunge wa Msalala kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, barabara ya Bulyanhulu kwenda Kahama kama alivyosema nikweli usanifu ulishakamilika na fedha ipo sasa hivi kinachoandaliwa ni makabrasha tu kwa ajili ya kuanza kuitangaza hiyo barabara ili ianze kujengwa

kwa kiwango cha lami ikiwa ni pamoja na kusaidiana na wenzetu wa Twiga kwa maana ya Barrick, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Aida Khenani swali la nyongeza.

**MHE. AIDA J. KHENANI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipatia nafasi niulize swali la nyongeza. Barabara kutoka Mji wa Namanyere – Bandari ya Kipili ni lini itaanza kujengwa kwa kiwango cha lami?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Aida Khenani Mbunge wa Nkasi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, barabara aliyoitaja amekuwa anaulizia mara kwa mara na mwaka huu tuliipangia fedha na tulishawaambia mameneja wa Mkoa watangaze kwa gharama ile ambayo imepangiwa ili ianze kujengwa hata kama itajengwa kilomita moja, mbili lakini wazitangaze. Kwa hiyo, nataka nichukue nafasi hii kumkumbusha meneja wa Mkoa wa Rukwa aweze kufanya kama alivyopokea maagizo ya kuzitangaza hizi barabara, ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Omari Kigua swali la nyongeza.

**MHE. OMARI M. KIGUA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana, barabara ya Handeni – Kiberashi – Singida ni barabara muhimu sana na barabara hii nashukuru mkandarasi alikwisha ripoti *site* lakini kinachoendelea sasahivi ni kwamba kama vile kazi aiendelei Je, tatizo liko wapi? Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Kigua Mbunge wa Kilindi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, bahati nzuri wiki iliyopita nimetembelea barabara hii kuangalia changamoto ni nini? Mkandarasi yupo *site* ameishaanza kazi anakamilisha majengo ya Muhandisi mshauri na kulikuwa na changamoto ndogo ambazo tumeisha zi-*sort out* na tayari nataka nimuhakikishie Mheshimiwa Mbunge kuanzia wiki inayoanza hii kasi itaongezeka kwa hiyo barabara inaendelea. Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa David Cosato Chumi, swali la nyongeza, oooh! Mheshimiwa Daniel Baran Sillo swali la nyongeza.

**MHE. DANIEL B. SILLO:** Mheshimiwa Spika, ahsante, barabara ya Dareda – Dongobesh – Usariva usanifu wa kina umeishafanyika na zabuni kutangazwa Je, ni lini barabara hii itaanza kujengwa kwa kiwango cha lami?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Sillo Mbunge wa Babati Vijijini kama Ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, barabara imeishatangazwa na ipo kwenye hatua ya manunuzi kwa hiyo, sasa hivi kuna majadiliano yanayoendelea na mkandarasi ambazo ni taratibu za kawaida za manunuzi. Kwa hiyo, nimuhakikishie Mheshimiwa Mbunge barabara hii mara tutakapokamilisha hayo majadiliano mkandarasi tukishakubaliana atakabidhiwa *site* ili aendelee na ujenzi, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Hassan Zidadu Kungu swali la nyongeza.

**MHE. HASSAN Z. KUNGU:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipatia nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Je, ni lini Serikali itapeleka fedha za kujenga barabara kwa kiwango cha lami katika Wilaya ya Tunduru ambapo taasisi zote za Serikali zipo katika barabara hiyo?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Kungu Mbunge wa Tunduru Mjini kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kama ni barabara za *TANROADS* zinapita tuna mpango wa kuhakikisha katika kila Miji hasa ya Makao Makuu ya Wilaya, ambapo barabara zetu zinapita basi zijengwe kwa kiwango cha lami. Nimuombe Mheshimiwa Mbunge mara baada ya hapa tuweze kuonana kama barabara zetu zipo zinapita katikati ya taasisi hizo ambazo amezisema ili tuweze kuona utaratibu wa namna ya kuzijenga kwa kiwango cha lami katika hayo maeneo aliyoyataja, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Twaha Mpembenwe swali la nyongeza.

**MHE. TWAHA A. MPEMBENWE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwakunipa nafasi kuuliza swali la nyongeza. Barabara ya Kibiti – Dimani – Mloka iko ndani ya Ilani ya Chama cha Mapinduzi (CCM); je, lini Serikali wataanza mchakato wa kuitengeneza barabara hiyo?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Twaha Mpenbenwe Mbunge wa Kibiti kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kama alivyosema ipo kwenye Ilani na Serikali kwakweli inaendelea kutafuta fedha kwa barabara hii ili iweze kuijenga kwa kiwango cha lami, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Vita Kawawa swali la nyongeza.

**MHE. VITA R. KAWAWA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana, kwetu tuna barabara ya Mtwara – Pachani – Mkongo – Lusewa – Magazini – Nalasi na Mheshimiwa Naibu Waziri ulikuja kuitembelea na ina hali mbaya sana mpaka sasa hivi na uliwahaidi wazee wale kwamba itatengenezwa kwa kiwango cha lami Je, unawaeleza nini leo Mheshimiwa Naibu Waziri? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Vita Kawawa Mbunge wa Namtumbo kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli tulitembelea hii barabara ndefu yenye kilomita 300 tumemuagiza meneja wa Mkoa wa Ruvuma kwanza kuhakikisha anaainisha maeneo yote korofi ili yaweze kupata bajeti wakati Serikali inaendelea kutafuta fedha kuijenga hii barabara kwa kiwango cha lami.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nimuhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba tayari tumeishaongea na meneja wa Mkoa aangalie maeneo yote ambayo ni korofi ambayo tunaweza tukayadhibiti kwa muda wakati tunatafuta fedha ya kuijenga barabara yote kwa kiwango cha lami, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Charles Kimei, swali la nyongeza.

**MHE. DKT. CHARLES S. KIMEI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana, barabara ya Chekeleni – Kahe – TPC – na Mabogini iko kwenye Ilani awamu hii na awamu iliyopita na pia ni ahadi ya Viongozi Wakuu wa Serikali. Nataka kujua ni lini Serikali itaanza sasa kujenga barabara hii kwa kiwango cha lami kama ilivyoahidiwa? Natumaini hatasema kwamba ni mpaka hela ipatikane.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Kimei Mbunge wa Vunjo kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kama alivyosema ni ahadi ya viongozi lakini pia iko kwenye ilani naomba nimuhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali itaendelea kutafuta fedha kwa ajili ya kujenga barabara zote ambazo imeziaidi kuzijenga kwa kiwango cha lami ikiwa ni pamoja na barabara ambayo Mheshimiwa Mbunge wa Vunjo ameitaja.

Mheshimiwa Spika, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Tabasam Hamis Mwagao swali la nyongeza.

**MHE. TABASAM H. MWAGAO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kunipa nafasi, Mheshimiwa Naibu Waziri ulikuja Sengerema uliona kivuko chetu cha Buyabu – Mbalika mikataba ipo tayari na barabara yetu ya Sengerema – Buchosha mikataba ipo tayari lini utakuja kusaini mikataba hiyo ili tuondokane katika hadha tuliyonayo kwa huko kwetu Sengerema? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Tabasam hilo litaulizwa kama swali la msingi. Mheshimiwa Jafari Chege swali la nyongeza.

**MHE. JAFARI W. CHEGE:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi barabara ya Utegi – Shilati – Kilongwe yenye kilomita 56 upembuzi yakinifu umekwisha kamilika Mheshimiwa Waziri ni lini sasa barabara hii itajengwa kwa kiwango cha lami?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Jafari Chege Mbunge wa Rorya kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, barabara aliyoitaja nikweli ipo kwenye Ilani na imeahidiwa kujengwa kwa kiwango cha lami. Naomba nimuombe Mheshimiwa Mbunge asubiri bajeti hii tutakayosoma tutakuwa tumependekeza nini kuhusu barabara hii ya kutoka Mika – Utegi – Ruari hadi Kirongwe, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Benaya Kapinga swali la nyongeza.

**MHE. BENAYA L. KAPINGA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kuniona, Barabara ya Nyoni – Mlima mkali wa Mawono – Mapela – Maguu kilomita 25 ipo kwenye Ilani ni lini sasa barabara hii itaanza ujenzi?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Kapinga Mbunge wa Mbinga kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, barabara aliyoitaja ipo kwenye miinuko na tunachofanya kwa sasa nikuhakikisha kwamba inapitika kwa muda wote wakati tukifanya hivyo Serikali inaendelea kutafuta fedha ili kuweza kuijenga kwa kiwango cha lami, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mhandisi Stella Martin Manyanya Mbunge wa Nyasa sasa aulize swali lake.

Na. 38

**Kutatua kero ya barabara ya Nyoni hadi Mitomoni – Nyasa**

**MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itajenga barabara ya Luhindo hadi Ndondo katika barabara Kuu ya Nyoni hadi Mitomoni Wilayani Nyasa ?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE)** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa *Eng.* Stella Martin Manyanya, Mbunge wa Nyasa kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2022/2023 Serikali imetenga kiasi cha shilingi bilioni 1.046 kwa ajili ya matengenezo mbalimbali kwenye barabara ya Nyoni - Liparamba hadi Mitomoni. Tayari Mkandarasi yupo eneo la kazi akiendelea na kazi za matengenezo ambapo katika sehemu korofi zenye miinuko na miteremko mikali anazijenga kwa zege na kuweka makalvati maeneo kadhaa. Kazi hizi zinategemewa kukamilika tarehe 30 Juni, 2023, ahsante.

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Manyanya swali la nyongeza.

**MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA:** Mheshimiwa Spika ahsante sana, kwanza napenda kushukuru kwa majibu ya mazuri ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, kufuatia umuhimu wa barabara hii ya Nyoni – Mitomoni kiuchumi Serikali ina mpango gani wa kuanza kufanya upembuzi yakinifu kwa ajili ya ujenzi kwa kiwango cha lami. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, swali la pili, kwa kuwa Waheshimiwa Wabunge wa Mkoa wa Ruvuma wamekuwa wakilia, wakipiga magoti humu Bungeni kufuatia changamoto kubwa ya kuvuka katika Mto Ruvuma ulioko Mitomoni ili kutuunganisha na barabara ya Likwilifusi – Mkenda. Je, Serikali ina mpango gani wa kuanza kujenga daraja hili kufuatia kilio kikubwa cha wananchi hao? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Stella Martin Manyanya Mbunge wa Nyasa kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, nikweli daraja la Mitomoni ni muhimu sana kwa wananchi wa Jimbo la Nyasa nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba tayari tumeishapata mkandarasi na sasa hivi tuko kwenye hatua za mwisho za manunuzi ili mkandarasi aweze kuanza kazi hiyo kwenye kujenga hilo daraja ambalo litagharimu si chini ya bilioni 22. Kwa hiyo, tupo kwenye hatua za mwisho kabisaa za manunuzi kwahiyo daraja hilo litajengwa.

Mheshimiwa Spika, kuhusu kuifanyia upembuzi yakinifu na usanifu wa kina barabara hiyo, Meneja wa Mkoa wa Ruvuma alishaagizwa aweze kufanya tathmini, kufanya makadirio ya gharama ambazo zinaweza kuwa kwa ajili ya kuifanyia hiyo barabara upembuzi na usanifu wa kina wa hiyo barabara, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Innocent Bilakwate, swali la nyongeza.

**MHE. INNOCENT S. BILAKWATE:** Mheshimiwa Spika, ahsante kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Barabara ya Omulushaka Kwenda mpaka Mlongo mkandarasi ameshapatikana tangu mwaka jana, lakini mapaka leo mkataba bado haujasainiwa. Tatizo liko wapi ili mkataba uweze kusainiwa na mkandarasi aweze kuanza kazi?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Innocent Bilakwate, Mbunge wa Kyerwa, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, Barabara ya Olumushaka kwenda hadi Mlongo tayari mkandarasi alishapatikana, na hatua ambayo imebaki sasa ni hatua ya kusaini mkataba ili mkandarasi aweze kukabidhiwa *site;* na tutaanza kujenga kilomita 50, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Zuena Athumani Bushiri, swali la nyongeza.

**MHE. ZUENA A. BUSHIRI:** Mheshimiwa Spika, ahsante na mimi kunipa nafasi kuuliza swali la nyongeza.

Je, ni lini Serikali itajenga kwa kiwango cha lami barabara ya *KIA* - Sanya Juu ambayo ilikuwa ni ahadi ya Hayati Mheshimiwa Rais Magufuli?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mbunge, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, naomba Mheshimiwa Mbunge avute subira tuweze kusoma bajeti yetu. Naamini tutakuwa tumefanya mapendekezo ya nini kifanyike kwenye hii barabara ya *KIA* - Sanya Juu, ahsante**.**

**SPIKA:** Mheshimiwa Ally Kassinge, swali la nyongeza.

**MHE. ALLY M. KASSINGE:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa nafasi. Narabara ya kutoka Nagurukuru, Njenje mpaka Liwale ipo katika Ilani ya Chama Cha Mapinduzi. Je ni lini Serikali itajenga barabara hii kwa kiwango cha lami ambayo inaunganisha Jimbo la Kilwa Kusini, Kilwa Kaskazini pamoja na Liwale?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Ally Kassinge, Mbunge wa Kilwa Kusini, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, barabra hii Mheshimiwa Waziri alishaahidi. Aliahidi kwenye kamati lakini pia alimuahidi Mbunge, si tu Ally Kassinge lakini hata Mheshimiwa Kuchauka najua anahitaji sana hii barabara; na jana nimekusikia pia ukiichangia hiyo barabara. Naomba tusubiri bajeti tunayokwenda kuijadili sasa hivi, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Josephine Genzabuke, swali la nyongeza.

**MHE. JOSEPHINE J. GENZABUKE:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Je, ni lini Serikali itajenga barabra ya kutoka Simbo kwenda Kalia?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mhehsimiwa Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Josephine Genzabuke, Mbunge Viti Maalum Mkoa wa Kigoma, kama ifuatavyo: -

Mhehsimiwa Spika, Barabara ya Simbo – Ilagala - Kalia, ipo kwenye mpango wa kujenga kwa kiwango cha lami. Sasa hivi kitakachofanyika ni kwanza kupitia usanifu uliofanyika. Kitu tunachokifanya sasa hivi ni kwanza kulijenga daraja la Malagarasi ili liweze kupitika badala ya kutumia vivuko, na baada ya hapo sasa tunafuta kuijenga hiyo barabra yote kwa kiwango cha lami, ahsante.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, nadhani tukubaliane Mhehsimiwa Naibu Waziri amekwisha jibu maswali mengi sana kwa siku ya leo. Mheshimiwa Naibu Waziri ahsante sana kwa majibu yako mengi kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge. Waheshimiwa Wabunge tumefika mwisho wa kipindi chetu cha maswali kutoka kwenu na majibu upande wa Serikali. Kama mjuavyo, kipindi hiki cha Bunge la Bajeti maswali na majibu huwa ni saa moja tu, kwa hiyo niwaombe sana mjitahidi kupeleka maswali ya msingi ili hata ukikosa kwenye nyongeza ya kwako ya msingi yaweko huko mengi na yatakuja mengi tu Bunge hili.

Nitaanza, ninayo matangazo mawili hapa; la kwanza ni tangazo la wageni, kwa hiyo tutaanza na hilo la wageni. Wapo wageni ambao wako jukwaa la Spika, na tutanza na

hao. Wa kwanza kabisa, hawa ni wageni wa Bunge kutoka Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ambao ni Ndugu Charles Kichere, ambaye ni Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali. *(Makofi)*

Ndugu Kichere kwa kawaida ya haya makofi inabidi uwe umesimama mpaka yakiisha, sasa ya yenyewe naona ndio yanaishia, ahsante sana, ahsanteni sana. *(Makofi)*

Ameongozana na watumishi wenzake, yupo Ndugu Benjamin Mashauri ambaye ni Naibu Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (Serikali za Mitaa) karibu sana. *(Makofi)*

Yupo pia Ndugu Benja Majura ambaye ni Naibu Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (Serikali Kuu), karibu sana. *(Makofi)*

Yupo pia Ndugu Salhina Mkumba ambaye ni Naibu Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (Mashirka ya Umma), karibu sana. *(Makofi)*

Yupo pia Ndugu Wendy Massoy ambaye ni Naibu Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (Hazina), karibu sana. *(Makofi)*

Yupo pia Ndugu George Haule ambaye ni Naibu Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (Ukaguzi wa Ufanisi), karibu sana. *(Makofi)*

Yupo pia Ndugu Patrick Bwelindo ambaye ni Mkaguzi Mkuu Bunge, karibu sana. *(Makofi)*

Yupo pia Ndugu Gabriel Ntengo ambaye ni Msaidizi wa Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, karibu sana. *(Makofi)*

Yupo pia Ndugu Focus Mauki ambaye ni Mkuu wa Kitengo cha Habari, karibu sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge wapo pia wageni wawili wa Mheshimiwa Toufiq Salim Turky ambao ni familia yake kutoka Zanzibar; yupo Ndugu Banu Turky ambaye ni mke wake na Ndugu Tamima Turky ambaye ni mama yake. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, Ndugu Tamima Turky ambaye ni mama yake Mheshimiwa Toufiq Salim Turky huyu ni mke wa aliyekuwa Mbunge mwenzetu humu, Mheshimiwa Turky *Mr. White,* karibu sana mama. Lakini pia huyu Ndugu Banu Turky ndiye mke wa Mheshimiwa Turky, hebu asimame tumuone, ahsante sana na karibu sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, wapo baadhi yetu huku walituwakilisha kwenye hiyo harusi, sasa kama mimi na wewe hatukupata mwaliko leo mna nafasi ya kumsalimia shemeji na wifi yenu, naona ameshafika humu ndani. *(Makofi)*

Wako pia wageni wa Waheshimiwa Wabunge, wageni tisa wa Mheshimiwa Godfrey Kasekenya ambaye ni Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi ambao ni familia ya msaidizi wake kutoka Jijini Dodoma, haya karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wageni wanne wa Mheshimiwa Cecilia Paresso ambao ni familia yake kutoka Jijini Dodoma na hawa wameongozana na dada yake ambaye anaitwa Ndugu Celina Paresso, karibuni sana. Lakini pia katika hao wageni, yupo mtoto wake anayeitwa Lisa Steven, karibu sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, wapo wageni watatu wa Mheshimiwa Florent Kyombo ambao ni viongozi kutoka *Kagera Co-Operative Union (KCU)* kutoka Missenyi Mkoa wa Kagera wakiongozwa na Makamu Mwenyekiti Ndugu Respicious John, karibuni sana.

Tunao wageni watano wa Mheshimiwa Fatma Toufiq ambao ni Kamati ya Mashindano ya Pamoja na *Mama Cup*

kutoka Jijini Dar es salaam wakiongozwa na Ndugu Ummy Wencelaus ambaye wengi pengine tunamfahamu kama Dokii, karibuni sana, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao pia wageni kumi na tano wa Mheshimiwa Angelina Malembeka ambao ni kikundi cha Bega kwa Bega na Mama kutoka Mkoa wa Morogoro wakiongozwa na Ndugu Ruth Mateleka, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao pia wageni waliotembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo na hawa ni wageni watano kutoka Wilaya ya Chamwino, Mkoani Dodoma ambao ni viongozi wa *Mlambala Events Organization*, karibuni sana wageni wetu. *(Makofi)*

Wahehimiwa Wabunge, tangazo kutoka kwa Katibu wa Bunge; mnakumbushwa Waheshimiwa Wabunge na watumishi wote kwamba leo Alhamis tarehe 6 Aprili, 2023 kutakuwa na *Iftar* iliyoandaliwa na Mheshimiwa Toufiq Salim Turky, Mbunge wa Mpendae Zanzibar; na Katibu wa Bunge anawakumbusha Wabunge wote na watumishi wote tumealikwa kwenye *Iftar* hii na itaanza saa 12.30 jioni leo. Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge na watumishi wote mnaombwa kuhudhuria.

Waheshimiwa Wabunge, hayo ndiyo matangazo niliyokuwa nayo, tutaendelea na ratiba yetu. Katibu.

**NDG. EMMANUEL MPANDA – KATIBU MEZANI:**

## HOJA ZA SERIKALI

### Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Waziri Mkuu kwa mwaka wa Fedha 2023/2014

*(Majadiliano Yanaendelea)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge tunaendelea na majadiliano ya hoja iliyo mbele yetu, hoja ya Mheshimiwa Waziri Mkuu na ninayo orodha hapa ya Wabunge ambao wameomba kuchangia.

Tutaanza na Mheshimiwa Toufiq Salim Turky, atafuatiwa na Mheshimiwa Jesca Jonathani Msambatavangu, Mhehsimiwa Yahya Ally Yahya Mhata ajiandae.

**MHE. TOUFIQ SALIM TURKY:** Mhehsimiwa Spika, ahsante. Awali ya yote naomba tumshukuru Mwenyezi Mungu *subhanahu wa ta'ala* kwa kutujalia kufika siku ya leo nikiambatana na familia kwa mara ya kwanza pia nikiwa na mke. Wengi wanasema ametoka Uhindini lakini ni Mturuki, kwa hiyo nimetafuta asili kidogo. Pia naomba tumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia mfungo huu wa Ramadhan umefika kwa salama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nataka nichukue fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Rais wetu, Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa kweli katuheshimisha sana ndani ya Tanzania yetu na nje ya Tanzania yetu. Kwa kipindi kifupi mno, na hususan wengi tukiamini akina mama *speed* zao zinakuwa ndogo, lakini kusema kweli wengi wetu katufunulia macho yetu na kudhihirisha kuwa mama anafanya kazi kubwa mno, katika nyanja zote. Kama tukiongelea kilimo basi kulikuwa kuna mapinduzi ya kilimo nafikiri sote mashahidi; tukijaa katika suala la zahanati, sasa hivi kila Wilaya sasa hivi inaongelea masuala ya zahanati, shule, maji, umeme.

Mhehsimiwa Spika, nilikuwa katika Bunge la Afrika ya kule *South Africa,* wenzetu wana mgao wa umeme wa masaa sita, hakuna umeme ni bara linasemekana kuwa la kwanza ndani ya Afrika na wapo katika G-20 hawana umeme, *South Africa,* lakini Tanzania tuna umeme. Sasa ni muhimu sana tukawa watu tunaongelea mengi tu. Najua bado hatujafikia kiwango kikubwa tunachokitaka lakini kazi

tunafanya. Kwa hivyo ni muhimu sana linapokuja wakati wa kupongezana ni muhimu kutoa hiyo taarifa. Si umeme tu; lakini nitashangazwa; tulikuwa katika *mall* fulani kule *Johannesburg* katika mji mkuu kabisa basi ndani ya lile *mall* kulikosekana maji. Sidhani kama tumeenda sisi sehemu hapa zetu kuu tukakosa maji, nafikiri tunapaswa pakubwa sana kumpongeza Mama yetu kwa namna kazi namna anavyochapa kazi.

Mheshimiwa Spika, hali kadhalika tumeona katika Bahari, hususan katika maziwa tuna *MV* Mwanza sahivi, ni meli ya namna yake ambayo imejengwa kwa kuhakikisha katika maziwa yetu masuala ya safari, mizigo yanaenda salama na uchumi unaweza kuimarika. Lakini pia mwenzangu hapa alikuwepo Bw. Tabasamu akaniambia daraja lake la Kigongo limeshakamilika, limebakia nguzo tatu tu na mkandarasi ashalipwa kila kila kitu. Kwa hivyo hapo tunatakiwa tumpongeze mno.

Mheshimiwa Spika, na mimi katika hoja hii ya kumchangia Mheshimiwa Waziri Mkuu naomba nimpongeze sana kwa hotuba yake ya jana. Amegusa sehemu zote, nafikiri Watanzania tuliosikiliza imeigusa kila mwana Tanzania; na tumeona namna gani Serikali ya Mama na hususan kupitia Mhehsimiwa Waziri Mkuu, namna walivyojipanga kuhakikisha umasikini unazidi kupungua na watu wanapata faraja ndani ya Tanzania yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, leo hii nilitaka kuchangia hoja moja tu, na mara nyingi napenda kuichangia hiyo kwa sababu watu wameona kama ipo mbali sana lakini hili suala haliko mbali bali lishafika.

Mheshimiwa Spika, wakati wa zamani uchumi ulivyoanza wakulima walikuwa wanatumia mikono. Zilipokuja mashine wengi wao wakaona kazi inaanza kupungua zinaenda kwenye mashime sasa sisi hatutafanya kazi, ajira. Ikaja wakati

sasa wakaona kumbe sio kwamba tutapungukiwa lakini ile *work force* ikahama ikaenda katika *industrialization;* kwenye viwanda, kwa kuwasaidia karakana zile mashime ziweze kujengwa. Ikaja wakati wa 80 dunia ikapatwa na janga kubwa, ajira zikashuka kwa sababu yaliingia masuala ya kompyuta na watu wengi sana wakakosa zile ajira kwa sababu watu walikuwa wameshazoea ma-*typewriter* kuandika barua na nini yote yakachukuliwa katika *work force* ikaenda katika kompyuta, watu wakaona kazi zitakosekana. Ni kweli zilikosekana zikachukua muda, lakini baada ya hapo watu wakapata kazi na dunia ikaendelea.

Mheshimiwa Spika, nimesoma majarida mbalimbali na imefanyiwa tathmini; kwamba, miaka mitano mpaka kumi ijayo takriban robo ya *Europe* na Marekani, robo ya *work force* itakuja kuondoka, inaondoka wapi? Kuna kitu kinaitwa *Artificial Intelligence;* ambapo kuna wahariri, waandishi wa habari humo ma-*journalist* waliozoea kuandika vitabu majalada, matoleo mabalimbali na *newspaper;* hata watu wetu wa *hansard* hizo kazi zitaenda kwenye *a high;* ni mfumo, zinaenda kwenye mfumo watu hawahitajiki tena.

Mheshimiwa Spika, kuna kazi za utawala za kupeleka barua sijui za *administrative work;* zote zile zitapungua. Kazi za sheria, kuandika sijui mabarua ya kupeleka kisheria, kuandika zile *code* kila kitu nyingi zitapungua; hali kadhalika katika masuala ya ujenzi, mawasiliano na maitnaince. Hili sio kama litakuja tayari limeanza.

Mheshimiwa Spika, jana, kwa bahati, kuna *App* niliisoma; na naombeni Waheshimiwa Wabunge na nyie mkipata nafasi mnaweza mkai-*download* inaitwa *Chat-GPT*. Hii *Chat-GPT* umei-*download* unamwambia nataka nimuandikie barua Waziri Mkuu nimuelezee nina changamoto *a b c* basi, inaandika barua, tena unamwambia niandikie kwa namna ya *shakespeare* inakuandikia kila kitu na tena kwa namna ya *literature* unayoitaka wewe. Maana yake nini kama mtu

ulikuwa hujui kuandika, hujasoma sijui hujafanya nini, yote inafanya yenyewe. Sasa tujiulize wale watu waliokuwa wanafanya watapata wapi kazi hizo? Hata hivyo, sasa tunatakiwa na sisi tuwe na *think tank* yetu ambayo sasa humu ndani na naomba tuishauri Serikali kuwa na *think tank* ambayo itaweza kutathmini na sisi tutaathirika vipi katika hili wimbi jipya lililokuja duniani la *artificial intelligence. (Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mfano mdogo ni suala zima la madereva, kama tunavyokumbuka zamani madereva walikuwa unaenda zako sehemu mbalimbali wanakusimamisha njia, lakini sasa hivi una *bolt, bolt* ile imesababisha mtu yeyote anaweza kujiajiri, lakini wale madereva wa zamani sasa hivi wamepungukiwa na kazi kwa sababu, sasa hivi hutaki kujua akili yako. Kwa hivyo, naishauri Serikali kuwa na kamati, la kwanza kuwa na semina ya Wabunge humu ndani tufahamu nini *artificial intelligence,* ili tuweze kuwasaidia wenzetu wengi …

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Kengele ya pili imeshagonga Mheshimiwa. Kengele ya pili imeshagonga.

**MHE. TOUFIQ SALIM TURKY:** Mheshimiwa Spika, nashukuru na naunga mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Jesca Jonathan Msambatavangu, atafuatiwa na Mheshimiwa Ally Yahya Mhata na Mheshimiwa Kirumbe Shabani Ng’enda ajiandae.

**MHE. JESCA J. MSAMBATAVANGU:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi na nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa fursa hii leo tena.

Mheshimiwa Spika, kwanza nishukuru kwa hotuba nzuri ambayo Waziri Mkuu ameisoma jana ambayo imesheheni matumaini makubwa, lakini hoja yangu leo itakuwa ni umuhimu wa binadamu kutoa fursa kwa binadamu mwingine kuishi.

Mheshimiwa Spika, upo ukatili unaendelea juu ya binadamu na sisi tusipokuwa makini *specie* yetu kama viumbe hai kama binadamu tunakwenda kupotea.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri Mkuu amesema jana namna ambavyo Serikali imetekeleza mambo yake kwa mwaka ulioisha na fedha nyingi tulizowekeza huko, zaidi ya trilioni nane kwa ajili ya kutengeneza miundombinu mbalimbali ya kuhakikisha kwamba, ustawi wa binadamu katika nchi yetu unaendelea kuwepo. Naamini kabisa fedha nyingi tunazowekeza kwenye miradi ya kimkakati nia na madhumuni yake sio kutusaidia sisi tunaoishi leo peke yetu, tuna nia ya kuwasaidia watoto wetu, tuna nia ya kuwasaidia wajukuu zetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tumewekeza zaidi ya bilioni 762 kwenye reli ambayo tunategemea itaishi zaidi ya miaka 100 ijayo na yamkini sisi katika miaka 100 ijayo sisi hatutakuwepo. Tumewekeza katika bwawa la umeme zaidi ya bilioni 800, Bwawa la Mwalimu Nyerere, hatutakuwepo. Tunawekeza katika miundombinu ya viwanja vya ndege zaidi ya bilioni 77 na Iringa tumepata bilioni 41 kwa ajili ya kujenga Kiwanja cha Nduli, kimefika asilimia 42 lakini tunajua tuliambiwa mpaka Septemba kitakuwa kimekamilika, tunajua zitaletwa fedha, lakini nia na madhumuni ni kwamba, tusaidie watoto wetu na wajukuu zetu na vizazi vijavyo, kama Watanzania na Waafrika.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri Mkuu ameeleza mipango ya maliasili za Taifa letu, jinsi tunavyotaka kuendelea kulinda maliasili zetu sio kwa ajili yetu sisi tu, kwa

ajili ya watoto wetu na uzao ujao. Mama alivyojitolea kwa ajili ya kufanya ile *movie* ya *Royal Tour,* nia na madhumuni sio ataiona yeye peke yake na Awamu yake ya Sita, nia na madhumuni wajukuu wetu pia waje waione.

Mheshimiwa Spika, yapo mambo yanayoendelea katika jamii yetu. Tusipokuwa makini na tukienda kwa ku-*copy* na ku-*paste* kwa sababu, watu fulani wamesema au mataifa fulani yamesema, sisi tusipoamua kutumia akili zetu na kwamba, tumepewa fursa na Mungu na sisi kama Watanzania kuamua mambo yetu, upo wakati na sisi kama Watanzania tutoe fursa mataifa mengine yaje yajifunze kutoka kwetu namna ambavyo tunalea watoto wetu, namna ambavyo tunakuza watoto wetu.

Mheshimiwa Spika, sisi kama Waafrika hatukufundishwa kujifunza tu kwa watu wengine. *Afterall* Mungu aliumba mtu mke na mume hakuangalia *color* ilikuwa ni *color* gani, kwa hiyo, na sisi watu wengine, mataifa mengine wanatakiwa waje wajifunze namna ambavyo Afrika inatunza watoto wake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hapa katikati ukatili kwa watoto wetu umezidi mno. Tunashangaa, hatuelewi imetokea wapi? Imekuwaje? Waziri Mkuu ameeleza hali ya usalama wa nchi yetu na utulivu iko vizuri, mipaka yetu iko vizuri na ni kweli, wote tunashuhudia tuko vizuri, lakini kumbe ndani ya nchi kwenye uzao wetu tayari hatuko salama. Watoto wetu wamefanyiwa vitu vya hovyo mno. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, leo kumbe humu ndani tuna taasisi, tena Mheshimiwa Waziri Mkuu katika ku-*wind up* hotuba yake ameeleza mambo muhimu ambayo anataka yafuatwe. Moja katika yale sita, ameeleza jambo la tatu anasema, viongozi wetu wa Serikali, dini, mil ana vyama vya siasa wakemee kwa nguvu zote ushiriki wa sehemu yoyote ya jamii katika matendo yasiyoendana na mila, tamaduni na desturi za

Watanzania. Hii ni pamoja na wazazi na walezi wote kushiriki kikamilifu katika makuzi na malezi bora ya watoto yatakayosaidia kuwaepusha na vitendo viovu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, *it is a high time* suala hili linalohusiana na ukatili kwa watoto wetu, ulawiti kwa watoto wetu, ubakaji kwa watoto wetu, masuala ya ndoa za jinsia moja yasifumbiwe macho. Tuyaongelee Makanisani, tuyaongelee Misikitini, tunaanza hapa Bungeni, tuyaongelee Serikalini, tuyaongelee kwenye familia zetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tutapotea. Hizi reli zitakuja kupandwa na popo kama ilivyokuwa Sodoma na Gomora. Huu umeme hautakuwa na maana. Haya majengo makubwa tunayojenga hayatakuwa na maana. Barabara ile wanayotujengea Iringa kwenda *Ruaha National Park* nani atapanda nani ataangalia wale tembo? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimesema lazima binadamu mmoja atoe fursa kwa binadamu mwingine. Kama babu yangu mimi asingetoa fursa kwa baba yangu mimi leo ningekuwa wapi? Angemua babu yangu mimi aolewe na babu mwingine wa Kijiji kile ingekuwaje? Mimi leo ningekuwa wapi? Kama mama yangu angeona ndoa zina shida akaamua kuolewa na mwanamke mwingine, mimi leo ningekuwa wapi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lazima vijana wetu waambiwe ukweli. Sisi tunawapenda, tunawaheshimu ndio maana tunawekeza, ndio maana mama hakawii anazunguka huko na huko kwa sababu ya kuhakikisha kwamba, tunalinda Watanzania na uzao wao. Sasa leo tukikaa kimya kwa sababu, ni *human right,* ni *human right* ipi wakati sisi hatutoi fursa? Sisi tulipewa *right* ya kuishi na moja *among the human rights* ni haki ya mtu kuishi na wewe unatakiwa kutoa fursa kwa mtu mwingine aishi, *you don't give the right* halafu unataka upewe *right,* haiwezekani! *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, twende kwenye shule zetu na si suala tu la Serikali kusema kwamba, sasa Serikali ije hapa maendeleo ya jamii watwambie hiyo jamii wanayoitunza ni ipi? Hii mipango tunayoitenga ya nini? Haya mabilioni ya fedha tunayaweka ya nini kama hayataangalia uzao wa tumbo letu? Kama hatutaangalia watoto wetu wanaishi vipi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, leo watoto wako kwenye *vulgar environment,* hawaelewi waende wapi. Wakija majumbani tafiti za *UN* zinaonesha kwamba, *66%* ya watoto wanafanyiwa ukatili majumbani kwa wazazi wao, *44%* inayobaki ni shuleni na sehemu nyingine. Wanakwenda shuleni tena wale *guardians* ambao tumewakabidhi watoto nao tena wanawalawiti watoto, wanawafanyia ubakaji watoto. Tanzania *where is this country heading to? (Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sisi *we need to be a role modal in this world. Other people should come also and learn from Tanzania* kwamba na sisi tumeweza kuwa-*groom* watoto wetu, sio lazima tuige kila kitu *from them.* Hata wao wenyewe wame-*confuse.* Nimemsikia Biden mwenyewe anasema, anashangaa anasema *my mum* alisema tu *it is sinful,* halafu akasema *it is cruelty* kwa binadamu, ni ukatili kwa binadamu. Wenyewe hawaelewi, yaani *they don't know what to say. They find somewhere to read,* wanataka mahali wakajifunze. Tanzania *we are ready,* tulikuwa tuna-*raise* vipi watoto wetu? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, leo Japani wanahangaika kwamba, uzao wao unakwisha kwa sababu, mwanamke ana uwezo wa kuzaa mtoto 1.3 kwa sisi tuliosoma hesabu maana yake kati ya wanawake wanne anayezaa watoto wawili ni mmoja tu. Wengine wanazaa mmoja wengine labda hawazai. Watu wanaona *population* yao inashuka, *they are fighting,* Waziri Mkuu yule ana-*fight* namna gani ainue *population* yake. Sasa kama *it is a human right* wao kuoana wanawake kwa

wanawake na wanaume kwa wanaume kwa nini wanawa-*force* watoto wetu waingie kwenye hizo kwa kuwalazimisha kufanya vitu? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wao nao wa-*grow* wafike waamue wenyewe. Nashindwa kuelewa *NGO* ndani ya nchi hii. Nimerudi Iringa nimekutana na hiyo, vijana wananiambia kuna mahali mmetupeleka tukafundishwe tukopeshwe, lakini *madam* mbona kama vile wanatufundisha mambo fulani? *In this country! (Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tumewaruhusu, halafu hiyohiyo Wizara ya Maendeleo ya jamii, hiyo hiyo ndio inasajili *NGO,* hiyo hiyo ndio inatakiwa kulinda jamii, hiyo hiyo ndio inatuletea watu wanagawa vilainishi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, *look here, we are privileged to be leaders in this country.* Ni neema, *it is a grace*. Tusije tukajiona kwamba, sisi ni wa maana sana kuliko watu wengine, *we are graced* na tusipotumia neema hii vizuri, leo tukikaa kimya Mungu atainua mawe yatasema, ila sisi na uzao wetu utapotea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, narudia tena, binadamu atoe fursa ya binadamu mwingine kuishi. *We love them, they are our kids.* Ni watoto wetu, tunawapenda, hata hawa walioingia kwenye mifumo hiyo ya ndoa za jinsia moja au ushoga hatuwachukii ni watoto wetu, mtoto wako hata akiwa kibaka utamkataa?

Mheshimiwa Spika, tutafute mbinu za kuwasaidia wale watoto wetu. Tuone namna gani tutakaa, kama *we think* kwamba, dunia ime-*advance scientifically let that science prove* kwamba, inaweza ku-*solve problems* kama hizi. *Science* ituhakikishie kama inaweza kumsaidia kijana wetu wa kiume aliye-*engage* huko, amepoteza kabisa viungo vyake, nguvu zake hazi-*function,* itusaidie. Hatujamaliza bado

kupambana na matatizo ya uzazi wa wanawake, leo tuanze kupambana na kubadilisha matumbo ya wanaume yawe ya akinamama, inawezekanaje? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, haya tu ambayo ni *original* tumepewa bure tumeshindwa kuyashughulikia…

**SPIKA:** Mheshimiwa Jesca Msambatavangu muda wako umeisha. Dakika moja, malizia.

**MHE. JESCA J. MSAMBATAVANGU:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. Naomba Waheshimiwa Wabunge tusimame kwa pamoja. Kwa agizo hili twende kwa pamoja, ukisimama hapa wekaweka kidogo mbwembwe, haiwezekani, Ubunge wetu hauna maana kama watoto wetu hawatakuwepo baada ya miaka 10. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hatuko tayari kuacha Tanzania iwe ni nchi kama ilivyo Sodoma na Gomora wanazaliana popo. *We are not ready, we are here* ku-*make sure* Watanzania wanaendelea kuwepo katika ulimwengu huu mpaka ukamilifu wa dahari, ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Haya ahsanteni sana.

Mheshimiwa Ally Yahya Mhata, atafuatiwa na Mheshimiwa Kirumbe Shabani Ng'enda na Mheshimiwa Muharam Mkenge ajiandae.

**MHE. YAHYA A. MHATA:** Mheshimiwa Spika, nami naomba kuchukua nafasi hii kwanza kumshukuru sana Mwenyezi Mungu, mwingi wa rehema ambaye ameniwezesha siku ya leo kusimama mbele ya Bunge lako hili Tukufu. Pili, naomba nimshukuru sana Rais wetu wa Jamhuri ya muungano wa Tanzania kwa kazi kubwa anayoifanya ya kuhakikisha kwamba, Taifa letu linakwenda mbele. Tatu, naomba nimshukuru sana Waziri Mkuu kwa hotuba yake nzuri

sana ambayo jana amelielezea Taifa letu, hotuba ambayo ime-*cover* mambo mengi.

Mheshimiwa Spika, sasa kwa ufupi, naomba nizungumzie mambo mawili makuu ambayo Mheshimiwa Waziri Mkuu ameyazungumza katika hotuba yake. Mheshimiwa Waziri Mkuu amezungumzia suala la maji. Sisi sote tunajua changamoto zilizopo sasa hivi juu ya mabadiliko ya hali ya hewa, lakini namshukuru sana Waziri Mkuu, naishukuru sana Serikali yetu ya Chama cha Mapinduzi kwa jitihada ilizofanya kukabiliana na tatizo hili la maji, hasa katika Jimbo langu la Nanyumbu. Ndani ya Jimbo langu la Nanyumbu wakati mama yetu Samia Suluhu Hassan anachukua nchi tulikuwa na changamoto kubwa sana ya maji. Ndoo ya maji ilifikia shilingi 2,500 ndani ya miaka hii miwili amefanya mapinduzi makubwa na sichelewi kuyaeleza ndani ya Bunge lako nini kimefanyika ndani ya jimbo langu.

Mheshimiwa Spika, wakati mama anaingia madarakani kata zifuatazo zilikuwa hazina maji kabisa na wala walikuwa hawajui nini maana ya maji ya bomba, lakini leo ninavyozungumza tuna maji ya bomba na wananchi wananufaika na huduma hiyo.  Kata ya Nandete walikuwa hawajui kabisa huduma ya maji, Kata ya Mikangaula walikuwa hawajuikabisa huduma ya maji, Kata ya Nangomba, Kata ya Mikangaula Nangomba walikuwa hawajui kabisa, Kata ya Kamundi walikuwa hawajui kabisa, lakini ndani ya miaka miwili yamefanyika mapinduzi makubwa, leo wananchi wanajua nini maana ya mabomba na nini maana ya maji safi na salama. Jambo hili namshukuru sana Waziri Mkuu kwa kuisimamia Serikali vizuri na hatimaye wananchi wananufaika na huduma hizi.

Mheshimiwa Spika, ndani ya hotuba yake Waziri Mkuu amezungumzia upatikanaji wa maji katika ile miji 28. Wilaya yangu ya Nanyumbu ni moja ya wanufaika wakuu wa ile miji 28.

Mheshimiwa Spika, utakumbuka kwamba, mwaka jana tulitia saini ule mkataba. Ule mkataba tulitia saini pale Ikulu kwamba, wakandarasi wale waje katika majimbo yetu na watekeleze mradi huu, lakini mradi huu umechelewa sana, ndani ya mwaka mmoja mradi haujaanza.

Mheshimiwa Spika, nimefurahi, jana mara baada ya Waziri Mkuu kuzungumza nikakutana na Waziri wa Maji na amenihakikishia kwamba, sasa kila kitu kimekamilika na huu mradi unakwenda kuanza. Naomba niwahakikishie wananchi wangu wa Jimbo la Nanyumbu, mradi huu unakuja kuanza na vijiji takribani 20 vitanufaika na mradi huu, hili ni jambo la kupongeza sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mradi huu wa maji pamoja na kwamba, unapita katika vijiji mbalimbali hadi kufika katika Mji wa Mangaka hapa ndipo kwenye walengwa wakubwa katika mji huu. Wananchi wa Mangaka wanashindwa kuwekeza katika miradi mbalimbali ya kiuchumi kwa sababu ya ukosefu wa maji. Leo utashangaa *guest house* zetu zote za Mangaka tunachukua maji ya kopo, hatuna maji ya bomba. Kwa hiyo, tuna imani kabisa kwamba, mradi huu utawezesha wananchi ambao wanaenda kuwekeza mbali na Wilaya yetu watarudi na kujenga nyumba nzuri, hoteli na hatimaye wale watu watalii wanaotoka Msumbiji kuja katika Mkoa wetu wa Mtwara watakuwa na mahali pazuri pa kufanya shughuli zao za starehe.

Mheshimiwa Spika, naomba pia niipongeze Serikali katika miradi, kuna miradi mikubwa ya mabwawa ndani ya jimbo langu. Kuna ukarabati mkubwa wa bwawa ndani ya Kata ya Sengenya ambao Serikali imetoa bilioni tatu na milioni mia nne, mradi huu unaanza hivi karibuni na takribani vijiji 10 vitanufaika na mradi huu; Mradi wa Upanuzi wa Bwawa la Sengenya.

Mheshimiwa Spika, katika Kata ya Maratani Serikali imejenga bwawa kubwa lenye thamani ya shilingi bilioni moja na milioni mia tano, lakini imeleta bilioni tatu na milioni mia sita kwa ajili ya kuweka mtandao wa mabomba, vijiji vinne vitanufaika na mradi huu, Kijiji cha Lipupu, Maratani, Mchanganee na Malema. Mambo yote haya ya maendeleo yamefanywa ndani ya kipindi kifupi chini ya utawala wa mama yetu Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kweli, nampongeza sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kama hiyo haitoshi, mradi wa uchimbaji wa visima. Ndani ya miaka miwili visima visivyopungua 25 vimechimbwa ndani ya jimbo langu na mikakati inaendelea katika kuhakikisha kwamba, sasa visima hivi vinawekwa mitandao ya maji, ili wananchi wanufaike.

Mheshimiwa Spika, baada ya kutoka hapo naomba niende kwenye mtandao wa barabara. Naipongeza sana Serikali, wakati mama yetu anaingia madarakani Jimbo langu la Nanyumbu lilikuwa linapata shilingi milioni 550 kwenye *TARURA,* leo ninavyozungumza tunapata bilioni mbili na milioni mia nne, ni jambo la kupongeza sana, lakini sio kupata fedha tu, fedha zile tunazisimamia. Mimi kama Mbunge wa Jimbo lile nahakikisha matumizi sahihi ya fedha, *value for money,* ionekane. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ndani ya miaka miwili tumeweza kujenga barabara kilometa 4.5 za lami, jambo ambalo ndani ya Wilaya ya Nanyumbu kitu lami kilikuwa hakipo ndani ya mji wetu. Leo ndani ya jimbo langu tumeweza kuweka taa za barabarani, jambo ambalo wananchi walikuwa hawajui kama kuna taa za barabarani. Hii yote imefanyika chini ya miaka miwili ya Dkt. Samia Suluhu Hassan, ni jambo la kupongeza sana sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kama haitoshi, tumeweza kujenga madaraja yasiyopungua 15, makalavati na vivuko mbalimbali, hii yote ni kwa sababu fedha zimekuja lakini tunazisimamia. Nami naomba niwape rai ndugu zangu Wabunge, fedha hizi zinapokuja tuwe wasimamizi wakuu wa hizi fedha. Tunatambua kwamba kuna *TARURA,* kuna *Engineer TARURA* lakini bado Mbunge una sababu ya kusimamia matumizi sahihi ya fedha hizi.

Mheshimiwa Spika, jambo la Tatu naomba niipongeze tena Serikali kwenye kilimo. Wilaya yangu ilikumbwa sana na baa la njaa. Serikali yetu ya Chama cha Mapinduzi chini ya Mama yetu Dkt. Samia Suluhu Hassan tuliomba msaada wa chakula cha bei nafuu na Serikali imetupatia takribani tani 1000. Wananchi wamepata mahindi ambayo yameuzwa kwa bei nafuu. Kuna baadhi ya watendaji ambao hawakuwa waaminifu walitumia fursa hii kujinufaisha.

Mheshimiwa Spika, ninampongeza sana Mkuu wetu wa Wilaya Mama Chaurembo na Kamati yake yote ya Ulinzi na Usalama kwa kazi kubwa waliyoifanya ya kupambana na hawa watumishi ambao siyo waaminifu na hivi ninapozungumza wengi wamepelekwa Mahakamani ili sheria ichukue mkondo wake. Kwa hiyo, mimi naipongeza sana Serikali ila rai yangu kwa Serikali, tunatambua tuna njaa, tunahitaji wananchi wawezeshwe pembejeo kwa wakati, mbolea kwa wakati ili waweze kuepukana na baa hili la njaa.

Mheshimiwa Spika, sasa hivi kinachofanyika, mbolea iko mbali na wananchi, haiwezekani Wilaya ya Nanyumbu mtu afuate mbolea kilometa 54 toka alipo, hili jambo litakwamisha sana maendeleo ya wakulima wetu. Kwa hiyo, naomba sana Serikali iliangalie hili chini ya Wizara ya Kilimo.

Mheshimiwa Spika, mwisho naomba tena kuchukua nafasi hii kuishukuru sana Serikali kwa yale yote ambayo

inaendelea kuyafanya ya kuhakikisha kwamba wananchi wa nchi hii wanaishi katika maisha bora na salama.

Mheshimiwa Spika,nashukuru sana kupata nafasi hii. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Kilumbe Shabani Ng'enda atafuatiwa na Mheshimiwa Muharami Shabani Mkenge, Mheshimiwa Dkt. Christine Gabriel Ishengoma ajiandae.

**MHE. KILUMBE S. NG'ENDA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii. Nami nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa Rehema kwa kuendelea kutupa uhai na afya, nitumie nafasi hii kwa kweli kuwatakia Wakristo ambao wako katika mfungo wa kwaresma na Waislamu ambao wako katika mfungo wa Ramadhani, heri ya funga na funga hii itusaidie katika kuleta baraka katika nchi yetu.*(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kumshukuru Mwenyezi Mungu nitumie nafasi hii kumpongeza na kumshukuru sana Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mama yetu, kipenzi chetu na mfano wa kuigwa wa wanawake wa Kiafrika katika uongozi bora na wote wanaomsaidia akiwemo Makamu wa Rais, Rais wa Zanzibar, Waziri Mkuu na wengine wote katika Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wakati mwingine hata tunapofika mahala tukasimama na kushauri na kukosoa baadhi ya mambo hatumaanishi kwamba kazi haifanyiki, kazi iliyofanyika ni kubwa sana, tunamshukuru sana Rais wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niweke salaam za pekee za shukrani kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa hotuba yake nzuri na zaidi

ya yote kwa mahusiano mazuri na uchapakazi mzuri, mahusiano mazuri na sisi Waheshimiwa Wabunge pamoja na Watumishi wengine wote wa Umma. Mheshimiwa Waziri Mkuu wewe ni mtu wa mfano wa kuigwa katika tabia njema na mahusiano mema, tunakushukuru sana.

Mheshimiwa Spika, pongezi hizo ziende sambamba na kupongeza hatua inayochukuliwa na ofisi ya Waziri Mkuu katika kusaidia tatizo la ajira kwa vijana nchini kwa kutoa mafunzo kwa vijana kwa *program* maalum ambayo inatolewa *VETA* inayoitwa Programu ya Waziri Mkuu. Nimetembelea Chuo cha *VETA* - Kigoma, nimewaona vijana waliotoka pale awamu ya kwanza, nimewaona wa awamu ya pili na sasa tunasubiri awamu ya tau. Mheshimiwa Waziri Mkuu na Ofisi yako tunawapongeza. *Program* hii endeleeni nayo ni ya manufaa katika kuwapa vijana ujuzi wa kujiajiri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pamoja na hilo ni vizuri ieleweke kwamba kutokana na hali zetu za maisha na hasa familia zingine ambazo ni duni wanazotoka vijana hawa, ni vizuri kuweka utaratibu wa baadhi ya vijana wanapotoka pale kupewa vitendea kazi ili waende wakaanze kujiajiri moja kwa moja. Kumfundisha mtu useremala bila kuwa na vifaa vya useremala ni kweli umempa ujuzi lakini umempa vilevile mzigo katika suala la kujiajiri. Kama inashindikana kufanya hivyo kwa kijana mmoja mmoja tufanye hata kwa vikundi, tutoe fedha za Serikali mbona zipo nyingi zinapotea na nyingine tutaanza kuzijadili hivi karibuni, tupeleke kwa hawa vijana wetu wajiajiri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pale Kigoma nilipotembelea *VETA* nimeona jambo la ajabu sana, kuna kijana mmoja anaitwa Zuberi Abdallah Ismail, huyo kijana ni mwanafunzi pale, kwa ubunifu ameweza kutengeneza redio, anarusha matangazo yeye mwenyewe katika eneo dogo, yule kijana akichukuliwa akaendelezwa anaweza akafanya mambo makubwa sana.

Nilimuuliza wewe ulipataje mawazo haya akasema nime-*search* kwenye redio nikaona *frequency* ambayo ukiweka haipati matangazo yoyote, yaani hakuna *Radio Station* yoyote nikaitumia *frequency* hiyo akatumia 87.5 akaanza kurusha matangazo yake huko Ujiji na yanakwenda umbali wa mita kama 200. Unaona sasa hawa ndiyo vijana wanaweza. *Transmission system* kaitengeneza mwenyewe.

Mheshimiwa Spika, tukifika mahala tukakuza vipaji hivi tunaweza kutengeneza magari, pikipiki, lakini hii imekuwa ni nchi ambayo mpaka *forklift* ya kubebea mizigo bandarini tunaagiza kutoka nje na sisi tunao watu wana akili wamezaliwa na wanawake kama walivyozaliwa hao wengine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo nataka nilizungumzie ni vitambulisho vya Taifa - *NIDA*. Hapa ningeomba Mheshimiwa Waziri Mkuu anisikilize vizuri pamoja na kwamba ninaona Mheshimiwa Waziri Ummy anamsemesha sana, nataka niseme kwamba katika jambo ambalo tunaweza tukadaiwa na Watanzania na tukakosa maelezo ya kutosha ni vitambulisho vya *NIDA*. Ninataka niseme kwamba anayefikiria vitambulisho vya *NIDA* vinatolewa kwa hiari ya Serikali siyo sahihi asome Ilani ya Uchaguzi Ibara ya 105(q) kinasema hivi: ‘‘Kuwezesha Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa, kuendelea kutambua, kusajiri na kutoa vitambulisho vya Taifa kwa Raia wa Tanzania, Wageni Wakazi, kwa kuhakikisha watu wote wenye sifa ya kusajiliwa wanapata utambulisho wa Taifa, wanasajiliwa na kupatiwa vitambulisho na Taasisi zote za Umma na binafsi zinaunganishwa na mfumo wa *NIDA*’’.

Mheshimiwa Spika, hili ni jambo ambalo limeahidiwa na CCM kwenye mikutano ya kampeni, hii ni ahadi kuhakikisha kila mtu. Leo hii Mkoa wa Kigoma kati ya watu waliochakatwa kuomba vitambulisho watu 964,967 ni watu 582,683 sawa na asilimia 60.4 tu ndiyo waliopata vitambulisho,

haiwezekani! Leo tunazungumza suala la vitambulisho vya Taifa leo ni mwaka wa 12 tulianza mwaka 2011 na nataka ieleweke na Serikali hapa ielewe vizuri kwamba inakwamisha maendeleo ya watu mengi sana kwa kuwanyima vitambulisho vya Taifa.

Mheshimiwa Spika, wapo watu ambao wanataka kuingiza umeme majumbani kwao wanaombwa kadi za *NIDA*, wapo watu wanataka kuingiza maji, wapo watu wanataka kuingia katika mfumo wa *TRA*, wapo watu wanataka kuomba *passport* za kusafiria kwenda kwenye masuala mbalimbali ya maisha yao lakini wanakwama kwa sababu ya vitambulisho vya *NIDA*. Na hili ningekuomba sana Mheshimiwa ni kwa sababu nimelisema katika Ofisi ya Waziri Mkuu na Mheshimiwa Waziri Mkuu ndiyo Msimamizi Mkuu wa Serikali na tunakujua Mheshimiwa Waziri Mkuu wewe ni mtu makini na mahiri, tukuombe sana kama hapa katikati labda ulitikisika tikisika na vineno vya wahuni usijaali simama imara fanya kazi, umeaminiwa! Katika Tanzania hii ni historia Waziri Mkuu mmoja kuaminiwa na Marais wawili, chapa kazi hakuna kurudi nyuma simamia Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwisho ninataka kuzungumzia usafiri wa mabasi yaendayo Mikoani. Kuna watu wangu wa Kigoma wanapata adha isiyokuwa na sababu. Sababu kubwa inayozungumzwa ni tatizo la usalama. Watu wanakuja kituo cha basi cha Magufuli wanalala pale ili Saa 12 asubuhi waondoke maana mtu hawezi kutoka Mbagala akaja akawahi basi, analala pale anatoka hapo anakwenda akifika Kaliua Tabora analala, kesho yake ndiyo afike Kigoma. Ninaishauri Serikali, jambo jepesi kabisa kwamba wekeni utaratibu wa kiusalama, lakini kwa sababu eneo lile la Kigoma ambalo lilikuwa na Wakimbizi ndiyo lina tatizo la usalama, mabasi ya Kigoma yaondoke saa Nne usiku Dar es Salaam, yapite maeneo yote haya yafike eneo lile la Kigoma wanapita, siyo watu wanakuja kulala stendi ya Magufuli ,wanakwenda tena kulala stendi ya Kaliua!

Mheshimiwa Spika, kadri tunapofika mahala tukawapotezea watu muda ndiyo tunavyofanya shughuli za uzalishaji kuchelewa. Nchi zilizoendelea watu wanasafiri usiku, asubuhi wanafika mahala wanafanya shughuli zingine za kimaendeleo.ninaiomba sana Serikali…

**MHE. ALOYCE A. KWEZI:** Mheshimiwa Spika, taarifa!

**SPIKA:** Taarifa inatokea wapi, aah! Kwa Mheshimiwa Aloyce Andrew Kwezi.

**MHE. ALOYCE A. KWEZI:** Mheshimiwa Spika, nilitaka nimpatie…

**SPIKA:** Subiri kidogo, subiri kidogo. Mheshimiwa Kirumbe Ng'enda kuna taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Kwezi. Mheshimiwa Kwezi.

**MHE. ALOYCE A. KWEZI:** Mheshimiwa Spika, nilitaka ninampa taarifa Mheshimiwa mzungumzaji ni kwamba yale mabasi kulala Kaliua yanaukuza uchumi wa Wilaya ya Kaliua ni hilo tu,, ahsante. *(Kicheko)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Kilumbe Ng'enda unaipokea taarifa hiyo.

**MHE. KILUMBE S. NG'ENDA:** Mheshimiwa Spika, taarifa naipokea lakini kila mafanikio yana changamoto, kwa hiyo hayo mafanikio anayoyapata yeye ni changamoto kwangu, kwa hiyo tu-*balance*, ameshavuna nyingi sana za watu wa Kigoma, sasa awaache na wenyewe waendelee kuchapa kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo naunga mkono hoja, ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Nadhani hoja ya msingi hapo ni kuruhusu mabasi kutembea usiku hasa maeneo ambayo hayana shida ya usalama.*(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, nilikuwa nimeshamtaja Mheshimiwa Muharami Mkenge kwamba atafuatiwa na Mheshimiwa Dkt. Christine Gabriel Ishengoma, Mheshimiwa Ester Matiko ajiandae.

**MHE. MUHARAMI S. MKENGE:** Mheshimiwa Spika, napenda kushukuru kupata nafasi hii ya kuchangia hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu. Kwanza kabisa napenda nitoe pongezi zangu za dhati kabisa kwa Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mama yetu Samia Suluhu Hassan kwa kazi kubwa ambayo anaifanya katika kuliongoza Taifa hili la Watanzania.

Mheshimiwa Spika, ni ukweli usiofichika, ndani ya kipindi cha miaka miwili ya kiongozi wetu Mama Samia, mambo makubwa sana yamefanyika katika nyanja mbalimbali katika kuendeleza nchi yetu. Mimi binafsi nianzie katika suala la miundombinu.

Mheshimiwa Spika, katika suala la miundombinu Mheshimiwa Rais pamoja na Serikali yake wamejitahidi kwa hatua kubwa sana, nikichukulia kwangu kwa mfano Bagamoyo, ndani ya miaka miwili ya Mama Samia tumepata zaidi ya shilingi bilioni moja katika ujenzi wa barabara zetu, ukiachilia mbali barabara na taa za barabarani sasa hivi zinawaka, kwa hiyo Bagamoyo inawaka na Bagamoyo inang'ara, hizi zote ni juhudi za Mheshimiwa Rais wetu kipenzi Mama Samia Suluhu Hassan.

Mheshimiwa Spika, nizungumzie suala la nishati. Mheshimiwa Waziri Mkuu katika hotuba yake amezungumzia suala la nishati na amezungumza karibuni sasa hivi asilimia 76.7 ya nishati tuko vizuri lakini bado kuna changamoto nyingi

sana katika suala la nishati na hasa katika suala la umeme. Katika suala la umeme bado vijiji vingi pamoja na vitongoji vingi havijapata umeme. Ukienda sehemu mbalimbali bado utakuta nguzo zimewekwa lakini huduma ya umeme bado katika usambazaji wake. Suala la nishati ni muhimu sana katika nchi, wananchi wanapopata umeme ndipo maendeleo yanapopatikana.

Mheshimiwa Spika, pamoja na hayo bado tunanishati ya kupikia, nishati ya kupikia bado Tanzania tuna changamoto kubwa sana. Watanzania wengi sana asilimia kubwa wanatumia mkaa, hii inasababisha misitu yetu pamoja na vyanzo vyetu vya maji kuharibiwa kutokana na watu kukata misitu, hii kwa kweli ni changamoto kubwa sana. Hivyo basi, nilikuwa naishauri Serikali katika hili suala la nishati ya kupikia waweke mipango madhubuti kabisa kama walivyofanya ruzuku katika mafuta, watoe ruzuku katika gesi, watoe ruzuku katika vifaa vinavyoshughulika na majiko ya gesi ili Watanzania wengi waweze kupata gesi.

Mheshimiwa Spika, hakuna ubaya wowote kusema kwamba mwezi huu tunatoa ruzuku ya mafuta, mwezi huu tutatoa ruzuku katika gesi ya kupikia na vifaa vya gesi kama majiko pamoja na vifaa vinginevyo ili Watanzania wengi waweze kupata nafuu ya kupika kwa kutumia nishati hii ya gesi ili kuepuka kukata misitu hovyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, suala lingine ambalo napenda sana niipongeze Serikali ya Mama Samia ni suala zima la bandari. Suala la bandari Mheshimiwa Rais amejitahidi sana. Mheshimiwa Waziri Mkuu jana katika hotuba yake amezungumzia kuna bandari ya nchi kavu ambayo iko maeneo ya Kwala, hii bandari ujenzi wake umefikia asilimia 87 itakapokamilika bandari hii itasaidia sana kukuza uchumi wa nchi. Kuna faida nyingi za bandari ile ikimalizika, hata msongamano wa magari makubwa kutoka Vigwazo kuelekea Dar es Salaam, utapungua kwa kiasi kikubwa sana,

kwa hiyo watu wengi watafanya shughuli zao kwa wepesi zaidi.

Mheshimiwa Spika, tuzungumzie sula la Bandari ya Bagamoyo. Nimefarijika sana jana katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu kuzungumzia bandari ya Bagamoyo. Kwa kweli sasa imefika wakati hii bandari itakapojengwa uchumi wa Taifa utakua.

Mheshimiwa Spika, kuna changamoto ambazo zinaukabili ujenzi wa bandari ya Bagamoyo. Bandari ya Bagamoyo inajengwa katika Kata ya Zinga sambamba na ujenzi wa bandari, iliunganishwa ujenzi wa bandari fidia zile pamoja na kongani za biashara - *EPZA* mpaka sasa mwaka wa 13 wananchi wa Kata ya Zinga hawajui nini wafanye kutokana na fidia ambazo hawajalipwa na hivyo wanasikia kuwa ujenzi wa bandari unakuja na wao bado hawajalipwa fidia zao, kwa hiyo ninaiomba Serikali ihakikishe kwamba inafanya juhudi za maksudi kabisa wananchi wa Zinga waweze kupata fidia zao ili kuwe nafuu zaidi katika suala zima la ujenzi huu wa bandari.

Mheshimiwa Spika, nizungumzie suala la maji, ninaipongeza Serikali ya Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan imefanya kazi kubwa katika miradi ya maji. Mimi kwangu kule Bagamoyo watu wengi karibia asilimia 87 wanapata maji katika Jimbo langu, lakini kuna baadhi ya sehemu zina changamoto kubwa ya maji hasa katika kata mbili, Kata ya Makurunge pamoja na Kata ya Fukayosi, hizi Kata zina changamoto kubwa sana ya maji, inafikia hatua wananchi wanakaa mpaka mwezi mzima maji ya bomba hayatoki, unapowauliza wenzetu wanaoshughulika na masuala ya maji watakwambia kwamba mitambo imekorofisha, umeme mdogo. Kwa hiyo, ninaiomba Serikali ijitahidi kabisa kuhakikisha kwamba suala la upatikanaji wa maji katika hizi Kata na maeneo yote ambayo hayana maji katika nchi hii yanakuwa sawasawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nirudi sasa katika suala la kilimo, ninaipongeza Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inayoongozwa na Mama Samia katika suala zima la kilimo. Ule mpango wa Serikali kuandaa vijana ili waende sasa wakalime ni jambo la msingi sana, lakini naomba kadri siku zinavyokwenda waongeze idadi ya vijana katika suala zima la kilimo. Kwa sababu tumeangalia takwimu ambazo zimechukuliwa mwaka huu, kila Wilaya imepata vijana Wanne. Hivi kweli kila Wilaya ikipata vijana Wanne kutakuwa na maendeleo gani katika suala la kilimo? *At least* tuongeze wigo sasa kuhakikisha kwamba vijana wengi wanachukuliwa kutoka katika Wilaya zetu kwenda kushiriki katika mafunzo waweze kupata tija katika hayo mafunzo ya kilimo.

Mheshimiwa Spika, kwa hayo machache ninashukuru sana, naunga mkono hoja, ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Dkt. Christine Gabriel Ishengoma atafuatiwa na Mheshimiwa Ester Nicholas Matiko, Mheshimiwa Mohammed Lujuo Moni, ajiandae.

**MHE. CHRISTINE G. ISHENGOMA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipatia nafasi ya kuchangia hotuba ya Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa, nampongeza sana Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kazi nzuri sana anayoifanya Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Amefanya mambo mengi. Kila mkoa, kila Mbunge aliyepo humu ndani, kila mwananchi anaona mambo yote aliyoyafanya kwenye mkoa wake, kwenye kata yake kwa maendeleo yetu Watanzania. Kweli tunampongeza sana.

Mheshimiwa Spika, pili, naomba kumpongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa hotuba yako nzuri ambayo umeitoa, ni nzuri sana.

Mheshimiwa Spika, nawe pia nakupongeza kwa jinsi unavyoendesha Bunge letu hili. Hongera sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mkoa wangu wa Morogoro umefaidi mambo mengi sana kwenye maendeleo anayoyaleta Mheshimiwa Dkt. Samia, Rais wetu. Nianze na ujenzi wa Reli ya Mwendokasi. Kama ulivyosema kwenye *Speech* yako, kutoka Dar es Salaam mpaka Morogoro ambayo ina kilomita 300 na inagharimu jumla ya Shilingi za Kitanzania bilioni 792.99 ambazo zinajenga reli hii na kuendelea mpaka Dodoma, yaani inakwenda vizuri, imebakia asilimia kidogo kumalizika.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, tunaomba sana na Watanzania wengi wanaisubiri sana hii reli ambayo Mheshimiwa Rais anaisimamia iweze kukamilika na kuleta manufaa ya kiuchumi, mawasiliano, na mengine mengi ya kuinua pato kwa wananchi na nchi yetu ya Tanzania kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, ushauri wangu kwa upande wa wananchi, hii reli tuisimamie na kuitunza na siyo kuiharibu kama tunavyoharibu miradi mingine wakati mwingine.

Mheshimiwa Spika, mradi mwingine ambao tunajivunia sana ni wa kufua umeme wa Mwalimu Julius Nyerere. Bahati iliyoje tuliyonayo kwa Mkoa wa Morogoro? Hili bwawa liko kwenye Mkoa wa Mororogoro Halmashauri ya Wilaya ya Morogoro Vijijini pamoja na Mkoa wa Pwani. Hii itafua umeme kwa megawati 2015 na inagharimu hela za Kitanzania shilingi bilioni 869.93. Kweli tulijivunia, tulikwena, nami nilikuwepo wakati inawekwa maji na Mheshimiwa Rais alishuhudia maji yanawekwa. Kwa kweli Mheshimiwa Rais tunajivunia sana kwa Bwawa letu la Mwalimu Nyerere.

Mheshimiwa Spika, hili Bwawa la Mwalimu Nyerere licha ya kuwa na lengo la kufua umeme ambao utatosheleza nchi

yetu, ambapo tutaweza kuuza nchi za nje, pia ni kivutio tosha cha utalii kwa watu wa Tanzania, hasa na watu wengine.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo naweza kusema kwa Bwawa la Mwalimu Nyerere, limeleta ajira kwa vijana wetu na hasa vijana wa Mkoa wa Morogoro na Mkoa wa Pwani ambao wanajivunia kuwa na bwawa na Watanzania wote kwa ujumla. Bwawa hili la Mwalimu Nyerere limeweza kukuza Kata na Miji ambayo imeizunguka. Mfano, mzuri ni Kata ya Mvuha pamoja na Kisaki ambayo ukienda unaona kweli maendeleo yanakuja.

Mheshimiwa Spika, sasa tufanye nini? Ushauri wangu; ili kuendeleza na kulifikia hili Bwawa la Mwalimu Nyerere, ili paweze kufikika kwa urahisi, miundombinu mpaka sasa hivi siyo mizuri. Kwa hiyo, nilikuwa nashauri, barabara ya kuanzia Ubena - Mvuha mpaka Kisaki na barabara ya kuanzia Bigwa - Mvuha - Kisaki mpaka kwenye Bwawa la Mwalimu Nyerere ziweze kujengwa kwa kiwango cha Lami ili kusudi liweze kufikika kwa urahisi.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo naomba kuongelea ni kuhusu Mradi wa Sukari pale Mkulazi. Bahati nzuri hii Mkulazi na yenyewe iko kwenye Mkoa wa Morogoro. Kuna Mkulazi Na.1 na Mkulazi Na. 2 ambako kuna kiwanda kinachojengwa pale Dakawa Mkulazi kwa shilingi bilioni 39.84.

Mheshimiwa Spika, ninachoomba ni kuwa, miwa inalimwa ambapo mpaka sasa hivi imeshalimwa na kiwanda kimejengwa na kimefikia asilimia 75. Mara kitakapokamilika, kitazalisha tani 50,000 za sukari; ambapo zitakapozalishwa hizo tani 50,000 zitasaidia kupunguza uhaba wa sukari katika nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ni hekta 2,974 mpaka sasa hivi zimelimwa. Ushauri wangu, wakulima wamejitokeza wengi kutoka Kijiji cha Mbigili, Kata ya Mbigili Wilaya ya Kilosa

ambao na wenyewe wamewekeza kwa wingi, kwa hiyo wamepata ajira. Tatizo lililopo, hawapati maji ya kutosha. Kwa hiyo, nilikuwa nashauri Serikali waweze kuwapa maji, kwa maana ya kilimo cha umwagiliaji kusudi tuweze kuzalisha sukari kwa wingi na wakulima waweze kufaidi katika kazi hii ya kilimo kwenye Mkulazi Na. 1 na Mkulazi Na. 2. Zikifanya vizuri itaweza kwenda vizuri.

Mheshimiwa Spika, mradi mwingine ni ujenzi na ukarabati wa viwanja vya ndege. Naipongeza Serikali na Mheshimiwa Rais kwa kukarabarti viwanja vya ndege vilivyopo kama Geita na Dodoma kama nilivyovitaja na viwanja vingine.

Mheshimiwa Spika, swali langu moja kwa Serikali, ilikuwa ni kiwanja cha Ndege cha Morogoro; kwa niaba ya wananchi wa Morogoro, habari ya hiki kiwanja tulishaiongelea humu Bungeni. Kwa hiyo, naomba kujua hatima yake na bajeti ya fedha ya kiwanja hiki kitajengwa lini, ili kusudi wananchi wa Morogoro pia waendelee kufaidi matunda ya Serikali. Tunamshukuru sana Mheshimiwa Rais.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ni Benki ya Kilimo. Tunamshukuru sana Mheshimiwa Rais anaitolea fedha ambazo mpaka sasa hivi imeshapata takribani Shilingi bilioni 78.54 ambayo imenufaisha wakulima takribani 119,797.

Mheshimiwa Spika, tunavyofahamu ni kuwa, takribani wananchi wa Tannzania asilimia 65.5 wanategemea kilimo. Kwa hiyo, wakulima hawa wamehamasika sana kwenye kilimo, uvuvi pamoja na mifugo. Kwa hiyo, ushauri wangu, kwenye Benki hii ya Kilimo ambayo ni mkombozi kwa mkulima iweze kuongezewa fedha kusudi wanufaika waweze kuwa wengi kwenye benki hii ya kilimo ambayo inapata fedha hizo lakini hazitoshelezi.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo ningeomba kuongelea ni kuhusu masuala ya Lishe. Bila kuwa na lishe nzuri hatuwezi kuwa na Taifa lenye afya na lenye kuendeleza mambo kiutaalamu. Kwa hiyo, nilikuwa nashauri kuwa masuala haya ya lishe tuyachukulie kiundani na twende nayo vizuri. Kwa sababu sasa hivi tunaona kuwa kuna ukondefu ambao umepungua ndiyo kwa jitihada zilizotolewa, lakini tufuate ushauri wa lishe, tuweze kutumia chakula cha lishe.

Mheshimiwa Spika, ushauri mwingine, nilikuwa naomba elimu iweze kutolewa kwenye kliniki...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Kengele imeshagonga Mheshimiwa.

**MHE. CHRISTINE G. ISHENGOMA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana, namalizia kwa kusema kuwa ukatili wa watoto naomba kwa kweli kama ilivyoongelewa humu ndani utiliwe maanani.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi. Nakushukuru sana, na ubaraikiwe na Mwenyezi Mungu. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Ester Nicholas Matiko atafuatiwa na Mheshimiwa Mohammed Lujuo Moni, na Mheshimiwa Saashisha Elinikyo Mafuwe, ajiandae.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa fursa nami kuchangia kwenye bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Spika, nina masuala kadhaa kama manne hivi ambayo naenda kugusia.

Mheshimiwa Spika, kwa kuanzia, kwa masikitiko kabisa, nianze kujielekeza kwa kutokutekelezwa kwa bajeti ambazo tunazipitisha kwenye Bunge lako Tukufu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ukiangalia Fungu Na. 65 ambalo tulitenga takribani shilingi bilioni 26.6 na tukazielekeza kwenye Ofisi ya Waziri Mkuu, (Kazi, Ajira, Vijana na Watu wenye ulemavu), Wizara ambayo ni muhimu kabisa, lakini cha kusikitisha, mpaka kufikia Februari, 2023 zilikuwa zimepelekwa shilingi bilioni 5.5 tu kama asilimia 22 tu. Tulitenga shilingi bilioni tatu kwa ajili ya kukarabati na kujenga vyuo vya watu wenye ulemavu, kundi ambalo ni maalumu kabisa, lakini mpaka leo hata senti moja haijawahi kutolewa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, fedha hizo ambazo tulizitenga, pia ilikuwa ni kwa ajili ya kwenda kukuza kazi ya staha nchini, programu ya kukuza ujuzi, Mpango wa Maendeleo kwa Ustawi wa Taifa na mapambano dhidi ya UVIKO-19, Mfuko wa Maendeleo ya vijana, vyote hivi ni muhimu, lakini bajeti inatekelezwa kwa asilimia 22 tu.

Mheshimiwa Spika, mbaya zaidi, mwaka wa fedha 2022/2023 waliomba shilingi bilioni 26.6; mwaka huu ambao wanaenda kutekeleza mambo hayo hayo, wameomba shilingi bilioni 14 kama fedha za maendeleo. Wametekeleza *below,* lakini pia mwaka huu wa fedha wameomba chini zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tulikuwa tunaomba, Serikali ijielekeze hii Wizara ni muhimu sana. Kila mwaka tafiti zinaonesha vijana takribani 900,000 wanaingia kwenye soko la ajira, lakini ni vijana kati ya 50,000 na 60,000 tu wanaopata ajira. Sasa tunaacha Watanzania zaidi ya 800,000 *plus* bila ajira. Kwa hiyo, hii ni Wizara nyeti sana ambayo ingeweza kuwekeza fedha ikahakikisha ina-*absorb* vijana aidha kwenye sekta zilizo rasmi na zisizo rasmi, na hiyo ni pamoja na makundi ya watu wenye ulemavu kama nilivyosema.

Mheshimiwa Spika, kitu kingine ni kuhusiana na utawala bora. Waziri Mkuu ameainisha jinsi nchi yetu inavyoendelea na utawala bora, nami kwa kweli napenda kutumia fursa hii kipekee kabisa kumpongeza Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwanza kuirejeshea nchi yetu uanachama kwenye *OGP (Open Government Partnership)* ambayo ilikuwa imeondolewa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pili, tulimwona Mheshimiwa Rais anatekeleza kwa vitendo. Juzi aliposema kwa machungu kabisa kwamba anakemea ubadhilifu ambao ulikuwa *inflated* katika manunuzi ya ndege Dola milioni 49 ambazo ni sawa na shilingi bilioni 117 za Kitanzania.

Mheshimiwa Spika, nilijaribu kufuatilia, ile ndege ilikuwa inunuliwe kwa dola milioni 92 ambayo ni sawa sawa na fedha za Kitanzania shilingi bilioni 220. Zikawa zimelipwa *advance payment* dola milioni 55, zikabaki dola milioni 32. Sasa kweli nchi yetu ilivyo sasa hivi, tuna bajeti iyojitegemea, tunategemea wahisani, mikopo na kila kitu. *Balance* imebaki ya dola 32 imekuwa *inflated* kwa dola milioni 86, ongezekeo la dola milioni 49.

Mheshimiwa Spika, ndiyo maana nasema nampongeza Mheshimiwa Rais kwanza kwa kuwa muwazi; pili, kwa kukemea uwajibikaji, pale aliposema, wale wote ambao walikuwa wanahusika na ku-*invoice* hizi *amount,* waweze kuwajibika.

Mheshimiwa Spika, kwa sababu Waziri Mkuu ndio msimamizi wa mambo yote ya Serikalini, Bunge lako Tukufu tungependa, kwanza aje atueleze mpaka sasa hivi, na baada ya ile *statement* ya Mheshimiwa Rais; kama Bunge lazima tuisimamie na kuishauri Serikali, hizi fedha ni nyingi sana. Tungesema tuzielekeze kwenye madarasa, tungeweza kujenga zaidi ya madarasa 5,800 Tanzania. Leo tusingekuwa

tunaona watoto wanalundikana. Juzi nimeona kule Uvinza, Kigoma zaidi ya watoto 2000 wanalundikana kwenye darasa.

Mheshimiwa Spika, tungesema tuzielekeze kwenye ujenzi wa vituo vya afya hizi ambazo wamezi-*inflate* 117 laiti Rais asingeziona zilikuwa zinaenda kupotea ambazo zingeweza kujenga vituo vya afya 234 tuka-*save* maisha ya Watanzania ambao wanakufa kwa kukosa huduma za afya.

Mheshimiwa Spika, tungesema tuzielekeze kwenye kujenga nyumba za walimu, waache kupanga mbali, mvua zikinyesha miundombinu mibaya hawafiki shuleni, watoto wanashindwa kupata elimu, tungejenga nyumba za walimu (ngoja nifanye hesabu zangu) takribani elfu mbili na kitu, kwa sababu tuseme wao *average cost* ni kama Shilingi milioni 40 hivi. Haikubaliki, haiingii akilini, tutakuwa Taifa la ajabu kabisa kuruhusu watendaji hawa kuendelea kukaa na kubadilisha hizi.

Mheshimiwa Spika, nikawa najiuliza, *probably* zimekuwa zikitokea huko nyuma kwa haya manunuzi ya ndege, maana yake najua ndege zilipelekwa Ikulu. Kama haya yalikuwa yanatokea wana-*inflate* hivi, Taifa letu limeweza kudidimizwa kwa kiasi gani?

Mheshimiwa Spika, Waziri wa Fedha, *Pay Master General* anatoka kwake na kila siku anavaa hiyo tai ya Tanzania, na hata leo amevaa kuonesha uzalendo. Tunataka kujua haya yote yanayotokea. Inaumiza sana! Haya yote yanayotokea, imeonekana tu hii. Ni mangapi yanatokea huko ambayo yanapoteza fedha za Watanzania masikini walipa kodi ambao wangeweza kuelekezwa na tukafanya mambo makubwa sana kwenye Taifa letu? Tungechukua hata hizi fedha tukawekeza kwenye utalii wa michezo, tungejenga viwanja vingi sana vya kisasa Tanzania, hata Mataifa mengine yakawa yanakuja tu-*host* michezo hapa, uchumi wetu ungekuwa maradufu.

Mheshimiwa Spika, tungechukua hii fedha ambayo isingeonekana inapotea, tukawekeza kwenye utalii hata utalii wa mikutano, tungepata fedha nyingi sana. Sasa nataka waiokoe hii Serikali. Waziri Mkuu anapokuja hapa ku-*windup* hapa watueleze bayana, *mostly* watendaji kama kweli wameshapisha kama Rais alivyosema. Hata wakipisha, lazima tuangalie *the source of it* ili tuweze kukomesha haya mambo ya ubadhirifu wa fedha Tanzania *once and for all*.

Mheshimiwa Spika, kitu kingine ambacho nataka nigusie, Waziri Mkuu ameonesha hapa kwa kina kabisa.

**WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Spika, Taarifa.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Spika, muda wangu.

**SPIKA:** Bahati mbaya muda wa taarifa huwa unatumika wa yule anayechangia. Mheshimiwa Waziri wa Fedha.

**T A A R I F A**

**WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Spika, naomba nimpe taarifa mchangiaji, amenitaja kwa jina, akataja na tai na hakusema kwamba hivi vitu vinapita vingapi? Nilitaka nimpe taarifa kwamba, utaratibu wa malipo uliowekwa hapa nchini, na niwatoe hofu Watanzania, ni utaratibu imara sana. Hivi vitu haviwezi vikapita pita ovyo ovyo.

Mheshimiwa Spika, moja, hakuna malipo ya kila mwezi yanayoweza kufanyika bila Mheshimiwa Rais kujua. Kwa hiyo, la kwanza, mahitaji yote ya Wizara zote yanapokuja Wizara ya Fedha, tunayapitia tunawianisha na mapato, tunayaombea ridhaa kwa Mheshimiwa Rais. Yakishapata ridhaa ndipo yanakwenda kulipwa.

Mheshimiwa Spika, hata hilo la ndege analolisema, yalipoletwa mahitaji, Wizara ya Fedha tuliona kwamba limekuja lina ongezeko ambalo kama ni la kimkataba lazima tupate ushauri wa Mwanasheria Mkuu. Kama ni la kimkataba na lina mzozo kwamba linabadilika kutoka bei iliyokuwepo ni lazima tupoate maoni ya Mwanasheria Mkuu. Hatukuwa nayo.

Mheshimiwa Spika, vile vile kama lina mkataba, linahusisha *variation,* lazima tujue waliokaa na kuongeza hiyo *variation* mpaka ikubalike. Sasa haya yote hayakuwepo, tukakataa malipo hayo. Kwa utaratibu kwa kimalipo, ilibidi tutoe taarifa pia kwa mamlaka ambayo ndiyo inaidhinisha, na mamlaka ikachukua hatua ya kusema hayo malipo ya aina hiyo yasilipwe. Kwa hiyo, hatua za kinidhamu zitachukuliwa kwa wale ambao wamefanya huo utaratibu wa mwanzo ambao ulihusisha mpaka hizo hatua zikaweza kufika kwetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, niwatoe hofu Watanzania, mifumo ya malipo iko imara, na ndiyo maana tunaongeza nguvu kupambana kule *site* ambako fedha zinaenda, ndiyo maana tumemwongezea fedha CAG, na Mkaguzi wa Ndani. Mheshimiwa Rais akaelekeza uwazi, ambapo ni kitendo kikubwa Mheshimiwa Rais amekifanya.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Rais, angeamua kuweka usiri akaamua kutokuongeza fedha kwa *CAG,* Bunge ambalo *CAG* ndiyo jicho lake msingeweza kutambua tunayoshauri. Kwa hiyo, tumshukuru sana Mheshimiwa Rais. Niwahakikishie Watanzania kwamba hazina yao iko salama na iko mikono salama.

Mimi umasikini wa Watanzania Mheshimiwa Ester sijausoma kwenye vitabu, nauelewa na siwezi kupindisha fedha nyingi za aina hiyo wakati madaarsa yana hali hizo.

Mheshimiwa Spika, naomba nitoe taarifa hiyo.

**SPIKA:** Mheshimiwa Ester Matiko, subiri kidogo. Kwanza unaipokea taarifa ya Mheshimiwa Waziri wa Fedha?

**MHE. ESTHER N MATIKO:** Mheshimiwa Spika, nitakuwa sijitendei haki. Siipokei.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri ametoa maelezo yake, nimesema siipokei. Sasa haya ni malipo makubwa ambayo yanaenda mpaka yanamfikia Rais. Kuna malipo mengine madogo ambayo yanapotea ambayo hayamfikii Mheshimiwa Rais. Kama Taifa, Watendaji Serikalini ambao wamepata dhamana lazima waangalie kwa umakini kabisa. Hili hapa amelielezea vizuri, lakini hayo mengine ambayo yanapita yanaleta ubadhirifu lazima yakemewe. Hii ni *alarming,* tena *alarming* kubwa sana. Kama watu hawatakuwa na *guts* za ku-*inflate* 49 *million dollars, you are talking about 117 billion shillings, it is not a joke!* Yaani anapitisha bila uoga mpaka yanaenda kwa Rais. Rais! Mh!

Mheshimiwa Spika, nilikuwa nataka nizungumzie Mheshimiwa Waziri mkuu ameonyesha hapa na nakubali kabisa, tuwekeze kwenye maendeleo ya watu kwa maana ujenzi wa miundombinu mashule, hospitali, Vituo vya Afya na wewe umesema hapa asubuhi vizuri kabisa. Lakini kama nchi, kama taifa hatujaweza kuwekeza na kuweka jicho kwenye rasilimaliwatu unaweza ukajenga majengo ya kutosha usipokuwa na rasilimaliwatu ya kuendana na majengo uliyoyajenga ni kama vile unafanya kitu hakuna.

Mheshimiwa Spika, ninachukua mfano tu wa kwenye Elimu, kuna upungufu mkubwa sana wa Walimu hasa masomo ya Sayansi, Walimu kwa mfano shule ya msingi kuna upungufu wa zaidi ya asilimia 45. Walimu shule za sekondari kuna upungufu wa zaidi ya 51 na hiyo inakuja ku-*reflect* kwenye matokeo yao mathalani matokeo ya *form two*

ambayo tuliyapigia kelele sana, ufaulu wao kwenye somo la hesabu unaonyesha upungufu wa Walimu ni takribani asilimia 71 *failure* yao ilikuwa asilimia 83 unaweza ukaona zinakuwa *directly related* yaani upungufu wa walimu asilimia 71 una-*reflect* wanafunzi kufeli kwa asilimia 83. Ukija somo la *Physics* upungufu wa walimu asilimia 77 Wanafunzi wakafeli kwa asilimia 82, ukija somo la *Chemistry* upungufu wa Walimu asilimia 64 Wanafunzi wakafeli kwa asilimia 67. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, unafikiri *private* sekta wanafaulu kwa ajili ya nini? Miundombinu *plus* walimu, *input* zote za ufundishaji lazima ziwepo, tutajenga majengo, majengo tutajenga ni *physical things* vinaonekana vya *tangible* wananchi wataona, watatupigia makofi *we are doing good job but in reality, we are killing education of this country,* ahsante. *(Makofi) (Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana, nilikuwa nimeshamtaja Mheshimiwa Mohamed lugio mon atafuatiwa na Mheshimiwa Saashisha Elinikiyo Mafuwe Mheshimiwa Zuberi Kuchauka ajiandae.

**MHE. MOHAMED L. MONNI**: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa nafasi nianze kumshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa mambo makubwa kabisa ambayo anaifanyia nchi hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nashukuru pia kwa hotuba nzuri ya Waziri Mkuu kila mtu humu ndani anafahamu namna ambavyo Waziri Mkuu ni mwema, muungwana ambaye ni rahisi kabisa kufikika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nataka nichangie kwenye maeneo mawili muhimu, Eneo la kwanza ni eneo la maji, moja ya maeneo ambayo yamekuwa na shida kubwa ya maji kwenye nchi yetu hii ni Wilaya ya Chemba ni kwa sababu ya

hali ya kijiografia ni maeneo machache sana ambayo ukichimba maji unapata.

Mheshimiwa Spika, nataka nimshukuru Waziri wa Maji baada ya kuelewa changamoto hizi yapo mambo makubwa sasa Chemba yanafanyika naomba nitaje miradi michache tu ambayo sasa inaendelea. Ninafahamu watanzania wote wanafahamu moja ya changamoto kubwa ya wananchi ni maji. Na hasa maeneo ya vijijni kama kwetu, kwenye eneo langu la chemba kuna miradi mingi inaendelea moja ya miradi hiyo ambayo kwa dhati kabisa namshukuru Mheshimiwa Rais.

Mheshimiwa Spika, kuna mradi wa Kelema ambao una milioni 500, Mradi wa Babayo ambao unaendelea una milioni 500, Mradi wa Kubungo unaendelea unazaidi ya milioni 335, Mradi wa Chandama milioni 550, mradi wa machija una milioni 700 na mradi wa visima 11 vya awali milioni 550. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, haya yanaenda kupunguza kwa kiwango kikubwa upatikanaji wa maji. Naomba nichukue nafasi hii kumshukuru Mheshimiwa Rais lakini pia namshukuru Mheshimiwa Waziri wa Maji. Mara kadhaa kule ambako nimeenda kutoa ushauri ni namna gani tutatue chamgamoto ya Chemba kwa sababu ni maalum ameweza kunielewa na kunisikiliza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika. Pamoja na miradi hiyo lakini pia tuna miradi mikubwa ya mabwawa nimshukuru sana Mheshimiwa Waziri Mkuu jana katika hotuba yake alielea kwa kina namna gani wanaenda kutekeleza mradi wa Bwawa la Farukwa. Kwenye bajeti iliyopita tulitengewa milioni 283 nishukuru watu wako *site* na kazi inaendelea.

Mheshimiwa Spika, kwenye mradi huo kuna jambo la kufanya Mheshimiwa Waziri Mkuu. Ukisoma vizuri andiko la

mradi ule linaeleza linaenda kuhudumia watu milioni 2.5 wa Dodoma mjini haliongelei kokote Habari ya Chemba. Mheshimiwa Waziri Mkuu tumefika kwenye eneo la mradi ukatuahidi na sisi tutapata maji naomba wataalamu wetu waanze kufikiria ni namna gani na sisi tuaenda kupata maji kwenye mradi ule.

Mheshimiwa Spika, nishukuru sana namna ambavyo Katibu Mkuu wa Wizara ya Maji, Waziri wa Maji ambaye mara kadhaa umefika kwenye mradi huo. Lakini pia niwashukuru kumekuwa na miradi ya mabwawa midogomidogo. Tumechimba mabwawa manne kwenye mwaka huu wa fedha lakini pia tuna mradi mkubwa wa bwawa la bilioni tatu pale Chidoka. Kandarasi ilitangazwa tukaenda kumtambulisha mkandarasi lakini Mheshimiwa Waziri Mkuu mpaka leo yule mkandarasi hajawahi kufika sijui nini kinaendelea.

Mheshimiwa Spika, ninaomba sana hebu yule mkandarasi afike kwa sababu tulimchezea ngoma siku ile tunafungua ule mradi sasa akipotea moja kwa moja nauliza sasa zile ngoma tulicheza mbona sasa hivi hayumo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naishukuru sana kwa kweli Wizara ya Maji lakini pamoja na shukrani hizo yapo maeneo naomba wanisaidie tumefanya *survey* wenyewe kwenye vijiji tisa kwa ajili ya kupata maji. Na nafahamu kuna hizi mashine za Uviko zimekuja Dodoma kwa sababu tume *survey* wenyewe kwa gharama zetu kwenye vijiji vya Chang,ombe, Magandi Jinjo, Jangalo, Songoro, Piho, Tandala, Dinai, Takwa tunaomba zile mashine zikaanzie eneo la Chemba kwa sababu ndio eneo ambalo lina asilimia ndogo zaidi ya upatikanaji wa maji kwa Mkoa wa Dodoma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ndani ya miaka miwili hii ya Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan tumepunguza upungufu wa maji kwa asilimia kubwa sana watu ambao

wanafikafika Chemba wanafahamu kwamba miaka miwili iliyopita upatikanaji wa maji ulikuwa ni asilimia 23 sasa hivi tume *jump* mpaka asilimia 36, haya ni mageuzi makubwa sana lakini miradi hii ikikamilika, miradi hii ambayo sasa hivi inaendela tunaenda kupanda mpaka kwenye asilimia 54. Kwa hiyo, nisipomshukuru Mheshimiwa Rais kwa fedha nyingi ambazo zinapatikana nitakuwa siyo muungwana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia naomba nitoe shukrani kwenye eneo la barabara miaka miwili iliyopita bajeti ya barabara ya Chemba ilikuwa ni milioni 700 tu lakini mtandao mzima wa barabara ulikuwa ni kilomita 736 unaweza ukafikiria ni namna gani unaweza kutengeneza unamtandao kilometa 700 halafu unapata bajeti ya milioni 700. Nimshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa sasa tumeongezewa zaidi tunapata bilioni 2.3 angalau maeneo mengi ya vijijini yanaweza kupitika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninaombi kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu. kwa barabara ambayo inatoka Kontoro, Sanzawa, hadi Ntendo lakini pia inavuka eneo la Mto Bibu kwa hiyo bajeti ya bilioni 2.3 hakuna namna ambavyo tunaweza kujenga imeshafanyiwa kila kitu na inahitaji zaidi ya bilioni tatu yenyewe peke yake. Wakati Mheshimiwa Rais amekuja Chemba Dkt. Samia Suluhu Hassan nililisema hilo na tukaahidiwa sasa tuwasiliane na Wizara husika ili kazi ile ikafanyike nikuombe sana Mheshimiwa Waziri Mkuu hebu tusaidie katika hilo maana fedha zinazokuja kwa ajili ya barabara hatuna uwezo wa kutumia maana tulitumia fedha hizo bilioni 2.3 maana yake sasa tutumie fedha zote kwenye barabara moja wakati barabara nyingine zitakuwa zina hali mbaya.

Mheshimiwa Spika, tuna barabara kubwa ambayo imetangazwa kandarasi, barabara ya kutoka Kibarashi, Handeni hadi Singida. Barabara hii zaidi ya kilomita 100 ipo kwenye jimbo langu na ambaye nina uhakika barabara hii

ikijengwa Maisha ya watu wa Chemba itakuwa rahisi sana. Lakini barabara hiyo ina viunganishi vya barabara ambavyo kujenga peke yake itakuwa changamoto nyingine.

Mheshimiwa Spika, ninomba kuna kiunganishi cha kutoka Goima Mondo hadi Bichwa kuunganisha na barabara kuu ya Arusha chenye kilomita kati ya 24 na 28 nacho naomba kiangaliwe namna ya kujengwa lakini si hiyo tu kuna barabara ya kutoka Malamaya kiunganishwe na hiyo barabara eneo la Donsee kilometa kati ya 28 na 26 nazo hizo barabara zinatakiwa zitafutiwe fedha ili ziweze kujengwa kwa hiyo kufanya hivyo tutakuwa tumepata *package* nzima ya barabara yote ambayo hii sasa tunaongelea ya kutoka Kibarashi hadi Singida kwa kiwango cha lami. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo naomba pia kuishukuru Serikali kwa sababu yapo mambo mengi yamefanywa kwenye Afya. Miaka miwili iliyopita Chemba haikuwa na Hospitali ya Wilaya kulikuwa na ujenzi umeanza lakini tumepata fedha zote na hospitali imekamilika zipo changamoto za Watumishi, sasa hivi pale, ipo changamoto ya Gari ya *Ambulance*. Ninakuomba sana Mheshimiwa Waziri Mkuu ikikupendeza kwa sasa hivi hospitali inahudumia watu wengi sana inahudumia watu zaidi ya laki tatu. Kama kuna uwezekano wa kupata gari sehemu yoyote kwa sababu kwa saizi hali iliyopo inabidi tukachukue gari la Kituo cha Afya Mbijo ili lije lifanye kazi kwenye Hospitali ya Wilaya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimuombe sana Mheshimiwa Waziri Mkuu, tatizo hilo limekuwa ni tatizo la muda mrefu na nimewahi kuliuliza kwenye swali la nyongeza lakini nikaahidiwa mpaka sasa hivi hatujapata gari hilo.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema haya nakushukuru sana, kwa nafasi, naunga mkono hoja. Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Saashisha Elinikyo Mafuwe atafuatiwa na Mheshimiwa Zuberi Mohamed Kuchauka Mheshimiwa Justin Lazaro Nyamoga ajiandae.

**MHE. SAASHISHA E. MAFUWE:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi niweze kuchangia kwenye hotuba ya Mheshimiwa Waziri mkuu kuhusu mapitio na mwelekeo wa kazi za Serikali.

Mheshimiwa Spika, kwanza nimshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa kutupa afya na uzima lakini nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa kweli sote tunakubaliana ni mtu wa kazi, ni mtu rahimu sana, ni kiongozi wa mfano wa kuiga Mheshimiwa Waziri Mkuu tunakushukuru na kukupongeza sana. Pia nakupongeza kwa ziara nzuri unazozifanya kwa Taifa letu ukiwa unashughuluka na wale ambao wanaturudisha nyuma Mheshimiwa Waziri Mkuu hongera sana. Napongeza wasaidizi wako wote kwa kazi kubwa wanayoifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa kweli wananchi wa Hai wamenituma kwa dhati kubwa sana kwamba nisimame hapa nimshukuru sana Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na wamenipa lugha yao ya kusema, wameniambia niseme "*nahavachee lakini ashenalee ologhandumaa,* lugha hizi zinamaanisha uzito wa shukurani zikisema asante kwa Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya muungano wa tanzanaia siyo jambo la kawaida leo tunazungumza Mheshimiwa Rais amekanyaga Mkoa wa Kilimanjaro na Wilaya ya Hai mara saba na pale Hai mimi ni mnufaika maana akishuka Uwanja wa Ndege lazima asalimie watu pale Bomang'ombe. Tunamshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa mambo makubwa aliyoyafanya.

Mheshimiwa Spika, kwa kweli acha tuseme tulikuwa na hali mbaya miaka 15 hatukuyaona haya ambayo nitasema hapa, tulikuwa na tatizo la maji pale kata zetu za ukanda wa

chini Bomang'ombe, Bhundugai, Muungano, *KIA* leo Mheshimiwa Rais ametuletea fedha bilioni 3.3 na mradi umeshakamilika watu wa Hai wanapata maji.

Mheshimiwa Spika, nikubalie niseme kuhusu Huduma za Afya, tuna Vituo vya Afya vitano vipya havikuwepo vinajengwa ndani ya Wilaya ya Hai Chekimaji, Mkwansila, Kisikii imekarabatiwa, Luongoi niseme haya ni makubwa sana Mheshimiwa rais anatutendea, ukienda upande wa elimu ndio usiseme shule kongwe kwa maana Machame Girls, Nyamungo zimefanyiwa ukarabati fedha kemkem zimeletwa kwa ajili ya shule zetu chakavu.

Mheshimiwa Spika, kwa kweli wananchi wa Hai wanasema ahsante sana. Barabara ndio usiseme pale Bomang'ombe barabara nne zinajengwa kwa kiwango cha lami na taa juu. Kuna barabara nimehangaika nayo mpaka ilikuwa imepewa majina yasiyofaa leo ni barabara ya lami inajengwa Makoa mferejini tayari kilometa saba mkandarasi yuko *site* na saba nyingine zinakuja tunamshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa haya anayoyafanya.

Mheshimiwa Spika, Viwanda, nimesema hapa jana kiwanda cha *machine tools* kinaunguruma tunaomba tu Serikali sasa ilete zile taasisi zikanunue chuma pale na vipuri lakini pia *common use facilities* mnafahamu kwamba tumeshatengewa fedha nikumbushe wizara ya kilimo wakamalizie kazi hiyo. Skimu za umwagiliaji pale Longo "A" fedha imekuja. Hayo ni mambo makubwa sana Mheshimiwa Rais anayotufanyia nampongeza na namshukuru sana.

Mheshimiwa Spika, niseme pamoja na mazuri hayo Mheshimiwa Waziri Mkuu naomba nikukabidhi hili linaitwa Soko la Kwasadala, kabisa kabisa nenda nalo Mheshimiwa Waziri Mkuu kafanye nalo kazi soko hili lijengwe ni kichocheo muhimu sana kwa uchumi wa Mkoa wa Kilimanjaro. Niombe pia tunashule ya sekondari pale Lemila nimeshaiomba hapa

Mheshimiwa Waziri Mkuu nakukabidhi haya machache najua wewe utaenda nayo pamoja na chuo kile cha Losoa ni ahadi hizi za Serikali nisaidie Mheshimiwa Waziri Mkuu hili nalo likatekelezwe.

Mheshimiwa Spika, naomba kwa haraka sana niguse jambo moja hapa. Hizi kuta zisipochukua kumbukumbu zetu tutakuwa hatujajitendea haki. Kila mmoja aliyeko humu ndani alishika kitabu anachoamini nacho akaapa pale na nitatumia kile ambacho nilikitumia kuapa hapa kuzungumza ambayo yanaendelea kwenye jamii yetu.

Mheshimiwa Spika, kwenye hotuba ya Waziri Mkuu amezungumza Habari ya ukatili wa Watoto. Nitaenda mbali si ukatili wa watoto tu lakini na hiki kinachoendelea cha ndoa za jinsia moja. Asubuhi amenipigia Sheikh Omari, Sheikh wa BAKWATA Wilaya ya Hai akaniambia Mheshimiwa Mbunge msiposema mawe yatasema, semeni huko Bungeni na sisi BAKWATA Mkoa wa Kilimanjaro siku Jumamosi tuna maandamano ya kupinga hizi ndoa za jinsia moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hili mnikubalie ninukuu kitabu cha Biblia ambacho nilishika kuapa hapa. Ukienda Wakorintho wa kwanza 6:9 kasome mambo haya yanakatazwa, ukienda Warumi 1:26-27 yanakatazwa mambo haya ya hovyo yasiyofaa kwenye jamii yetu lakini kwenye sheria na kanuni ya adhabu sura ya 16 inasema, naomba unikibalie nisome ile Ibara ya 154 nanukuu; "Mtu yoyote ambaye; (a) anamuingilia mtu yeyote kinyume na maumbile au anamuingilia mnyama kimwili au anamruhusu mwaume kumuingilia yeye mwanaume au mwanamke kumuingilia kinyume na maumbile atakuwa ametenda kosa atawajibika kwa adhabu ya kifungo cha Maisha wakati mwingine kifungo kisichopungua miaka 30". *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa unyenyekevu mkubwa sana naomba chombo chako hiki kitakatifu kitusaidie kusimamia

haya binafsi nakemea jambo hili vibaya mno. Wale wote wanaojihusisha na ndoa za jinsia moja ni jambo lisilokubalika hii ni laana, sisi ambao tumeshika vitabu vyetu vitakatifu hapa tukaapa tukasema Mwenyezi Mungu atusaidie tutailinda Katiba hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tuanze kuilinda Katiba hii kwa kukemea vikali lakini niombe Mheshimiwa Waziri Mkuu jambo hili lipo chini ya Ofisi yako, wale wote wanofanya mambo haya ambao wanatajwa kwenye jamii ambao wanaonekana Serikali ichukue hatua kutekeleza hili na wachukuliwe adhabu hadharani ili na wengine wajifunze. Mheshimiwa Waziri Mkuu tukiendelea kunyamaza kizazi kinachokuja watafukua makaburi yetu watuchape viboko maana sijui hata kama watakuwepo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, leo mwanaume amuingilie mwanaume uzao unatoka wapi? Mwanamke amuingilie mwanamke uzao unatoka wapi? Mimi niwaombe watanzania kwenye hili tuungane kwa pamoja kukemea vikali sana na niwaombe viongozi wetu wa dini wala wasione aibu maana wakati mwingine watu wanasema watu hawa wana manguvu, wanamanguvu kuliko mungu? Haiwezekani. mwenyenguvu ni mungu na yeye ndio ametuumba na yeye ndio anatukataza haya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya hapo nirudi kwenye hoja kuhusu matumizi ya fedha za Serikali. Kwenye Kamati yetu tumejifunza kitu kigumu sana kinachoitwa bakaa. Utakuta kila Halmashauri inakuambia wamevuka na fedha za mwaka uliopita, lakini fedha hizi zinapokuja sasa kuombewa tena kibali zinatumika nje ya utaratibu na unakuta zipo ambazo zimebaki na ukiwauliza hizo ambazo zimebaki zipo katika akaunti gani, hawakuambii

Mheshimiwa Spika, ningeomba waende wafanye mapitio ya sheria ile ya bajeti ya mwaka 2015 kifungu cha

*21(1)(4)* ambacho kinampa *pay master general* nguvu baada ya fedha kuvuka mwaka anaambiwa anaweza wakileta maombi anaweza kukubali sehemu ya maombi yale au kukubali yote au kutokukubali.

Mheshimiwa Spika, sasa kifungu hiki kinapora madaraka ya Bunge kwa sababu sisi tumeshapitisha bajeti hapa kwamba kituo cha afya kikajengwe. Kwa sababu tu ya uzembe wa watu wachache, wameshindwa kutekeleza miradi, fedha imevuka mwaka sasa tunaambiwa tuombe upya na bado *Pay Master General* anapewa *mandate* ya kukubali au kutokukubali ilhali sisi tumeshapitisha hapa.

Mheshimiwa Spika, na jambo hili tusipoangalia fedha nyingi za wananchi wa Tanzania itapotea; na inapotea si kwamba wananchi ndio wamekosea eti kuna mkurugenzi eti kuna afisa mipango ameshindwa kuwasilisha *reconciliation* za mahesabu yake kwa hiyo anayeadhibiwa sasa ni mwananchi kwa kutokujenga kituo cha afya.

Mheshimiwa Spika, jambo hili halikubaliki, halikubaliki kabisa. Tunawapa wananchi adhabu ya kukosa miradi kwa sababu eti watu watu hawakufunga hesabu. Mimi naomba sana jambo hili liweze kutazamwa vizuri ili tuweze kwenda kwenye uwajibikaji na yale ambayo tumeyapanga yaweze kufanyika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, na hili ni sambamba pia, nimesoma kwenye Hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, anasema vyama vinavyopewa ruzuku wamepewa bilioni 17.5 na akataja; kuna chama cha *NCCR* Mageuzi, CCM, CHADEMA, *DP*, *CUF*, *ACT* Wazalendo; na huko wakaangalie bakaa, kama kuna fedha zilivuka mwaka tuambiwe zitatumiwaje, kama hazikutumika mwaka huu wa fedha, sasa hizi bakaa zinaenda kutumikaje?

Mheshimiwa Spika, nimeona umeshashika *mic,* ishara ya kwamba nimemaliza muda wangu; nakushukuru sana naomba kuunga hoja mkono. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Zuberi Mohamed Kuchauka, atafutaiwa na Mheshimiwa Justin Lazaro Nyamoga, Mheshimiwa Kenneth Ernerst Nollo ajiandae.

**MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA:** Mheshimiwa Spika, nikushukuru kwa nafasi, lakini awali ya yote nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha mimi na sisi sote tuliomo humu ndani kuamka salama tukiwa na afya njema. Vilevile nielekeze shukurani zangu za dhati kwa Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa namna anavyolitendea haki Taifa letu na kwa namna anavyopambana katika kutekeleza Ilani yetu ya Chama cha Mapinduzi. Pia nimshukuru sana Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa hotuba nzuri iliyosheheni kila mahali na ufafanuzi wenye viwango.

Mheshimiwa Spika, mimi nitajielekeza kwenye mambo mawili makuu. Wakati naingia kwenye Bunge hili nilisema kwamba Wilaya ya Liwale ilikuwa kisiwani. Wakati ule wilaya ya Liwale ilikuwa kisiwani kwa sababu ilikuwa haifikiki kwa barabara wala kwa mawasiliano ya simu; lakini kwa namna Chama cha Mapinduzi kinavyotekeleza Ilani yake nashukuru kusema leo hii Wilaya ya Liwale inafikika kwa mawasiliano ya simu kwa zaidi ya asilimia 80.

Mheshimiwa Spika, lakini bado Wilaya ya Liwale ipo kisiwani kwa upande wa barabara. Kwa uelewa wangu mimi barabara ni kama mshipa wa damu kwenye mwili wa mwanadamu. Wilaya ya Liwale kipato chetu kipo chini sana na hali ya maisha ni ngumu sana, ni ghali sana kwa sababu ya barabara. Ili mazao ya mkulima yafike kwenye masoko yanahitaji barabara.

Mheshimiwa Spika, na kwa mwaka huu na miaka ya hivi karibuni tumepata miradi mingi sana kwenye halmashauri zetu. Hata hivyo Wilaya ya Liwale utekelezaji wake unakuwa mgumu kwa sababu gharama ya usafirishaji wa malighafi kupeleka *site* ni kubwa sana kutokana na ubovu wa barabara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimezungumza mara nyingi kuhusiana na barabara ya Nachingwea – Liwale mpaka Masasi, barabara hii upembuzi yakinifu umeisha mwaka 2014. Leo tukiambiwa kwamba Serikali inatafuta fedha za ujenzi wa barabara hii akili yangu ya kawaida inakataa, kwa sababu ziko barabara zilizofanyiwa upembuzi yakinifu 2015, 2016, 2017, 2018 zimeshajengwa. Hii maana yake ni nini? Maana yake ni kwamba utashi wa kujenga hii barabara bado haupo Serikalini, Serikali bado haijaona umuhimu wa kujenga barabara hii. Naomba sana Barabara hii ya Masasi – Nachingwea – Liwale ijengwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, na mimi nataka niseme ukweli kwamba shida yangu si kwenye bajeti; nimedumu kwenye Kamati ya Miundombinu miaka saba; maika yote saba barabara hii imekuwa ikitengewa fedha lakini haijengwi. Naomba sana Serikali, maendeleo haya yote ambayo tunayosema tumeletewa sisi Wilaya ya Liwale; upande wa elimu, afya na wa kilimo, kama hatutaweza kupata barabara ya uhakika haya yote kwetu yatakuwa ni kazi bure. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini barabara ya pili ninayoweza kuizungumza ni Barabara ya Nangurukuru – Liwale, barabara hii inazaidi ya Kilometa 230, upembuzi yakinifu umeisha kwenye baketi iliyopita ya mwala 2021/2022. Ninaiomba sana Serikali waone umuhimu wa kujenga hii barabara ili na sisi tuweze kutoka kuwepo kule kisiwani.

Mheshimiwa Spika, na nikienda mbali zaidi, Mheshimiwa Waziri wa Fedha kwenye bajeti ya mwaka jana alisema

mwenyewe kwamba hii barabara kwenye bajeti ya mwaka 2022/2023 itajengwa; lakini mpaka leo hakuna chochote kinachoeleweka kwetu watu wa Liwale. Tuliambiwa hii barabara inajengwa kwenye huu mradi wa *EPC+F* sijaelewa mpaka leo hii *EPC+ F* imeishia wapi na sisi tuna shida ya hii barabara ya Nachingwea – Masasi – Liwale.

Mheshimiwa Spika, lakini barabara nyingine ambayo naweza kuizingumzia, ambayo inaweza ikatutoa sisi kisiwani ni barabara ya Morogoro. Naomba sana Serikali yangu ya Chama cha Mapinduzi tuitoe Liwale kisiwani.

Mheshimiwa Spika, pointi nyingine, naomba niende sasa kwenye upande wa maliasili. Kwa upande wa maliasili huku nako kuna uelewa mdogo sana wa jiografia ya nchi yetu. Kwenye bajeti ya mwaka 2021 tuliletewa fedha kutoka *World Bank* kwa ajili ya kuendeleza utalii kusini lakini sisi Mkoa wa Lindi, Wilaya ya Liwale hela zile hatukupata. Nilipokuja kuuliza humu nikaambiwa kwamba eti fedha zile zimekwenda Songea, Morogoro na Mbeya, Nyanda za Juu Kusini, kwa hiyo sisi Liwale hatupo. Kwa bahati mbaya Mwenyezi Mungu naYe ana karama zake, Mheshimiwa Rais wa Awamu ya Tano akalipandisha hadhi *Pori la Selous* kuwa Hifadhi ya Mwalimu Nyerere, asilimia 60 ya hifadhi iko Liwale. Sasa wale waliosema kuendeleza utalii wa kusini wakimaanisha ni Mbeya, Songea na Morogoro kwa sababu wao ndio Nyanda za Juu Kusini wameumbuka kwa sababu tayari *TANAPA* ipo Liwale na Mkoa wa Lindi.

Mheshimiwa Spika, lakini hapo hapo utakuta kuna Mradi wa Bwawa la Mwalimu Nyerere. Mimi nisikitike sana, kama Bwawa la Mwalimu Nyerere mkaiweka Lindi tofauti na hiyo mnaikosea sana. Kwa sababu asilimia 60 ya Pori ya Selous iko Liwale. Sasa unapokwenda kutengeneza mradi ukasema Mradi wa Bwawa la Mwalimu Nyerere iko Pwani na Morogoro, mimi siwaelewi. Mimi nawaomba sana Watendaji

hebu nendeni mpitie jiografia ya Nchi yetu, mnaposanifu hii miradi pitieni jiografia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, maji ya Bwawa la Mwalimu Nyerere kwa asilimia 60 yapo Liwale, nendeni mkapitie jiografia. Mito yote tunayoitegemea kupeleka maji, Mto Rwebu, Mto Mbarang'andu, Mto Mbwemkuru yote hii imetoka Liwale. Hebu nendeni mkaangalie ramani hiyo, kututenga sisi na Bwawa la Mwalimu Nyerere mnatukosea sana.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine kwa upande wa Maliasili…

**SPIKA:** Mheshimiwa Kuchauka ngoja, na mimi nataka nielewe maana mimi sitoki Liwale; lile Bwawa la Mwalimu Nyerere pale lilipo ni Liwale? Wewe ni Mbunge wa pale?

**MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA:** Mheshimiwa Spika, lipo, ukitaka kulifahamu lile Bwawa lilipo, ukichukua zile heka zote ambazo zimetajwa kwenye Bwawa la Mwalimu Nyerere, nendeni mkaangalie ramani tunapopakana sisi na Songea…

**SPIKA:** Usitutume, usitutume kwenda kuangalia mimi ninazungumza na wewe, pale mahali bwawa…

**MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA:** Mheshimiwa Spika, jibu ni ndiyo.

**SPIKA:** Umeeleza kwenye maelezo yako, kwa nini nakuuliza, kwa sababu umeeanza kwa kusema mito inayopeleka maji kwenye lile bwawa inatoka Liwale. Kwa hiyo mito inayopeleka iko Liwale na Bwawa pia lipo Liwale.

**MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA:** Mheshimiwa Spika, jibu ni ndiyo kwa sababu sehemu ya bwawa lile ipo Liwale.

**SPIKA:** Sehemu ipi ya bwawa? Maana tulishaenda pale, tulimsindikiza Mheshimiwa Rais kubonyeza kile kitufe ili maji yaanze kujaa. Sehemu ipi ya lile bwawa?

**MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA:** Mheshimiwa Spika, upande wa kusini na upande wa magharibi wa lile bwawa iko Liwale. Mahali ambapo tunapakana na Mahenge na tunapakana na Kilwa.

**SPIKA:** Mheshimiwa Kuchauka unajua inabidi ukatafute hiyo ramani uniletee hapa mbele. Kwa sababu wewe upo Mkoa gani?

**MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA:** Mheshimiwa Spika, Mkoa wa Lindi, ndiyo

**SPIKA:** Kwa hiyo, Mkoa wa Lindi sasa hivi lile bwawa lipo Mkoa wa Lindi?

**MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA:** Mheshimiwa Spika, lipo sehemu ya Mkoa wa lindi.

**SPIKA:** Usiseme sehemu…

**MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA:** Mheshimiwa Spika, mimi nasema lipo Mikoa Mitatu, Pwani, Morogoro na Lindi.

**SPIKA:** Mimi nataka nikuelewe, Mheshimiwa Kuchauka kama ukisema kuhusu maji basi maji yanatoka kila mahali. Nataka nielewe hoja yako, mahali bwawa lilipo, pale ni Lindi?

**MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA:** Mheshimiwa Spika, ndiyo.

**SPIKA:** Pale ni Lindi?

**MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA:** Mheshimiwa Spika, ndiyo.

**SPIKA:** Sawa, kaa, ngoja tufuate hiyo ramani kwanza halafu utakuja kupewa nafasi. Maana naona tusije tukapata upotoshaji hapa wa ziada, sijui kama Serikali mtu wa nishati yupo hapa? Hebu tuelezee kidogo hiyo ramani maana tunaweza kujikuta tumeenda Lindi, Mheshimiwa Waziri Mkuu anatoka Lindi, sasa kumbe bwawa liko Lindi bwana, sisi kila siku tunasema Morogoro tunasema Pwani, hebu tuelezee.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru. Naomba kutoa taarifa kwamba Mheshimiwa Kuchauka alinifuata na kunipa hiyo taarifa yake lakini nikamwambia sisi kama Serikali kwa uelewa wetu na mipaka na ramani tulizokuwa nazo, bwawa lipo katika Mkoa wa Pwani na Morogoro. Ndio uelewa tuliokuwa nao, na nikamsisitiza kama anauelewa tofauti basi atusaidie ili na sisi tujifunze. Alikuwa anazungumzia *CSR* na nikamwambia sisi kwa uelewa wetu na ufahamu wetu Bwawa lipo katika Mkoa wa Pwani na Morogoro. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa umemaliza? Nilichokuuliza, Mheshimiwa Naibu Waziri umemaliza eeh?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Spika, nimemaliza.

**SPIKA:** Haya kuna maelezo nyuma yako hapo, Mheshimiwa.

**T A A R I F A**

**MHE. DKT. ENG. LEONARD M. CHAMURIHO:** Mheshimiwa Spika, nilikua naomba kumpa taarifa muongeaji kwamba ni kweli bwawa liko Mkoa wa Pwani lakini *catchment area* litakapojaa ndio asilimia hiyo nyingi ipo Liwale.

**SPIKA:** Sawa sasa, naomba tusaidie kwa sababu wewe unatatupeleka vizuri. Kwa hiyo Bwawa la Mwalimu Nyerere

liko wapi? lipo Mkoa gani? Maana umesema litakapojaa, sasa litakapojaa sasa maana yake litaendelea kutawanyika huko linakoelekea. Sasa hivi tukisema hivi, Bwawa la Mwalimu Nyerere litakalo zalisha umeme kilowati 2,115, liko wapi?

**MHE. DKT. ENG. LEONARD M. CHAMURIHO:** Mheshimiwa Spika, nadhani hapo mchanganyiko unakuja kwenye bwawa ni nini? Kwa sababu ile *infrastructure* iliyojengwa ile miundombinu iliyojengwa ipo Mkoa wa Pwani lakini litakapo…

**SPIKA:** Haya, ngoja, lile jengo. Wewe mwenyewe umesema pale palipojengwa na maji yatakayojaa tumeyatenganisha? yaani yametangana?

**MHE. ENG. LEONARD M. CHAMURIHO:** Mheshimiwa Spika, ndiyo.

**SPIKA:** Kwa hiyo pale palipojengwa ni mkoa mwingine, patakapojaa ni mkoa mwingine?

**MHE. ENG. LEONARD M. CHAMURIHO:** Mheshimiwa Spika, patakapojaa si mkoa mmoja tu ni huu Mkoa wa Pwani, Liwale…

**SPIKA:** Swali langu lililonifanya nimuulize Mheshimiwa Kuchauka si bwawa litaenda umbali gani? Hoja yangu Bwala la Mwalimu Nyerere liko Mkoa wa Lindi au liko Pwani na Morogoro ndiyo hoja iliyoko hapo.

**MHE. ENG. LEONARD M. CHAMURIHO:** Mheshimiwa Spika, lile liliojengwa lipo liko Mkoa wa Pwani lakini maji yakijaa ni mikoa minne.

**SPIKA:** Sasa ukianza maji yatakayojaa maana yake hata maji yanapotoka nako basi ni bwawa, maana hayo maji yanayojaa pale yanatoka mahali. Sasa jamani, ngoja ngoja

tusijichanganye wenyewe tusiwachanganye wananchi. Bwawa la Mwalimu Nyerere ukianza kusema litakapojaa litaenda mbali mpaka wapi, mimi ninafikiri tusiende huko na maji yatakapojaa mengine yataelekea wapi mimi nadhani tusiende huko la sivyo tutachanganya mambo na tutawachanganya wananchi. Kama zipo huduma ambazo zinahitajika kupelekwa Liwale kwa yale maji yanayojaa pale hilo ni suala lingine, lakini hatuwezi kusema bwawa sasa kijiografia liko wapi? Liwale. Sasa maana yake Morogoro limetoka na Pwani limetoka likahamia huko Liwale. Je, maji kama hayakujaa kiasi hicho cha kufika huko Liwale? Tunalihamishaje hilo bwawa? *(Kicheko)*

Mimi ninafikiri tutumie jiografia tena ile ya shule ya msingi kabisa, Bwawa la Mwalimu Nyerere Mheshimiwa Kuchauka kwa ufafanuzi huu uliotolewa kama umeelewa, liko mkoa gani? Ili nikuruhusu uongee, la si hivyo itabidi uniletee ramani inayoonyesha pale Liwale ipo wapi kwenye lile bwawa.

Mhesimiwa Kuchauka.

**MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA:** Mheshimiwa Spika, labda sikueleweka. Tunapozungumzia Bwawa la Mwalimu Nyerere sio pale tu mahali ambapo bwawa limejengwa. Tunapozungumza ujenzi wa Bwawa la Mwalimu Nyerere kuna *yard* ambayo yenyewe imejengwa na eneo lote lililochukuliwa ndiyo maana Mheshimiwa pale akasema kuna *catchment area,* kwa hiyo ile area imekusanya mikoa mitatu, ambayo ni Mkoa wa Morogoro, Mkoa wa Lindi na Mkoa wa Pwani, maana yangu ilikuwa ni hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunapozungumzia bwawa kama …

**SPIKA:** Nimeshakuelewa. Bwawa la Mwalimu Nyerere sasa hivi liko wapi? Wewe nijibu kijiografia tu, liko wapi? Sasa hivi tunapozungumza, liko Mkoa gani?

**MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA:** Mheshimiwa Spika, liko Mkoa wa Pwani.

**SPIKA:** Ahsante sana, malizia mchango wako.

**MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA:** Mheshimiwa Spika, bado niko upande wa maliasili. Kwa upande wa maliasili, kwanza niishukuru Serikali kwa namna inavyopambana na wanyamapori jamii ya tembo. Sisi Wilaya ya Liwale mwaka huu tuliletewa mahindi, namshukuru Mheshimiwa Rais kwa kutuletea mahindi ya msaada ambayo yameuzwa kwa shilingi 700, ili kufidia yale madhara ambayo wananchi wetu walipata madhara baada ya mazao kuliwa na wanyama hawa tembo.

Mheshimiwa Spika, lakini ninaiomba Serikali kwenye hatua hii, tuongeze bidii ya namna gani ya kupata nafasi ya kwenda kudhibiti wale wanyamapori. Kwa sababu mwaka huu tayari tumeletewa mahindi; na sisi Liwale hatuletewi mahindi kwa sababu ya hali ya hewa, hatuna ukame wa kushindwa kulima kupata mazao ya chakula, tulipatwa na njaa kwa sababu ya wanyamapori.

Mheshimiwa Spika, sasa mimi ombi langu, kama Serikali itashindwa kabisa kabisa kudhibiti hawa wanyamapori basi hayo mahindi mwakani tusiletewe kwa kununua, tupewe bure, kwa sababu hali yetu bado ni mbaya; wakulima wanakaa mashambani wanahama mashambani kwa sababu ya athari za wanyamapori jamii ya tembo. Tuliahidiwa kujenga vituo kwenye kata ya Lilombe, bado kituo kile hakijajengwa, tuliahidiwa kujenga kituo Kata ya Mkutano, Kijiji cha Nakipulyungu, bado hakijajengwa, tuliahidiwa kujengwa kituo Kata ya Mlembwe katika Kijiji cha Ndapata bado kituo kile hakijajengwa. Vituo hivi vikijengwa na askari wakiwepo hapo tutaweza kupata nafuu kidogo wakulima wakaweza kuvuna mazao yao.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine naomba nizungumze kuhusiana na Wizara ya Mambo ya Ndani. Wilaya ya Liwale kwa jiografia yake kituo chetu kile kidogo cha polisi pale hakina kituo cha karibu cha kweza kupata msaada wa kipolisi. Wizara walikuja wakatuahidi kujenga vituo viwili vya msaada ili kuisaidia Liwale kiusalama. Tuliambiwa tutajengewa Kituo cha Polisi kwenye Kata ya Lilombe, tukaambiwa kitajengwa Kituo kingine cha Polisi kwenye Kata ya Kimambi, lakini bado miradi hii haijakamilika. Hata hivyo, mimi niende mbali zaidi, hata Kituo chenyewe cha Polisi pale Liwale Mjini, nitasema hapa, kwamba ilikuwa ni nyumba ya mtu binafsi polisi wakapanga mpaka leo.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo kile kituo…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Kuchauka kengele ya pili imegonga, Sekunde 30 malizia.

**MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA:** Mheshimiwa Spika, ombi langu, pamoja na kwamba mimi nilitoa milioni 10 kwa ajili ya Mfuko wa Jimbo kujenga kituo kile lakini bado Serikali haikutupatia fedha kujenga kituo cha polisi katika Mji wetu wa Wilaya ya Liwale.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja, ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Justin Lazaro Nyamoga atafuatiwa na Mheshimiwa Kenneth Enerst Nollo, Mheshimiwa Jackson Gideon Kiswaga ajiandae.

**MHE. JUSTIN L. NYAMOGA**: Mheshimiwa Spika, awali ya yote nichukue nafasi hii kumshukuru mwenyezi Mungu kwa kutupa nafasi tena ya kuweza kuchangia hoja hii. Nichukue

fursa hii pia kumpongeza na kumshukuru Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa jinsi ambavyo ameendelea kutekeleza majukumu yake kwenye miradi mbalimbali na wananchi wa Kilolo wamenituma nishukuru sana kwa mambo mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, orodha ni ndefu sitaweza kuimaliza, lakini tushukuru kwamba baada ya miaka 30 ya kusubiri ameweza kutoa fedha kwa ajili ya ufufuaji wa mashamba ya chai ambayo yalikuwa yametelekezwa kwa miaka mingi. Pia zimetolewa fedha za ruzuku ya mbolea na wananchi wa Kilolo wamenufaika sana tunashukuru sana. Pia imetolewa fedha kwa ajili ya ukuzaji wa miche ya parachichi ambayo mkulima alikuwa ananunua kwa shilingi 5,000 na watu wa *TARI* wametuahidi kuuza kwa shilingi 1,000, ni punguzo kubwa na naamini kwamba wananchi watanufaika, tunamshukuru sana Mheshimiwa Rais. Iko miundombinu ya afya, lakini pia iko miundombinu ya elimu, kwa uchache wa muda kwa ujumla wake tunamshukuru sana Mheshimiwa Rais.

Mheshimiwa Spika, nichukue fursa hii pia kumpongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa kazi anayoifanya na nimkaribishe sana Kilolo kwa ahadi yake kwa ajili ya kuja kuhamasisha kilimo cha parachichi, tunamkaribisha sana Mheshimiwa Waziri Mkuu wananchi wa Kilolo wanamsubiri.

Mheshimiwa Spika, napenda nijielekeze sana kwenye suala la vijana hasa utaratibu wa ajira na kwenye changamoto mbalimbali wanazozipata kwenye masomo. Jambo la kwanza ambalo ningependa kuzungumza ni utaratibu wa ajira kwa vijana wanaojitolea kwenye taasisi mbalimbali hasa kwenye sekta ya elimu na sekta ya afya.

Mheshimiwa Spika, tulishatoa ushauri mara kadhaa tukiwa kwenye Kamati kwamba utengenezwe mfumo maalum wa vijana kujitolea na huo mfumo uanzie jinsi vijana wanavyopatikana. Tukianza kuangalia jinsi vijana

wanavyopatikana utengenezwe mfumo ambao hautoi upendeleo. Tukiacha hivi hivi maana yake ni kwamba mtoto wa Mwalimu ndiye atakayejitolea, mtoto wa mkulima hatajitolea na watoto wa watu wengine watajitolea na wengine hawatapata nafasi ya kujitolea. Tuanze na jinsi gani vijana watatakiwa kujitolea.

Mheshimiwa Spika, kitu cha pili, wale vijana wakishajitolea kuwe na mfumo mzuri wa ufuatiliaji ili ule mserereko inapofika wakati wa kuajiriwa waweze kuajiriwa. Sasa hivi hata namna wanavyopatikana wanavyoingia kujitolea bado haiko sawa na Serikali inajua wako vijana wanajitolea, waliingiaje? Ni rahisi kupanga namna wanavyoingia ili kuwafuatilia kwa sababu tukiacha hivi, kwa sababu watu ni wengi hata kuingia kujitolea nayo ni fursa. Kwa hiyo tuangalie namna vijana wanavyoingia kujitolea na jinsi wanavyolelewa mpaka wakati wa kuajiriwa ili uwe mserereko na huo unaweza ukatengenezwa mwongozo ambao Serikali inaweza ikautumia kuhakikisha kwamba kuna utaratibu mzuri hata wa kuingia kwenye kujitolea.

Mheshimiwa Spika, jambo la pili bado linahusu ajira na jinsi ya upatikanaji. Siku za karibuni kumekuwa na vijana wanaokwenda JKT. Wanapofika JKT unafika wakati wa kwenda kujiunga na jeshi, hizo nafasi zinatolewa pale lakini hakuna uwazi wa jinsi vijana wanavyotolewa JKT na kuingia kwenye ajira. Matokeo yake ni vi-*memo* vingi vya vijana walioko JKT kwa Wabunge na viongozi tuwasaidie wajiunge na jeshi. Serikali iandae utaratibu mzuri na iweke uwazi kwa vijana wanaokuwa JKT ili wanapoingia jeshini nafasi zinapotolewa kuwe na uwazi ili vijana wale wasiwe wanasema leo wamechukuliwa watatu, ni ndugu pengine wa mtu fulani, kuwe na uwazi wa kueleweka ili Serikali inapowachukua kila mtu aridhike. Wale vijana wanaotoka JKT zile nafasi hazitoshi wale vijana wanaotoka JKT ambao hawakuajiriwa watoke wakiwa wameridhika, lakini kwa utaratibu wa sasa siyo wa wazi, una malalamiko na

manung'uniko makubwa na siyo *fair* kwa vijana kutokujua uwazi huo umefanyika kwa kiasi gani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, bado niko kwenye vijana na kwenye sehemu ambazo kidogo zina changamoto. Sijajua kigugumizi cha kuwakopesha vijana wanaosoma vyuo vya kati kinatoka wapi? Vijana hao ni watoto wa maskini, vijana hao wakimaliza vyuo tunawaajiri sasa hivi tuna zahanati, *pharmaceutical technician,* tuna *lab technician* wametoka kule. Kwa nini vijana ambao ni wa vyuo vya kati hawapewi mikopo na wakati wa kuajiriwa wanaajiriwa? Wakati wao pia ni watoto wa maskini wakati ada zao nyingine ni ndogo? Tumeongea muda mrefu hapa lakini Serikali haitoi majibu ya kueleweka kuhusu vijana wa vyuo vya kati kupata mikopo?

Mheshimiwa Spika, niiombe sana Serikali na nimwombe sana Mheshimiwa Waziri Mkuu, tunao vijana wengi sana ambao wako vyuo vya kati na wao pia wana haki ya kupata mikopo kama wanavyopata vijana wa vyuo vikuu.

Mheshimiwa Spika, jambo la mwisho kuhusiana na vijana, ni uunganishaji wa miradi hii inapotengenezwa. Nataka nitoe mfano, hivi karibuni kulitokea tangazo la miradi ya *BBT*. Naishukuru sana Serikali kwa ubunifu mzuri, lakini kwenye maeneo yetu kuna vikundi vya vijana vya 10% ambavyo vinajihusisha na kilimo. Sasa ilikuwa ni rahisi ku-*search* vijana ambao tayari wako kwenye kilimo kupitia kwenye mikopo ya 10% na kuwaingiza kwenye *BBT* badala ya kuchukua vijana wapya ambao watatakiwa kuanza upya na hawa vijana wenye 10% ambao wana mikopo tayari wana mashamba ndiyo maana walikopa na *interest* yao ni kulima na ndiyo maana wamekopa mikopo ya kilimo. Kwa hiyo kama tungechukua vijana wale maana yake ni kwamba ni rahisi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi naomba *BBT* itakayofuata tuchukue vijana waliokopa mikopo ya 10%, wafundishwe kwa

sababu tayari ni wakulima, wako kwenye kilimo na ndiyo *interest* yao badala ya kuchukua vijana wapya na hao vijana wa 10% wako waliomaliza vyuo vikuu na wanataka kulima. Kwa hiyo itakuwa rahisi zaidi wao kwenda na kilimo kuliko mpya ambaye ametafuta tu fursa. Napendekeza kwamba hilo liangaliwe ili vijana waendelee kupata mikopo.

Mheshimiwa Spika, nitakuwa sitendi haki kwa kuwa pia watu wengi wamezoea kuniita mchungaji hapa kama sitazungumzia suala hili la mambo ya mahusiano ya jinsia moja ya ushoga na haya mambo mengine yanayoendelea ya unyanyasaji wa watoto. Pia nitakuwa sijakitendea haki kizazi hiki na kizazi kijacho.

Mheshimiwa Spika, Tanzania hii sisi kama viongozi inabidi tukemee kwa nguvu zote aina yoyote ya unyanyasaji wa kijinsia kwa watoto wetu walioko majumbani na kwenye taasisi. Niipongeze Serikali imepiga marufuku watoto wadogo kwenda shule za bweni, lakini nafikiri kuna hatua zaidi ya kuchukua tena nilikuwa najiuliza ni kigezo gani kilisema la tano ndiyo wanakuwa wameshafikia kwenda *boarding*? Kwa sababu kwa kawaida kulitakiwa kuwe na kigezo kwamba darasa la tano wana umri gani badala ya kuangalia darasa, tungeangalia umri kwa sababu wengine darasa la tano na bado ni watoto wadogo, lakini kwa ujumla wake ni vizuri tukatengeneza mifumo maalum ya kuwalinda watoto.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine hatuwezi kufundishwa na Taifa lolote jinsi sisi tunavyoweza kukuza mila na tamaduni zetu. Sisi wenyewe tunao uwezo wa kuelewa tunachotaka kukifanya, tunao uwezo wa kuamua namna mahusiano tunaweza kuwa nayo ambayo ndiyo yalijengwa na ndiyo yaliyosababisha sisi tuzaliwe. Kwa kweli tutajenga Taifa zuri kama tutaendelea kuheshimu mila, taratibu na desturi zetu katika mazingira yoyote yale na hapo tutakuwa pia tumelinda imani zetu ambazo sisi sote tunaabudu kwazo na tena kipindi hiki ni miezi mitakatifu kwa kila mmoja. Naomba

sana sana kila Mtanzania aone haja ya kuwajibika katika kulinda Taifa letu kwa kutunza mila na desturi zetu.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Kenneth Ernest Nollo atafuatiwa na Mheshimiwa Jackson Gideon Kiswaga na Mheshimiwa Moshi Selemani Kakoso ajiandae.

Waheshimiwa Wabunge, kabla ya Mheshimiwa Kenneth hujaanza kuzungumza nimeletewa ujumbe hapa kwamba kuna mgeni ambaye hakupata nafasi ya kutambulishwa asubuhi na huyu ni Ndugu John Joseph Mgango, mgeni wa Mheshimiwa Naibu Waziri wa Nishati, Mheshimiwa Byabato. Huyu ni mmoja kati ya watu waliotunga Wimbo wa Afrika Mashariki, kwa upande wa Tanzania yeye ndiyo alituwakilisha kwenye kutunga wimbo. Karibu sana Bungeni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Kenneth Nollo.

**MHE. KENNETH E. NOLLO:** Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua nafasi hii kwa dhati nikushukuru kwa kunipa nafasi niweze kuchangia kwenye Bajeti hii ya Ofisi ya Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Spika, ningependa nichangie maeneo matatu. Kwanza ni suala zima la kilimo katika Mkoa wa Dodoma, lakini suala zima la ukuaji wa viwanda hapa nchini na suala la utoaji wa huduma za elimu na afya hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, mwaka jana nilirudia katika mchango wangu kwa Wizara ya Kilimo kwamba Mkoa wa Dodoma ni lazima uchukuliwe kwa hali ya tahadhari kwa upekee ulionao kwamba hatupati mvua ya kutosha. Kwa kweli tumekuwa wahanga kila mwaka sisi hatupati mvua za kutosha na mwaka huu vile vile hatujapata mvua za kutosha na mwakani hatutapata mvua za kutosha na 2025

hatutapata mvua za kutosha kutokana na hali yetu ilivyo hapa.

Mheshimiwa Spika, nimekuwa na *challenge* mara nyingi kwamba tunahitaji tuwe na sera ya kilimo katika maeneo kame ikiwepo Mkoa wa Dodoma. Mkoa wetu nataka niseme Serikali bado inahitaji nguvu kuwekeza. Tunapata mvua kidogo kama nilivyosema, lakini ukija kwenye suala la pembejeo sisi tumekuwa siyo watumiaji wa mbolea kwa utamaduni wetu na ni kwa nadharia mbalimbali. Tunapata mvua kidogo, ukiweka mbolea ile itabaki pale pale juu na mimea itakauka. Kwa hiyo sisi hatutumii hii mbolea ya kemikali na tunatumia mbolea ya chumvi chumvi. Sasa kikubwa tunachofanya tunalima mazao yanayostahimili ukame; mtama mfupi umefanyiwa *research* unastahimili sana Dodoma unaweza ukachukua miezi miwili tayari ukawa umeiva, lakini mbegu hatupati. Mwaka jana nimefanya kampeni kubwa kwenye jimbo langu kuhamasisha wakulima walime mtama mfupi na tukawaorodhesha wakulima ili kila mmoja apate kiasi cha mbegu anachotaka kulima.

Mheshimiwa Spika, pamoja na jitihada hiyo, hatukupata mbegu. Tumefuatilia kwa wakala wa mbegu na jibu tulilopata kwamba mbegu hamna. Kwa hiyo maeneo mengine wanavyokuwa na utaratibu wa mbolea za bei nafuu za ruzuku kwetu sisi hakuna. Nataka niseme Serikali ilichukue kwa dhati kuona namna gani ya kuinua suala la kilimo katika mkoa wetu. Nachelea kusema tumetelekezwa, kama tumeachwa vile, tunajilimia tu. Kwa Mkoa wa Dodoma, naomba Serikali na hata bajeti inayokuja ya kilimo ioneshe nia thabiti kabisa ya kwenda kuinua kiwango cha kilimo katika mkoa wetu. Fedha inayokuja kwenye bajeti ni fedha ya uendeshaji na uratibu, lakini katika pembejeo bado hatupati kabisa katika kuinua kilimo chetu.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine Dodoma sisi tunastawisha zabibu na zabibu imekuwa ni mkombozi. Bahati

mbaya zao hili limekosa usimamizi na nataka kujenga hoja hapa kwamba kuwe na Bodi ya Zao la Zabibu. Zao la zabibu liko sasa chini ya Wizara ya Kilimo, lakini Wizara ya Kilimo ina mambo mengi, zao hili limekuwa halihudumiwi vizuri. Tuunde Bodi ya Kilimo na hili Bunge wengi wamepita wanaomba Bodi ya Kilimo. Tuna Bodi nyingi za Kahawa, za Chai, kwa nini Bodi ya Zabibu imekuwa ni mtihani mkubwa? Ikishaundwa Bodi itafanya mambo yake, itafuatilia yenyewe kilimo lakini vile vile hata kufuatilia masoko.

Mheshimiwa Spika, kwenye suala la mchuzi wa zabibu, Serikali imekuwa ikitoa fedha kwamba iwezeshe wanunuzi, lakini kuna *curtail* kwenye suala hili. Wako wanunuzi wanapewa fedha wanazunguka zunguka kununuanunua lakini hawanunui ile zabibu kwa wakulima na hata ule mchuzi kwa wakulima hawauchukui, bali ipo namna wanayoifanya. Wanachofanya wanaagiza *concentrate* ya unga hapa nchini lakini wanasema tumenunua. Ukiwauliza wanasema Vumi tumenunua kwa wakulima kiasi hiki, Chibelela kiasi, Mpunguzi kiasi hiki. Nenda kaulize mkulima aliowauzia, hakuna. Serikali bado inaagiza, inaruhusu *concentrate* iingie hapa kwetu nchini. Sasa zabibu itakua? Kwa hiyo suala hili ninachotaka kusema *curtail* ipo kwenye suala la zabibu na tunaomba Bodi iundwe tuwe na Bodi ya Zao la Zabibu. Nataka niwahakikishie kwamba kilimo cha zabibu kitainuka na biashara ya zabibu itasonga mbele.

Mheshimiwa Spika, suala lingine mwaka jana nilichangia kuhusu kukua kwa kutokutabirika kwa bei ya *cement* hapa nchini. Wote tunaweza tukachukua historia, sukari imetusumbua sana nchini, lakini kwa sasa uhakika wa bei ya sukari kutokupanda tumeshadhibiti. Kwenye *cement* bado hivyo hivyo kwamba *cement* haina uhakika na shida iliyopo ni kwamba ipo kampuni kubwa ina utaratibu wa kufunga kiwanda kwa ajili ya matengenezo na huwa inafunga mwezi wa 11 na bei ndivyo inavyopanda. Suala hili hatuwezi

kuruhusu nchi yetu ikaenda namna hiyo. Kwa hiyo tuna uhakika na mwakani tena *cement* itapanda.

Mheshimiwa Spika, nimepitia kwenye magazeti wiki hii, ipo tatizo kwamba Kampuni ya *Twiga Cement* inataka kufanya *acquisition* ya *Tanga Cement* na bahati mbaya wamepelekana mahakamani, lakini na chombo chetu cha Serikali nacho kiko humo, *The Fair Competition.* Sasa ninachotaka kukiona katika jambo lile, nimesoma sana makala zile na nimeelewa kwamba anapokuja kuchukua *share* kubwa, lipo tatizo hili tunaloweza kulipata kama nilivyoelezea la mwezi wa 11. Kwa hiyo hapa tunakuwa na mzalishaji ambaye anaweza kuamua na kupanga bei yeye mwenyewe.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo ujenzi wa Taifa letu wananchi kupata nyumba bora, hawawezi wakajenga makazi bora kama bado *cement* ni bei ya anasa. Kwa hiyo jambo hili naomba liangaliwe na suala hili la sakata kati ya *Tanga Cement* na *Twiga Cement* basi tupate maelezo watu waweze kulielewa.

**MHE. ELIBARIKI I. KINGU:** Mheshimiwa Spika, Taarifa.

**SPIKA:** Inatokea wapi?

**MHE. ELIBARIKI I. KINGU:** Ni mimi hapa Kingu, niko hapa.

**SPIKA:** Mheshimiwa Kenneth Nollo kuna taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Elibariki Kingu.

**MHE. ELIBARIKI I. KINGU:** Mheshimiwa Spika, napenda kumpa msemaji taarifa kwamba kwa mujibu wa sheria ya *Fair Competition Act* sikumbuki ni kipengele gani lakini kimezuia *monopoly* ya kampuni moja kuwa na *market share* ya zaidi ya 36. *Merger* anayoizungumza ya kiwanda hiki kinachotaka kumnunua mwenzake inakwenda kuzidi sheria tuliyoipitisha ya

Bunge ya *market monopoly.* Kwa hiyo kwa namna yoyote lazima Watanzania watakwenda kuumizwa kwenye bei ya *cement.*

**SPIKA:** Mheshimiwa Kenneth Nollo unaipokea taarifa hiyo?

**MHE. KENNETH E. NOLLO:** Mheshimiwa Spika, naipokea taarifa hii na nimepewa maelezo mazuri ya kisomi zaidi, nilikuwa naongea *layman* kwa ujumla lakini nashukuru kwa taarifa ya Mheshimiwa Kingu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwisho nataka niipongeze sana Serikali katika ujenzi wa majengo kwa ajili ya kutolea huduma za afya na elimu. Majengo yale tumejenga bahati mbaya kwenye elimu walimu bado hatujapeleka. Zipo shule shikizi tayari tumejenga. Ukienda kule sehemu inaitwa Mangwe Mnarani unaenda Ipole kule Igugule, unaenda Iyumba kule Nondwa majengo yapo lakini hamna Walimu. Hivyo hivyo zahanati nyingi zimejengwa katika vijiji kwenye jimbo langu lakini hakuna wahudumu wa afya. Kwa hiyo, naomba Serikali wananchi wana shauku kubwa ya kupata afya na kama ni majengo wameyaangalia kwa miaka miwili, wameshangaa vya kutosha sasa wanahitaji kupata huduma ya afya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwisho kabisa nataka niipongeze kwa dhati Ofisi ya Waziri Mkuu na Wizara ya Kilimo. Wamefanya kazi nzuri katika kutuletea mahindi ya bei nafuu. Kwa Wilaya ya Bahi nimekuwa mnufaika mkubwa sana. Kila kata imeweza kupata mahindi yale ya bei nafuu na nataka niseme utaratibu huu kwa kweli sisi ambao nimesema hali ya kilimo bado haijaimarika na mwakani uweze kuendelea, kama nilivyosema mwaka huu hatujapata mvua za kutosha, kwa hiyo Serikali iendelee na utaratibu wa kuweza kutupatia mahindi ya bei nafuu, lakini kikubwa zaidi iweze kuangalia

namna gani inaweza kusaidia mkoa wetu katika kuinua kilimo.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Jackson Gideon Kiswaga atafuatiwa na Mheshimiwa Moshi Seleman Kakoso na Mheshimiwa Daimu Iddi Mpakate ajiandae.

**MHE. JACKSON G. KISWAGA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia katika hoja hii muhimu iliyoko mezani na nianze kwa kuunga mkono hoja ya Waziri Mkuu kwenye Bajeti ya Waziri Mkuu.

Kwanza nimshukuru pia kwa uwasilishaji mpana ambao umegusa sekta mbalimbali lakini pia namshukuru sana Rais kwa kazi kubwa anayoifanya kwa kutuletea miradi mingi sana siwezi kueleza mmoja mmoja. Nilikuwa namwambia mtu mmoja wakati fulani nilikuwa nampongeza rais, akasema unampongeza Rais kwa nini mbona anafanya kazi yake? Nikasema wewe hujui kinachoendelea acha sisi tumpongeze kwa sababu tunajua aliyotufanyia kwenye majimbo. Kwa hiyo aendelee kupokea hizi pongezi, sisi tunampongeza kwa sababu tunamtia shime ili aendelee kupata moyo wa kuendelea kufanya kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kikubwa ni hiyo *fairness* yake ya kuhakikisha kwamba kila jimbo linapata mgao sawia. Zamani haikuwa hivyo unakuta mtu mwenye nguvu ndiyo anapata *share* kubwa zaidi, kwa hiyo ndiyo maana tunampongeza.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo kwanza nianze pia kuishukuru Wizara ya Kilimo kwa kutuletea mahindi hata Jimbo langu lilikuwa limeathirika lakini baadhi ya maeneo tumeshapokea hayo mahindi, rai yangu ni kwamba Watendaji wetu wa Serikali waendelee kuwa waaminifu kwa sababu inaonekana sehemu nyingine watu wanaandikisha

majina ya watu ambao hawana uhitaji, wakati wao ndiyo wanaochukua hayo mazao kwenda kujinufaisha, kwa hiyo niombe vyombo vinavyohusika Wakuu wa Wilaya na Maafisa Tarafa kwenye maeneo yote siyo tu Jimbo langu na sehemu zingine zote hili jambo walifatilie kwa karibu.

Mheshimiwa Spika, nia ya Serikali ni kuhakikisha kwamba watanzania wenye njaa wanapata chakula siyo watu kwenda kujitajirisha, hii tuwaonye pia hao wanaofanya hivyo kwa sababu watafungwa, Serikali haipo hapa kwa ajili ya kuchezacheza.

Mheshimiwa Spika, kwenye kilimo ningependa kuchangia zaidi, sasa hivi hali ya hewa inaendelea kubadilika sana kwa sababu ya haya mabadiliko ya tabianchi, hapa Tanzania tumezoea sana kulima haya mazao hasa mahindi kama ndiyo zao letu kuu, sasa tuone wenzetu wa kilimo waanze kufanya utafiti hasa kwenye zao la muhogo kama ndiyo kiwe chakula ambacho kinatoa zaidi, tunapozungumzia nafaka.

Mheshimiwa Spika, miaka ya nyuma huko hata kule kwetu Iringa tulikuwa tunalima sana mtama, lakini miaka ya hivi karibuni huu mtama umepotea. Kwa hiyo, wenzetu wa kilimo sasa watusaidie kwanza kutoa elimu pia kufanya utafiti zaidi kama tunaweza tukapata mtama ambao ni mwepesi zaidi wa miezi miwili pia utawanyike katika maeneo mbalimbali ya nchi kwa sababu tunakokwenda hali itakuwa mbaya zaidi.

Mheshimiwa Spika, hapo hapo kwenye kilimo kwenye vyuo vyetu vya *VETA* kuwe kuna mitaala mahsusi ambayo inaelezea namna gani tunawafundisha vijana kulima kwa sababu ukiangalia kadri tunavyoendelea ardhi inazidi kupungua, kwa hiyo, uhitaji wa kulima kwa tija unakuwa mkubwa zaidi, mtu atumie eneo dogo lakini azalishe kwa tija zaidi. Sasa hii itawezekana tu kama tutajikita katika kutoa

masomo yanayohusu kilimo lakini na zile shule zetu za kilimo za zamani ziweze kurudi ili tuanze kuwaandaa vijana kutoka huko, hiyo itasaidia sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwenye suala la mbolea ya ruzuku pia tunaishukuru sana Serikali kwa kutoa mbolea za ruzuku lakini tuwaombe wenzetu wa Wizara ya Kilimo waanze maandalizi mapema. Mwaka huu sehemu nyingi za Tanzania hata katika Jimbo langu la Kalenga wananchi wamechelewa sana kupata mbolea, pamoja na kuwa mvua zimekuwa pungufu lakini pia mbolea zenyewe zilichelewa sana. Kwa hiyo tunawaomba wenzetu wa kilimo maandalizi yaanze mapema ili mbolea zipatikane mapema, pale ambapo mvua zipo basi Watanzania waweze kunufaika na hii ruzuku ambayo Mheshimiwa Rais amewapa Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninapenda kuzungumzia eneo lingine la kukuza uchumi hasa upande wa bandari, kwamba bandari tunajua ni lango kuu la uchumi, naipongeza Serikali katika mipango yake ya kutaka kuanza kujenga Bandari ya Bagamoyo. Tanzania inaweza ikawa *hub* ya uchumi unaotokana na bandari katika eneo la Maziwa Makuu pamoja na Afrika Mashariki kwa ujumla wake pengine hata na *SADC,* kwa hiyo jambo hili liende haraka.

Mheshimiwa Spika, ombi langu kwa Serikali kwamba tulishaanza na tulishasikia kwamba kulikuwa kuna mpango wa kutengeneza mfumo wa kusomana kati ya *TRA* pamoja na shughuli zinazofanywa bandarini. Miaka miwili iliyopita tuliambiwa kwamba wanaanza majaribio, miaka miwili imepita hakuna kinachoendelea. Hii inaonesha kwamba nia ya bandari na nia ya *TRA* sioni kama iko vizuri! Kama wote wangekuwa na nia moja hii ingekuwa imeshakwisha na tunaweza kama Serikali tukapata fedha nyingi sana mambo yetu yanapopita kwenye mfumo. Kwa hiyo ninawaomba wenzetu *TRA,* Bandari mharakishe hili jambo la mifumo

kusomana ili nchi iweze kunufaika na kazi kubwa. Muoneshe nia vinginevyo mnatutia mashaka kwamba hizi fedha zinazovuja wenzetu mnanufaika nazo. Kwa hiyo, hilo naomba muweze kuliangalia kwa ukaribu zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo ninapenda kuzungumza ni kwamba tunavyoelekea bajeti yetu hii mpya, kweli shule zetu za zamani zimechakaa sana, ninaiomba Serikali kwamba katika bajeti zake sasa tuanze kuziangalia shule zetu kongwe, hasa za shule za msingi nilishazungumza tena nalirudia tena, shule hizi ambazo zimejengwa miaka ya 1970, 1980 zimeshaanza kuchoka. Tunavyoweka nguvu katika kujenga shule mpya basi tuhakikishe kwamba ukarabati wa shule za zamani pia tunaendelea kuziboresha. Hilo nalo ni jambo jema Serikali ione namna gani tunafanya.

Mheshimiwa Spika, pia umaliziaji wa yale maboma katika maeneo ya mashule, katika maeneo ya hospitali kwa maana ya zahanati na vituo vya afya, ambapo tayari wananchi walishaanza. Vipo vituo vya afya ambapo vilijengwa siku nyingi unakuta vina wodi moja ya akina mama lakini hata sasa hivi wakina baba wanaumwa sana. Kwa hiyo, tungependa pia Serikali ione umuhimu katika vile vituo vya afya vya zamani kwangu Kalenga na nchi nzima kuanza kujenga pia wodi za wanaume kwa sababu uhitaji upo na tunavyokwenda huko tunakuta wananchi wanatuuliza.

Mheshimiwa Spika, suala lingine ambalo ninapenda kuzungumza ni suala la upimaji wa viwanja. Kwa mfano, Serikali inajitahidi sana kutoa huduma kwa wananchi lakini kwa sababu ya ujenzi holela, mimi niko katika kijiji fulani, nimekaa hapa leo ninaamua naona kuna shamba kilometa 10 nakwenda nafyeka najenga kesho namleta Binamu, kesho namleta na Mjomba baadaye unashangaa eneo lile lina watu watano, lina watu kumi, tayari tunaanza kuisumbua Serikali, hamtuletei maji, hamtuletei shule. Sasa inaonekana kwamba Serikali haifanyi kazi lakini kwa sababu tumeshindwa

kudhibiti ni namna gani tunaweka matumizi bora ya ardhi hasa katika eneo la makazi.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo hilo Serikali iwekee mkazo mkubwa ili tusiwe na hizi changamoto tunakwenda kukagua miradi ya maji unaambiwa bwana mahali fulani sisi hatujaletewa maji, kwa nini kuna kitongoji fulani tumeanzisha. Kwa hiyo Serikali kwenye hiyo mipango miji iende pengine kwa haraka zaidi itaweza kuisaidia nchi ili mipango ikae vizuri zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, eneo lingine ni eneo la umeme. Serikali imefanya vizuri tunaishukuru, katika Jimbo langu la Kalenga nilibakiwa na vijiji vitatu sasa hivi wanavimalizia tunashukuru Serikali. Vipo vitongoji vingi sana ambavyo ni vikubwa katika bajeti hii Serikali sasa ione namna gani tutakwenda kupeleka kwa kasi umeme katika vitongoji ambavyo tayari maombi hayo kwenye TANESCO na *REA*. *REA* sasa kwa kuwa wanakwenda kumaliza vijiji, nguvu zaidi waelekeze kwenye vitongoji ili nako tuweze kukamilisha mambo hayo.

Mheshimiwa Spika, naona muda wangu umeisha ninashukuru sana kwa kunipa nafasi ahsante sana, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Moshi Selemani Kakoso atafuatiwa na Mheshimiwa Daimu Iddi Mpakate na Mheshimiwa Benaya Liuka Kapinga ajiandae.

**MHE. MOSHI S. KAKOSO:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuwa mchangiaji kwenye hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Spika, nami nichukue nafasi hii kumshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa jitihada kubwa ambazo anazifanya za kuleta fedha za maendeleo kwenye maeneo

yote ya nchi yetu. Miongoni mwa walionufaika ni sehemu ya Mkoa wa Katavi, Wilaya ya Tanganyika tumepata fedha nyingi za maendeleo, kwenye sekta ya elimu, maji, miundombinu na kwenye afya tumeletewa fedha nyingi za maendeleo ambazo zinaonesha kabisa jitihada za Serikali zilizofanywa na Mheshimiwa Rais.

Mheshimiwa Spika, ninawapongeza Watendaji wa Serikali wakisimamiwa na Mawaziri kwa jitihada zao ambazo wamezifanya kusimamia miradi ile ya maendeleo.

Mheshimiwa Spika, nizungumzie mradi wa bandari. Serikali imewekeza mradi mkubwa wa bandari eneo la Kalema ambao una thamani ya Shilingi Bilioni 48. Mradi huu ni mradi mkubwa na una manufaa kwa nchi yetu, kitu ambacho tunaiombe Serikali ni kuhakikisha sasa mradi huu ili uweze kufanya kazi ni lazima Serikali ijenge barabara yenye kilometa 110 kutoka Kagwira kwenda Karema ili ile bandari iweze kufanya kazi kuliko ilivyo sasa.

Mheshimiwa Spika, wenzetu wa DRC Congo wanaitumia fursa hii ya kupatikana kwa bandari ili waweze kuleta mizigo ipitie Bandari ya Karema na hatimaye kufika kwenye Bandari ya Dar es Salaam. Ninaiomba Serikali iharakishe mchakato wa ujenzi wa barabara hiyo ili iweze kusaidia shughuli za kiuchumi kwenye maeneo hayo, vilevile kuifanya Bandari ya Dar es Salaam kuondoa msongamano uliopo pale eneo la Tunduma pindi utakapokuwa umekamilika mradi huu wa barabara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, eneo lingine ambalo tunaishukuru Serikali ni miradi ya umeme wa *REA* ambao mimi kwenye Jimbo langu tuna vijiji 26, kwa bahati nzuri Serikali ilitoa fedha na ikapata Mkandarasi lakini kumekuwa na changamoto kubwa sana Mkandarasi aliyepewa dhamana ya kupeleka umeme vijijini kwa Mkoa wa Katavi ameshindwa kutekeleza mradi ule kwa wakati. Ninaiomba Serikali Wakandarasi

wanapopewa kazi wasimamiwe vizuri ili waweze kukamilisha miradi ambayo wameiweka kwa ajili ya kuwafikia wananchi.

Mheshimiwa Spika, ninavyo vijiji 26 ambavyo alipewa huyu mkandarasi lakini mpaka sasa bado hajakamilisha na kila mwaka wanamwongezea muda ili aweze kukamlisha. Ninaomba kwenye eneo hilo Serikali ilifanyie kazi ili mradi huu uweze kukamilika.

Mheshimiwa Spika, kumekuwa na changamoto kubwa sana mkandarasi aliyepewa dhamana ya kupeleka umeme vijijini kwa Mkoa wa Katavi ameshindwa kutekeleza mradi ule kwa wakati. Niombe Serikali wakandarasi wanapopewa kazi wasimamiwe vizuri ili waweze kukamilisha miradi ambayo wameiweka kwa ajili ya kuwafikia wananchi. Nina vijiji 26 ambavyo alipewa huyu mkandarasi lakini mpaka sasa bado hajakamilisha na kila mwaka wanamwongezea muda ili aweze kukamilisha. Ninaomba kwenye eneo hilo Serikali ilifanyie kazi ili mradi huu uweze kukamilika.

Mheshimiwa Spika, eneo jingine ni miradi ya maji. Tunaishukuru Serikali Halmashauri yangu imepata Shilingi Bilioni 8.9 kwa ajili ya kutekeleza miradi mbalimbali na Serikali imejitahidi kupeleka miradi, iko iliyokamilika na mingine bado ambayo haijakamilika ukiwemo mradi wa eneo la Mishamo wenye thamani ya shilingi bilioni1.3. Shida kubwa ambayo ipo katika eneo hilo ni Mkandarasi aliyepewa hana uwezo wa kwenda kufanya kazi na asilimia kubwa anatafuta fedha apewe fedha kabla hajafanya kazi wala kwenda kwenye eneo la *site*.

Mheshimiwa Spika, ninaomba Serikali iweze kutoa Mkandarasi mwingine kuliko yule ambaye walimpa na hana uwezo. Mkandarasi huyo anaitwa Hamwa, kazi anayoifanya ni kwenda kufanya *lobbying* na kutisha watendaji wa Serikali waidhinishe kumpa fedha wakati uwezo wa kufanya kazi haupo.

Mheshimiwa Spika, ipo miradi mingine ya maji katika Vijiji vya Kapalamsenga wenye thamani ya Shilingi Bilioni 1.3 inaenda vizuri lakini tunaomba Mkandarasi aliyepewa kazi hiyo aweze kuisimamia ikamilike kwa wakati. Kubwa zaidi ambalo tunalihitaji wananchi wa Wilaya ya Tanganyika na Mkoa wa Katavi kwa ujumla kwenye mradi wa maji tuliishauri Serikali kuhakikisha mradi ambao unaweza ukabeba matumaini ya wananchi wa Wilaya ya Tanganyika na Mkoa wa Katavi ni mradi ule mkubwa wa maji kuyatoa Ziwa Tanganyika kuyapeleka Makao Makuu ya Mkoa wa Katavi.

Mheshimiwa Spika, najua jitihada za Serikali zimefanywa hatua za awali, tunaomba kwenye bajeti hii waangalie umuhimu wa kuanza ujenzi wa mradi huu mkubwa wa maji ambao utatatua kero ya maji Mkoa wa Katavi.

Mheshimiwa Spika, sehemu nyingine ambayo tulikuwa tunaishauri Serikali ni ujenzi wa meli wa Ziwa Tanganyika. Tumejenga Bandari lakini bado vitendeakazi havipo. Ili bandari zilizopo Mkoa wa Kigoma, Katavi na Mkoa wa Rukwa ziweze kufanya kazi tunahitaji kuwa na meli. Meli ambazo zitafanya kazi kwenye Ziwa Tanganyika na ni kitendo cha aibu kwamba katikati ya nchi zilizozunguka Ziwa Tanganyika eneo la nchi yetu tu ndiyo ambayo haina vyombo vya usafiri. Niombe Serikali iweze kufanya mchakato wa haraka ule ambao wameuanzisha wa kuanza kujenga meli kwenye Ziwa Tanganyika tupate meli za mizigo na abiria kwa ajili ya kuwasaidia wananchi. Bila kufanya hivi hata uwekezaji tuliouwekeza kule utakuwa ni sawa na hakuna. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, eneo hili ni muhimu kiuchumi na wenzetu nchi za Burundi, Congo wanaitumia kama fursa na sisi hii fursa tuitumie ambayo itatusaidia sisi na kwa nchi kwa ujumla. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sehemu nyingine ya mchango wangu ni kwenye eneo la kilimo. Tunaishukuru Serikali ilileta

mbolea zenye ruzuku ya Serikali kwenye eneo hili. Tunaipongeza sana, lipo jambo ambalo tulikuwa tunaomba na kuishauri Serikali iweze kulifanyia mchakato kwa kiwango kikubwa. Mbolea za ruzuku za Serikali zilizotolewa zimebagua baadhi ya maeneo hawakupewa kwa ajili ya kuwasaidia wakulima wetu. Wakulima ambao wanatoka Mikoa inayozalisha zao la tumbaku hawajanufaika na ruzuku iliyotolewa na Serikali. Ninaomba kwenye mchakato huu na wao waangaliwe kwa sababu na wao ni sehemu ambayo wananufaika na wana mchango mkubwa kwenye Pato la Taifa.

Mheshimiwa Spika, mfuko mmoja unauzwa kati ya shilingi 170,000 na hawa wakulima faida yao inakuwa ndogo sana kwa sababu gharama ya uzalishaji inakuwa kubwa sana. Ninaomba Serikali ilichukue hili na ilifanyie kazi ili iwasaidie wananchi kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, sehemu ya pili kwenye eneo la kilimo juu ya mbolea hizo, tunaomba utaratibu ambao ulifanyika mwaka huu mwakani ufanyiwe maboresho kwa kiwango kikubwa ili iwafikie walaji waliowengi kuliko ilivyokuwa sasa walionufaika ni wachache na pengine unawanufaisha watu wengine ambao ni wafanyabiashara *middleman* ambao wanatumia hizo huduma zilizotolewa na Serikali kuliko wale walengwa ambao ni wakulima halisi.

Mheshimiwa Spika, niendelee kuishukuru Serikali kwenye miradi ya afya. Tumeletewa miradi mingi ya afya kwenye Mkoa wa Katavi lakini tatizo kubwa tulilonalo ni watumishi ambao wanahitaji kutoa huduma za afya. Kwenye zahanati, vituo vya afya, hospitali ya Wilaya bado uhitaji mkubwa wa watumishi ni mkubwa kwenye maeneo haya. Mimi binafsi tu kwenye Wilaya yangu nina vituo vya afya ambavyo vimejengwa zaidi ya vitano lakini watumishi tulionao ni wachache, tuna hospitali ya Wilaya ambayo inahitaji huduma kutolewa kwa wananchi, bahati mbaya sana hata

vitendeakazi havipo! Kwa hiyo, tunaomba uwekezaji uliowekezwa na Serikali kwenye eneo hili ni vizuri sasa na ni muhimu wakatoa fedha kwa ajili ya kutoa ajira kwa wananchi.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Daimu Iddi Mpakate atafuatiwa na Mheshimiwa Benaya Liuka Kapinga.

**MHE. DAIMU I. MPAKATE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi mchana huu ili kuchangia hoja ya hotuba ya Waziri Mkuu. Kwanza naunga mkono kwa asilimia 100.

Pili, naomba nimshukuru Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kazi kubwa aliyoifanya kwenye maeneo ya Jimbo la Tunduru Kusini na Tunduru kwa ujumla kwa miradi ya afya, elimu pamoja na miundombinu ambayo imerahisisha maisha ya Watanzania kwa maana ya wakazi wa Tunduru Kusini.

Mheshimiwa Spika, pamoja na shukrani hizo nitaongea mambo matatu. Jambo la kwanza ni suala la kilimo. Jambo la pili suala la elimu na jambo la tatu ni miundombinu ya barabara.

Mheshimiwa Spika, kwanza nimshukuru Rais wetu kwa kutupatia mahindi ya bei nafuu kwa Wilaya ya Tunduru. Baada ya maombi yetu kupelekwa kwenye *RCC* tunashukuru tulipata mahindi na yamesambazwa kwa kiasi kikubwa katika eneo letu ila tunaomba nafasi hii kwa safari ijayo uweke utaratibu tofauti ulivyofanywa sasa.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa katiba Ibara ya 35 inasema bayana kwamba shughuli zote za utendaji wa Serikali ya Jamuhuri ya Muungano zitatekelezwa na Utumishi wa Serikali kwa niaba ya Rais, na kwamba utaratibu wa masharti ya kutoa fedha za Seriakli, pengine kutoka hata Mfuko Mkuu wa Hazina unabainishwa katika Ibara ya 136, Ibara ya 137 na hata Ibara ya 40 inabainisha pale ambapo Rais ametajwa kwamba anaweza kushughulikia mambo haya ya fedha lakini ni Rais au Waziri aliyemteua.

Mheshimiwa Spika, sasa tunaposema kwamba malipo haya yanapaswa au yanapitiwa na Rais ili yaweze kulipwa, ili hali Rais mwenyewe juzi amesimama na kutoa malalamiko yake jinsi ambavyo hakuridhishwa baadhi ya wakandarasi wanapokuwa wanarundikiwa, wanacheleweshwa kulipwa na kusababisha riba zaidi ya shilingi bilioni 400.

Mheshimiwa Spika, sasa ninajiuliza kama ingekuwa Rais ndio anaidhinisha malipo haya na sio wale ambao amewakasimu madaraka kwa mujibu wa katiba, leo uzembe unapotokea na ufisadi unaotokea kwa tafsiri ya maelezo ya Waziri, ninavyoyaona maana yake yote yana idhini ya Rais jambo ambalo si kweli hata kidogo, vinginevyo ufisadi huu, tusingekuwa tunawa-*attack* wale ambao ni maafisa masuhuli na mlipaji mkuu wa Serikali ambaye tunamsimamia na Waziri mwenye dhamana ya fedha.

Mheshimiwa Spika, je, ni sahihi kutumika kwa jina la Rais katika mazingira hayo kama ambavyo kanuni ya 71(9) inavyoeleza. Nilikuwa najaribu kuliona jambo hili linapeleka taswira ambayo sio njema kwamba Rais lazima aidhinishe fedha hizo ndipo ziweze kulipwa katika kipindi hiki ambacho wimbi la ufisadi limeweza kubainishwa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali.

Mheshimiwa Spika, nilikuwa naomba mwongozo wako kama ni sahihi kutumika kwa maneno aliyoyatumia Waziri

katika eneo hilo. Wakati Wabunge wanaeleza masikitiko ya baadhi ya malipo ambayo hayajakaa vizuri, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri nimeombwa Mwongozo naona umesimama.

Waheshimiwa Wabunge, kwanza tumefika mwisho wa kipindi chetu cha asubuhi ambapo baadhi yenu mmepata nafasi ya kuchangia. Kabla sijasitisha shughuli za Bunge amesimama hapa Mheshimiwa Ole-Sendeka akiomba muongozo wa Spika kwa mujibu wa kanuni ya 76 ambayo inampa fursa Mbunge kuweza kutaka kufahamu jambo ambalo limetokea hapa Bungeni mapema kama linaruhusiwa au haliruhusiwi, ametoa maelezo pia akatupeleka kwenye Kanuni ya 71 ambayo kwa maelezo yake yeye lengo lake la kutumia kanuni ya 76 ni kutaka kujua kama kanuni ya 71(9), kifungu kidogo cha 9 hatuna, lakini ukisoma kwa sababu anaeleza kuhusu matumizi ya jina la Rais ni kanuni ya 71(1)(g).

Sasa wakati akitoa maelezo Mheshimiwa Waziri, akimpa taarifa Mheshimiwa Esther Matiko, ambaye alikuwa anazungumzia pesa ambazo zimeongezwa ama tuseme zimeongezeka kwenye hati ya madai ambayo ilipaswa kudai milioni 37 za kimarekani ikadai milioni 86. Muktadha ulikuwa ni huo, sasa wakati wa Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Waziri wa Fedha akitoa tarifa alieleza kwa sehemu ya hayo aliyoeleza, alieleza kwamba pesa hiyo, nilivyomuelewa na nitampa nafasi hapa nilivyomuelewa ni kwamba pesa hiyo haijalipwa lakini hata yale madai ni kwamba Rais ameyafahamu kwa sababu yamepelekwa na upande wa yeyote aliyepokea hizo taarifa akampelekea Rais.

Sasa muktadha wa taarifa ya Mheshimiwa Mwigulu na naweka muktadha ili asilamike hapa kutumia muda mrefu kama nitakuwa nimemuelewa ama sijamuelewa. Na kama

sijamuelewa basi mwongozo utatolewa baadae ikiwa atatoa maelezo tofauti na haya.

Sasa muktadha wake ni kwamba, hiyo taarifa ambayo yeye alikuwa anaitoa ni kwamba Mheshimiwa Rais hakuna malipo ya yanayofanyika bila yeye kufahamu na ndio maana hata hili lilifika kwake kwa sababu madai yanayodaiwa lazima yeye ndio aidhinishe. Sasa hoja iliyojitokeza ni kwamba yeye ndiye anayeidhinisha sasa ule mwongozo uliiomba pale Mheshimiwa Waziri ili utakapopewa nafasi ya kuzungumza.

Mwongozo unaoombwa ni hivi, je, Rais ndiye anayeidhinisha malipo kama ambavyo ulitoa maelezo na ndio maana nitakupa nafasi ili ufafanue ni malipo ya aina gani Rais anahusika na yapi hausiki. Ili kumtenga Rais na haya ambayo yanatokea kwamba kuna mahali pengine fedha zimelipwa bila utaratibu, ama kuna mahali fedha zimeliwa kwa sababu kama zimeliwa na yeye ndiye aliyeidhinisha maana yake anafahamu kwamba zimeenda kuliwa. *(Makofi)*

Kwa hiyo, nitakupa nafasi ili ulitolee ufafanuzi kwa mahali hapo, swali la Mheshimiwa, Mheshimiwa, muongozo alioniomba Mheshimiwa Ole-Sendeka uko hapo kwamba je, malipo Mheshimiwa Rais ukiacha yale yaliyotajwa ya Mfuko Mkuu wa Hazina na ule utaratibu wa pesa kutoka, haya malipo mengine yeye Rais hapo umemuingizaje kwa nini kwa sababu kanuni zetu zinasema jina la Rais lisitumike kwa namna hiyo ndio maana yeye kasimama, kama isingekuwa hivyo angekuwa ameliacha lilivyo. *(Makofi)*

Kwa hivyo, nitakupa utoe huo ufafanuzi na kama kuna sababu basi pengine nitasema mwongozo utatolewa baadae ili nikazipitie vizuri, nikapitie vizuri ule mchango wako, pengine sikuelewa vizuri ama sikusikia vizuri. Sasa nakupa nafasi uafafanue hiyo sehemu ili niweze kumpa mwongozo vizuri Mhehsimiwa Ole-Sendeka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii nifafanue kwa mifano miwili. Iko namna hii Serikalini kuna mlipaji mkuu wa Serikali amabye ni Katibu Mkuu wa Wizara ya Fedha. Lakini ili ifike kwenye ulipaji wa Katibu Mkuu ambaye ndio mlipaji mkuu wa Serikali, Katibu Mkuu haamki tu anapokea nanii za Wizara za kisekta halafu nanazipeleka kwenye kulipa.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, kuna utaratibu wa kuidhinisha matumizi, sasa matumizi hilo ni *bracket* kubwa ambayo ni kama tunavyoleta bajeti hapa. Waziri wa Fedha huleti tu bajeti, *tax measures*, hauzileti tu *tax measures* hivyo vitu vyote vikubwa vinapata idhini ndio vinaenda kwenye ngazi ya utekelezaji.

Mheshimiwa Spika, sasa kwa nini tunasema kuna hatua za uwajibikaji ni wale wanaolipa, hatua za uwajibikaji zinaenda kwa wale wanaolipa kwa sababu kwa mfano, ameongelea Mheshimiwa Ole-Sendeka kwamba kuna malalamiko ya hii imechelewa hii haijachelewa. Idhini za matumizi ya Serikali kwa mwezi husika yanakuwa yamepata idhini kabla ya tarehe 17 katika mwezi husika *from there* ni matumizi kwenda kwenye mafungu yanayohusika ambako mlipaji mkuu anayetoa idhini ya haya matumizi anakuwa Katibu Mkuu wa Sekta.

Mheshimiwa Spika, sasa kwenye ngazi ya jambo hili mahsusi ambalo nilikuwa namuelezea Mheshimiwa Esther Matiko yamekuja mpaka kwenye wizara yetu ni jambo kubwa, jambo kubwa kama hilo, kama ni la kisheria lazima tupate idhini ya Mwanasheria Mkuu kwamba halina mzozo. Lakini jambo kubwa kama hilo limeongezeka lazima tumtaarifu mwenye nchi, hatuwezi tukashughulika na jambo kubwa hivyo halafu bila kumuhusisha mwenye nchi.

Mheshimiwa Spika, kuna Wizara za Kisekta ambazo, kuna Wizara amabazo ufanyaji kazi wake kwa mfano Waziri wa Nchi TAMISEMI mwenye Wizara ni Rais, lakini jambo la Wizara ya Fedha, fedha yenyewe ni jambo kubwa hatuwezi tukashughulika na jambo kubwa la aina hiyo bila kumuhusisha mwenye nchi, kwamba tumepokea *invoice* ni kubwa sababu za msingi hatujazipata tumewarudisha walifanyie kazi lakini na yeye lazima apate picha. Na jambo lile pia halikuwemo kwenye *frame* ya matumizi ya mwezi huu, halikuwa limepata ridhaa ya *frame* kwenye *frame* ya matumizi ya mwezu huu.

Mheshimiwa Spika, sasa utaratibu wa udhibiti ambao umezoeleka Serikalini tangu niko Naibu Waziri, tangu niko Naibu Waziri sio sasa hivi, tangu niko Naibu Waziri miaka karibu 10 iliyopita, utaratibu mkishafanya *ceiling* katika mwezi, *ceiling* katika mwezi na hiyo ndio *practice* ya Serikali, mkishafanya *ceiling* ifikapo tarehe 10 lazima *ceiling* hiyo iwe imefika mezani kwa Mheshimiwa Rais. Awamu ya Nne yote ilikuwa hivyo, Awamu wa Tano yote ilikuwa hivyo na sasa iko hivyo. Halafu kabla ya tarehe 17, lazima hiyo *ceiling* iwe imeshapata *go ahead* ya kiongozi na ikishapata *go ahead* hiyo *ceiling* ndio tunaenda kwenye taratibu za kimalipo ambazo mlipaji mkuu wa Serikali ni Katibu Mkuu wa Hazina, kwa hiyo Rais sio mlipaji mkuu, mlipaji mkuu ni…

**SPIKA:** Sawa Mhehsimiwa Waziri, sehemu ndogo tu, neno Rais ndiye anayeidhinisha malipo ni sahihi au siyo sahihi? Sehemu ndogo tu hiyo.

**WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Spika, ni katika *levels* ile *bracket* ya matumizi yote ya Serikali kabla hayajaenda kwenye *level* ya utekelezaji idhini ya matumizi katika mwezi, *ceiling* ile katika mwezi lazima ipate idhini ya mamlaka.

**SPIKA:** Ahsante sana.

**WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mhehsimiwa Spika, siwezi tu kujua kwa awamu ya kwanza, ya pili na ya tatu lakini kwa awamu ya nne, ya tano na sasa hiyo ndio *practice* na idhini ikishatolewa ndio mnaendelea.

**SPIKA:** Haya ahsante sana Mheshimiwa. Waheshimiwa Wabunge nimeombwa mwongozo hapa kwa hivyo napaswa kutoa mwongozo kama jambo hilo linaruhusiwa ama haliruhusiwi. Wakati wa, nimeshatoa maelezo kwa sehemu ya kwanza kwa hiyo, sina haja ya kuyarejea hayo. Lakini ile kanuni aliyokuwa ameitumia Mheshimiwa Ole-Sendeka ya 71(1)(g) inazungumzia, inasema bila kuathiri masharti ya Ibara ya 100 ya katiba yanayolinda na kuhifadhi uhuru wa mawazo na majadiliano katika Bunge, Mbunge (g) hatatumia jina la Rais kwa dhihaka katika mjadala au kwa madhumuni ya kutaka kulishawishi Bunge kuamua jambo lolote kwa namna fulani. *(Makofi)*

Ametupeleka pia kwenye vifungu kadhaa vya katiba ametueleza kuhusu Ibara ya 136, 137 na ibara nyingine hapo zinazohusu malipo kutoka kwenye Mfuko Mkuu wa Serikali, lakini pia alieleza kuhusu matumizi ya Ibara ya 35, na mimi nataka nitoe mwongozo wangu kupitia hiyo Ibara ya 35 ambayo inaeleza kuhusu utekelezaji wa shughuli za Serikali na namna ambavyo Rais anakasimu madaraka yake.

Hiyo Ibara ya 35(1) inasema shughuli zote za utendaji za Serikali ya Jamhuri ya Muungano zitatekeleza na watumishi wa Serikali kwa niaba ya Rais. Ya pili kifungu kidogo cha pili kinasema amri na maagizo mengine yanayotolewa kwa madhumuni ya ibara hii yatathibitishwa kwa namna itakavyoelezwa katika kanuni zilizowekwa na Rais, kwa kuzingatia masharti ya katiba hii. Sehemu ya msisitizo ni yatathibitishwa kwa namna itakayoelezwa katika kanuni zilizowekwa na Rais, kwa hiyo shughuli za Serikali zinazofanywa, Rais anakuwa amekasimu kwa hao wasaidizi wake. *(Makofi)*

Sasa kwa muktadha huo kwa namna Mheshimiwa alivyoeleza kuhusu yale malipo na kwamba Rais anaidhinisha kwa mwongozo wa katiba na kanuni zetu malipo yale ya nafanywa na wale maafisa waliopewa kazi hiyo ya kulipa na sio Rais. Kwa hivyo, lile neno idhini kwamba Rais ndiye anayeidhinisha malipo, katiba yetu imeshaweka wazi, kanuni atakuwa ameziweka Rais namna ya yale kama kuna maagizo mengine ya ziada ambayo katiba haijasema. *(Makofi)*

Sasa kwa mwongozo ambao umeuomba Mheshimiwa Ole-Sendeka jina la Mheshimiwa Rais kwa maana ya matumizi kwenye kifungu hiki kwa sababu kwanza tulikuwa hatuelekei kwenye kufanya maamuzi yoyote lakini pia mtoa taarifa hakulitumia jina la Rais kwa dhihaka, kwa hiyo, lile linaondoka lakini kwa maana ya maelezo yale yaliyotoka kuhusu Rais kwamba anaidhinisha kila malipo, Rais amekasimu hayo madaraka kwa maafisa wake kwa mujibu wa katiba yetu inavyosema. *(Makofi)*

Kwa hiyo, kwa Rais kupata taarifa kwamba kuna jambo fulani ambalo lina paswa kufanyiwa kazi au kuna malipo fulani yanapaswa kufanyika si kwa kutaka idhini kwa Rais kwa sababu Rais ameshatoa, ameshakasimu hayo madaraka kwa watu wengine na ndio maana Mheshimiwa Ole-Sendeka uko sahihi kwamba Rais hausiki kwenye jambo hili la malipo moja kwa moja. *(Makofi)*

Nadhani kwa mwongozo huu nilioutoa huo ndio utaratibu, Rais hausiki moja kwa moja kwenye malipo kwa hivyo pia hausiki kwamba malipo yatakapofikia mahali ukaguzi tumefanya, tunaanza kunyoosha vidole kule, Hapana. Katiba yetu imeeleza wazi wanaofanya kazi ambao wamekasimu madaraka kwao. Kwa hiyo, kama kuna namna ambayo kanuni alizotenegeneza yeye zinaelekeza kwamba jambo fulani lazima ajulishwe sasa lile ni jambo la Kiserikali, sio

jambo ambalo linahusu jambo la jumla kama hili. Nadhani nitakuwa nimeeleweka kwa muongozo huo. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo kabla sijasitisha wako wabunge ambao tutawasikiliza michango yao katika hoja hii ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, tutawasikiliza katika kipindi chetu cha pili kwa maana ya kipindi cha mchana, tunao Mheshimiwa Hamida Mohamed Abdallah, tunao Mheshimiwa Priscus Jacob Tarimo, Mhehsimiwa Emmanuel Peter Cherehani, na wengine wataendelea kutajwa kadri muda utakavyokwenda.

Baada ya kusema hayo nasitisha Shughuli za Bunge mpaka Saa Kumi Kamili jioni leo.

*(Saa 7.15 mchana Bunge lilisitishwa hadi Saa 10.00 Jioni)*

*(Saa 10.00 Jioni Bunge lilirudia)*

*Mwenyekiti (Mhe. Daniel B. Sillo) alikalia kiti*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa tukae.

Katibu.

**NDG. EMMANUEL MPANDA – KATIBU MEZANI:**

**HOJA ZA SERIKALI**

**Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Waziri Mkuu kwa Mwaka wa Fedha 2023/2014**

*(Majadiliano Yanaendelea)*

**MWENYEKITI:** Ahsante, Waheshimiwa Wabunge mjadala wa hoja iambayo iko mbele yetu na inayoendelea ni hoja ya Ofisi ya Waziri Mkuu. Hapa ninayo orodha ya wachangiaji.

Tutaanza na Mheshimiwa hamida Mohamed Abdallah, atafuatiwa na Mheshimiwa Priscus Jacob Tarimo, Mheshimiwa Emmanuel Peter Cherehani ajiandae.

**MHE. HAMIDA M. ABDALLAH:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia Bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kukupongeza wewe binafsi kwa kushika nafasi hiyo ya uwenyekiti na kuweza kuliongoza Bunge letu, na Mwenyezi Mungu aendelee kukuongoza na kukubariki. Pia nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa kuwasilisha taarifa ya utekelezaji wa miradi mbalimbali ya maendeleo katika kipindi cha mwaka 2023/2024. Taarifa ni nzuri, imesheheni mambo mbalimbali ya maendeleo yaliyotekelezwa na miradi mikubwa ya kimkakati. Vile vile imegusa maeneo mengi katika kuboresha sekta mbalimbali kama vile sekta za elimu, afya, barabara, kilimo na mambo mbalimbali.

Mheshimwa Mwenyekiti, nitumie nafasi hii kumpongeza kwa dhati kabisa Mheshimiwa Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa namna ambavyo ana maono makubwa pamoja na kuwa na mapenzi makubwa kwa Watanzania, mpenda maendeleo, mzalendo na mwanamapinduzi wa kweli mwenye huruma ya kipekee kabisa, na hatuna mfano wa kumfananisha. Tuendelee kumtakia kila la kheri na kumuombea maisha mema ili Mwenyezi Mungu aendelee kumuongoza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ninaomba nizungumzie suala la kilimo. Niipongeze Serikali kwa kuendelea kuiimarisha sekta ya kilimo. Tumeona namna mbalimbali ambavyo inaendelea kuimarisha kwa kuifanya Benki ya Kilimo kuendelea kukua na kuendelea kuwahudumia wakulima wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeona namna ambavyo Serikali inaendelea kutoa ruzuku. Si hivyo tu, bado tumeendelea kuona namna ambavyo wanapata mafunzo mbalimbali ya kufanya kilimo chetu kiwe kilimo cha biashara na kuendelea kupata masoko kupitia mitandao mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hayo bado tuna changamoto katika eneo la kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mikoa yetu ya Kusini, sisi wana Kusini zao letu kubwa ni zao la korosho, na ni zao la biashara, ni zao ambalo linatufanya wananchi tuweze kuishi na tuweze kumudu kuendesha maisha yetu. Kwa hiyo panapotokea changamoto ya kutetereka zao la korosho hata kidogo tunapata shida kubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi cha miaka mitatu mfululizo tumeona kwamba bei ya korosho inazidi kuporomoka. Hii ni changamoto kubwa sana kwa wakulima ukizingatia kwamba zao hili unapozalisha, unapolihudumia mpaka kufikia hatua ya kupeleka sokoni pana njia ndefu na mchakato ni mrefu sana. Sasa, mkulima anategemea anapopeleka sokoni anaweza kupata bei nzuri ya kuweza kurudisha gharama ambazo ameweka katika kuhakikisha kwamba anazalisha korosho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba sana Serikali ilitazame suala hili la bei ya korosho na tuhakikishe kwamba tunawatia nguvu wakulima ili waendelee kuwa na moyo wa kulisimamia zao hili la korosho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa pembejeo Kanda ya Kusini tuna msimu wa kalenda ya upuliziaji (Sulphur) kwenye mikorosho. Sasa, kanda ya kusini hatulingani na kanda nyingine. Tunaiomba Serikali kutuletea pembejeo kuendana na kalenda yetu ya kilimo cha korosho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile bado tuna hoja ya usajiri wa wakulima wetu. Tunajua kwamba Serikali inaendelea kusimamia usajiri wa wakulima ili kuwabaini wakulima wa korosho waweze kupata huduma nzuri kutoka Serikalini na kuwabaini na kujua idadi ya mikorosho ambayo ipo katika maeneo ambayo tunalima korosho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini nitumie nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Mohamed Bashe, Waziri wa Kilimo kwa kuja na Mpango wa Jenga Kesho Ijayo Iliyo Bora. Mpango huu wa kuwashirikisha vijana kuingia katika sekta ya kilimo, kuwafanya vijana waweze kupata mafunzo na kupata mitaji ili kuingia katika uzalishaji wa shughuli za kilimo ni mpango mzuri. Si hivyo tu, pia kuwafanya vijana hawa kuwasimamia na kupata masoko ya mazao ambayo wanayalima.

Mheshimiwa Mwenyekiti huu ni mpango mzuri kwa sababu unatuongezea ajira kubwa kwa vijana kwa sababu kumekuwa na changamoto kubwa sana ya ajira nchini. kwa hiyo mpango huu ni mzuri, lakini pia utakuza uchumi wetu kupitia shughuli zakilimo kwa vijana wetu. Tumeanza vizuri ingawa zipo changamoto ndogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa, kwa kuwa mpango huu ndiyo unaanza, tuutakie kila la kheri, Mungu aubariki uende salama na vijana wetu waweze kufanikiwa. Mwaka kesho tutakapokuja basi tuhakikishe kwamba katika maeneo yetu walau tutoe uwiano wa vijana wanaotoka katika majimbo yetu. Kwa mfano mwaka huu katika jimbo langu ametoka kijana mmoja tu, lakini ukiangalia katika majimbo mengine utakuta kuna vijana sita hadi nane katika jimbo moja. Kwa hiyo mwakani tuhakikishe kwamba tunaingia katika uwiano ambao walau kidogo unafananafanana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie kuhusu nishati. Tunaishukuru Serikali, kwamba inaendelea kusimamia na

kuimarisha sekta ya nishati. Zipo changamoto ndogondgo ambazo zinaendelea, lakini Serikali bado inaendelea kuzisimamia kuhakikisha kwamba Watanzania tunapata umeme.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna matumizi ya gesi nyumbani. Sisi pale Lindi Manispaa tulianza na mpango huu katika Kata ya Mnazi Mmoja, na Serikali imeweka miundombinu ya matumizi ya gesi nyumbani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Watanzania tunatamani sasa kufanya matumizi ya gesi nyumbani na kuondokana na matumizi ya mkaa na kuni, lakini bado tuna changamoto. Changamoto iliyopo ni kwamba vifaa vya matumizi, majiko, pasi na vifaa vingine ambavyo vinatumika nyumbani vimekuwa vya gharama kubwa. Niiombe sana Serikali kuhakikisha kwamba vinapunguza kodi ili Watanzania walio wengi waweze kumudu kununua majiko ya gesi na umeme ili tuondokane na matumizi ya kuni na mkaa. Hii itaweza kutusaidia katika kuhakikisha kwamba tunatunza mazingira yetu, lakini pia itatusaidia kuona kwamba wanawake ndio watumiaji wakubwa wa majiko haya. Tuta-*solve* muda mwingi wa kukaa jikono na badala yake tutakwenda kufanya shuhguli mbalimbali za maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo ninaomba tuhakikishe kwamba kodi inapungua katika vifaa hivi na kuwafanya watu wengi waweze kutumia gesi nyumbani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nuzungumzie suala la Mradi wa *LNG*. Tunashukuru kwa hatua mbalimbali ambazo tumeenda nazo, na tunamshukuru Mheshimiwa Rais alitoa idhini ya kusaini mkataba wa awamu ya kwanza, na walituambia kwamba mkataba wa pili utasainiwa mwezi wa 12, lakini leo tunapoongea ni mwezi wa nne. Hatujui kuna changamoto gani zilizojitokeza zilizosababisha mkataba huu uwe haujasainiwa awamu ya pili. Wana Lindi na Watanzania

wanatamani kusikia changamoto ni nini na awamu ya pili ya kusaini mkataba huu itakuwa ni lini ili tuelekee kwenye utekelezaji wa mradi huu wa *LNG*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile tunayo changamoto kwa wazalishaji wa chumvi. Sisi tunaoishi ukanda wa bahari tunazalisha chumvi, lakini wazalishaji wetu wa chumvi wanapata changamoto ya masoko na bei kuporomoka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunajua kwamba tumefungua fursa za uwekezaji nchini, na tumetoa leseni kwa Mwekezaji mkubwa wa kuweka kiwanda cha chumvi nchini, kwa maana ya kwamba atusaidie kununua chumvi iliyopo ndani ya nchi yetu. Hata hivyo, matokeo yake mwekezaji yule ananunua chumvi nyingi kutoka nje na chumvi yetu ya Tanzania inaendelea kukaa. Kwa hiyo hii ni changamoto kubwa. Kama tatizo ni kwamba chuvi yetu haina ubora ule unaotakiwa ni vizuri mwekezaji akaja kutufundisha ni chumvi ya aina gani yeye anaitaka ili Watanzania waweze kuzalisha na kupata soko la chumvi. Hili ni jambo muhimu, tulisimamie na kulizingatia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna Wenyeviti wetu wa Serikali za Mitaa; wenyeviti hawa wanatufanyia kazi nzuri sana. Hata hivyo wenyeviti hawa hatuwapi nafasi yoyote ya kuwanunulia vifaa; vifaa wananunua wenyewe lakini kazi zetu wanatufanyia. Inafika wakati wenyeviti hawapati posho yao. Sasa tujue, kupata posho yao ni halali ama si halali? Na kwa nini hawapati posho zao. Tutafute namna ya kutatua changamoto hii tuliyonayo, hasa kule kwetu Lindi Manispaa, wenyeviti wana miezi 16 hawajapata posho zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunayo miradi ya *TACTIC*, na sisi Lindi Manispaa tumeingia katika…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa, nakupa sekunde 30 umalizie.

**MHE. HAMIDA M. ABDALLAH:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru kwa kunipa nafasi. Mambo mengine nitaandika kwa maandishi ili Serikali iweze kutusaidia mambo kadhaa ambayo tunayahitaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo ninaunga mkono hoja, ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Nilimtaja Mheshimiwa Priscus Jacob Tarimo, atafuatiwa na Mheshimiwa Emmanuel Peter Cherehani, Mheshimiwa Stanslaus Shing'oma Mabura ajiandae.

**MHE. PRISCUS J. TARIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa nafasi hii ya mimi pia kuchangia hotuba hii ya Bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu. Nianze kwa kusema kwamba ninaunga mkono hoja, ikiwa ni pamoja na haya nitakayokwenda kuyasema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuchangia mimi nitakwenda kwenye mfumo wa kurasa ili niweze Kwenda haraka. Ninaanza ukurasa wa 13, ambapo kwenye hotuba wameongelea Kiwanda cha Sukari cha Mkulazi. Napongeza sana hatua hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo kuna matatizo. Mashirika haya ya Serikali ambayo yanafanya biashara yamekuwa hayafanyi vizuri. Mfano mzuri ni pamoja na kile Kiwanda cha Ngozi ambacho kipo pale Moshi Mjini, ambacho kilitakiwa kiwe kinaajiri angalau watu 3,000; na kwenye mnyororo wake wa faid ampaka watu 10,000. Hata hivyo mpaka sasa kimeajiri watu 250 tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili hizi taasisi za kibiashara za Serikali zifanye vizuri ni vizuri namna ya kuwapata viongozi wake isiwe kwa namna ya uteuzi na badala yake tuwe tunawatafuta kutokana na *merits*, uwezo na *competence* yao kwenye hizo *fields*. Kwa kufanya hivyo viwanda hivi vitafanya kazi vizuri. Kwa hiyo kwenye hiki kiwanda kinachoanzishwa, ikiwa ni pamoja na vingine watu wapatikane kwa *merits* ili waweze kuviendesha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niende ukurasa wa 14 na ukurasa wa 45 ambao umeongelea viwanja vya ndege. Nichukue nafasi hii kumshukuru sana Mheshimiwa Rais, Mama Yetu Samia Suluhu Hassan. Moshi Mjini tunarekebisha kiwanja chetu cha ndege ambacho ni muhimu sana kwa Moshi Mjini, Mkoa wa Kilimanjaro pamoja na nyanja mbalimbali ikiwemo utalii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilete ombi; kuna nyumba ambazo zilivamia eneo lile; baadhi zina hati na nyingine hazina hati. Niombe, ili kuleta tija zaidi kwenye ule uwanja vile viwanja tutafute namna ya kuvifidia wakati huu ambapo mradi unaendelea ili kiwanja kile kiweze kupanuliwa katika kiwango kinachotakiwa kuwezesha mpaka hizi ndege hizi za bombardier kutua pale na kuleta tija zaidi. Kwa hiyo, kwa sababu ujenzi unaendelea ni rahisi kwa Wizara kuweka fidia pale kwa baadhi ya zile nyumba ili kuweka sura ile inayotakiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niendele ukurasa wa 41, na hili linaendana sana na swali ambali nimeliuliza asubuhi kwenye maswali ya nyongeza. Kwenye matumizi bora ya ardhi, pale kwenye ukurasa wa 41, hotuba imeelezea vizuri sana; lakini kuna maeneo ambayo yanahitaji kupewa kipaumbele zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Moshi Mjini ina ukubwa wa eneo la kilometa za mraba 58. Tulishaleta maombi yaliyopita kwenye michakato yote, ya kuongeza eneo eneo mpaka

kufikia kilometa za mraba 142, na tulishapata *GN No. 219* ya tarehe 15 Julai, 2016. Mchakato ule ulisimama. Nimeshaandika barua nimepeleka kwa Waziri Mkuu, Wizara ya Ardhi na TAMISEMI ili kuomba huo mchakato tu kwanza wa kupanua ile mipaka ukamilike. Tunaomba hivi kwa sababu ninavyoongea hapa sasa hivi Moshi Mjini tumekosa eneo la dampo, tumekwenda kununua eneo Moshi Vijijini ndiko dampo letu liliko. Pia makaburi yetu yanajaa, tutalazimika Kwenda kununua tena maeneo mengine ya makaburi na huduma nyingine za wananchi ilhali tayari kuna mchakato ulishafikia sehemu nzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, na niseme, kwa pale tulipo sasa, kwa sababu ni padogo sana hata pato letu haliwezi kuongezeka, hata eneo la viwanda haliwezekani kwa sababu viwanja vinakwenda pembezoni. Hata hivyo, zaidi ni kwamba yale maeneo ambayo tuliyaweka kwenye *master plan* ya kipindi cha nyuma, kwa ajili ya kupanua, tayari yanaendelea kuvamiwa na kujengwa kiholela. Si tu kuvamiwa, watu wanauza na yanajengwa kiholela. Maana yake ni kwamba hata mtakapokuja kuturuhusu kupanuka tutapanuka kuendana na maeneo ambayo hayajapangika vizuri. Kwa hiyo ninaomba sana hili la Moshi Mjini mlichukulie kwa uzito wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niende ukurasa wa 51, umeeleza vizuri sana juu ya elimu, na mimi hapa nitagusa Wizara zote mbili, Wizara ya Elimu na Wizara ya TAMISEMI kwa sababu ni suala ambalo linagusa kote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pale Moshi Mjini tuna Shule ya Sekondari ya Mawenzi, ni shule nzuri, ina miundombinu mizuri na ina eneo kubwa. Shule hii ina mchanganyiko. *O-Level* wako *day* lakini *A-Level* wako *boarding.* Ninaleta ombi, Wizara ionge namna ya kuifanya shule hii iwe na *boarding* kuanzia *O-Level* mpaka *A-Level.* Hii ni kwa sababu kuna eneo kubwa hivyo itakuwa miongoni mwa shule nzuri kama zilivyo

Shule ya Moshi na Shule *Moshi Tech*. Kwa hiyo tunaomba sana watuwekee mabweni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini shule mpya tuliyoijenga, shule ya Msandaka ambayo iko pembezoni kidogo, nayo Halmashauri tumetenga zaidi ya milioni 150 kwa ajili ya mabweni. Tunaomba Wizara sasa nayo iangalie ili tuongeze shule hizi za mabweni katika manispaa yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niende kwenye ukurasa wa 61 na 62, kumeongelewa masuala ya kazi, wafanyakazi na mifuko ya jamii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna viwanda vya Serikali vilibinafsishwa. Kiwanda cha magunia, Kiwanda cha *Moshi Leather,* kiwanda cha *utilization*; wafanyakazi waliokuwa wanafanya kazi kwenye hivi viwanda wakati vikiwa vya Serikali hawajawahi kulipwa mafao yao na wanaendelea kudai. Wanasumbuka kuja ofisini kwangu kwa makundi kila siku, na wengine mpaka wameshaaga dunia wakiendelea kudai. Naomba Serikali ifanye mpango, iangalie namna ya kutafuta fedha ili kuwalipa waliokuwa watumishi wa mashirika ya umma yaliyobinafsishwa ambao wanatangatanga, hawapewi hatima yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye ukurasa wa 62 ni kuhusu mifuko ya jamii, nako kumekuwa kuna usumbufu mkubwa usio wa lazima. Baadhi ya watu wanapokuwa wamemaliza muda wao wa utumishi, wengine ni watumishi wa Serikali, kama walimu, unakuta amestaafu kabla hajapandishwa daraja. Anapokwenda kutafuta daraja lililokuwa haki yake anazungushwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa, wastaafu hawa ambao wameshaitumikia Serikali wanapopata huu usumbufu kwa kweli wanatupa picha mbaya sana kw ahata hawa

wanaotumika sasa hivi kuona kwamba unaweza ukatumikia kwa moyo lakini mwishowe ukaja ukapata mateso.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukurasa wa 65 ni kuhusu uwezeshaji wa wananchi kiuchumi; nilishaliongea mara nyingi na ninashukuru sana Mheshimiwa Rais ameona twende kwa njia hiyo. Hii mikopo ambayo hairejeshwi ni kwa sababu ya watu tuliowapa kazi hiyo, Maafisa Maendeleo ya Jamii hawana utaalam wa ku-*assess* mradi, kukopesha na kwenda kuchukua mkopo huo. Ninaungana moja kwa moja na wazo la Mheshimiwa Rais kwamba tutafute benki ambazo tutawapa hizi kazi na sisi tuendelee kuwa wasimamiaji wakuu na kusiwe na *interest* wala *collateral* kama ilivyo, ni jambo linalowezekana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukurasa wa 69 na 73, kuhusu mapambano dhidi ya rushwa na mapambano dhidi ya dawa za kulevya; kwa bahati mbaya hapa nitatumia lugha ambayo si rafiki sana. Kwa hii rushwa tunayoona, kwa haya mazingira tunayoyasikia kutokana na taarifa ya *CAG* suala ya rushwa tuchukue njia waliyoichukua China, tutoe adhabu kali zaidi, miaka 30, 40, 50, hata ikibidi adhabu za kunyongwa, kwani tunachoogopa ni nini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna siku tulikuwa na mjadala kuhusiana na adhabu ile ya kubaka. Mtu akibakwa afanywe nini miaka 30, mmoja wa watu waliokuwa wameshiriki ile washa akasema hapana ni kubwa mno tukamwambia basi wewe umejiandaa kubaka. Kama wewe unaona adhabu hiyo ni kubwa umejiandaa kufanya hilo tukio. Hili suala la rushwa, suala la madawa ya kulevya tupitishe sheria hapa itakayoweka adhabu kali, miaka 30, 40 na ikibidi kunyongwa kwa wale wanaoshiriki ili tukomeshe, kwa sababu tunapoona aibu kusema hivyo maana yake hawa wanaokosa hizo haki nao wanateseka na wengine wanakufa kwenye mahospitali na kwenye maeneo yetu ya haki. Kwa hiyo, mimi nimeona

nichukue njia hiyo ngumu kuishauri Serikali tufikirie suala hilo kwa njia hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukurasa wa 83, kuna ukatili dhidi ya watoto. Nashukuru sana kwa sababu maazimisho ya Dawati la Jinsia Kitaifa yalikuja kuzinduliwa Moshi Mjini na taarifa iliyosomwa na Waziri wa Kisekta Dkt. Gwajima, ilionesha katika asilimia 100 ya watoto wanaofanyiwa ukatili, asilimia 60 wanafanyiwa nyumbani na kwa sababu nyumbani wanafanyiwa na ndugu na kama ni ndugu maana yake kesi haziendi mahali. Sasa tuna kitu cha kufanya, ni lazima tutafute namna bora hata ikibidi tuwe na namba maalum ya watoto kuweza kuifikia, wakifanyiwa ukatili waweze kutoa taarifa na inapoonekana ni ndugu, sisi Serikali tuichukue sisi na sio ndugu, maana ndugu wanaombana msamaha, wanamaliza wakati mtoto anakuwa ameshaharibika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni lazima tuwe na njia ya kuhakikisha tunawalinda hawa watoto. Haya madhara ambayo tunayaongelea ya hii tabia inayokuja pengine wengine wanalazimika kwenda kwa sababu walishafanyiwa ukatili, wakaona ile ndio njia. Kwa hiyo nashauri sana kwenye ukatili huu wa Watoto, tuwe na namba maalum ambayo watoto wanaweza kuipiga lakini tuwe na uwezekano wa kubadilisha sheria nazo ziwe kali na hata ikibidi tunaweza tukafanya vitu ambavyo kimsingi vitaonekana sio vizuri. Kwa mfano, hakuna sababu ya ndugu ambao wameshafikia umri wa *mature* kuendelea kukaa na kulala chumba kimoja na watoto wetu, tunaamini kwamba ni ndugu hawatawadhuru lakini taarifa ndio hiyo imetoka asilimia 60 wame…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa.

**MHE. PRISCUS J. TARIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuunga mkono hoja. Nakushukuru sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Priscus Jacob Tarimo. Mheshimiwa Emmanuel Peter Cherehani atafuatiwa na Mheshimiwa Stanslaus Shing'oma Mabula na Mheshimiwa Janejelly James Ntate ajiandae.

**MHE. EMMANUEL P. CHEREHANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nikushukuru lakini niendelee kukupongeza kwa nafasi hiyo ya pekee na unaonesha ujasiri mkubwa sana kwamba hatukukosea kukuchagua, hongera sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa nimshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa kibali cha pekee kusimama tena mbele ya Bunge lako Tukufu kwa ajili ya mchango mkubwa sana wa Mheshimiwa Waziri Mkuu. Kwanza kabisa niendelee kumpongeza sana Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kazi nzuri anazowafanyia wananchi wa Ushetu. Nina mwaka mmoja nikiwa Mbunge Bungeni lakini fedha zilizokuja Ushetu kwa mwaka mmoja ni zaidi ya Bilioni 17 zimeletwa na Mheshimiwa Rais.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye afya tu peke yake tumepokea zaidi ya bilioni 4.9, kwenye Kilimo ndio usiseme bilioni 21 ikiwemo na suala la ruzuku ya pembejeo, lakini kwenye elimu ni zaidi ya bilioni 5.8, ukienda kwenye maji na juzi tumepewa fedha nyingine za *BOOST* zaidi ya bilioni mbili, lazima tumshukuru Mheshimiwa Rais amefanya kazi kubwa sana. Pia lazima tumshukuru Mheshimiwa Rais hata wakati anaingia madarakani, mfano tu kwenye Benki ya Kilimo *(TADB)* ilikuwa na mtaji usiopungua bilioni 60 na ndio ilikuwa inawakopesha wakulima, lakini mwaka 2021 Mheshimiwa Rais alipeleka fedha zaidi ya bilioni 208 kwenye Benki ya Kilimo. Benki ya Kilimo hiyo hiyo mwaka 2022 iliweza kupeleka fedha kwa wakulima, kwenye viwanda zaidi ya shilingi bilioni 268,

ina maana ni zaidi ya asilimia 102, ni kazi ya Mheshimiwa Rais, ni kazi ya Rais wetu kafanya kubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niendelee kuomba tu, tunaongelea sana wakulima na ni asilimia 60 ya Watanzania wako vijijini wanalima. Niendelee kumpongeza sana Mheshimiwa Rais na Wizara ya Kilimo, lakini tuendelee kuipelekea fedha *TADB* Benki yetu ya Kilimo kwa sababu inahitaji mtaji mkubwa. Wakulima wengi wako vijijini hawana mitaji hawana mikopo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikukumbushe tu kwenye azimio letu la mwaka jana Novemba, 2022, tuliazimia benki hii iwe inapewa bilioni 100 kila mwaka kwa ajili ya kuongeza mtaji wake na kwenye Azimio namba saba, naomba kwa ridhaa yako niweze kusoma kipengele kidogo; "Kwa kuwa pamoja na jitihada za Serikali kuipa kiasi kikubwa cha bilioni 208 mwaka 2021, kuna ahadi ya Serikali ambayo kama ingewezeshwa benki hii ingekuwa na mtaji wa jumla ya bilioni 706."

Mheshimiwa Mwenyekiti, niendelee kukuomba benki hii ipelekewe fedha ili iendelee kuwakopesha wakulima wadogo wadogo, iendelee kukopesha vyama vya ushirika na ndio iliyotoa mfano mkubwa sana kupeleka fedha kwenye vyama vya ushirika. Vyama vingi vya Ushirika mwaka huu vimenunua pamba na vimeleta ushindani sana kwenye nchi yetu. Kwa nini sasa bilioni 100 hii isiendelee kupelekwa kila mwaka?

Mheshimiwa Mwenyekiti, niendelee kukuomba Mheshimiwa Mwenyekiti na Bunge lako Tukufu benki hii ipelekewe fedha. Nishukuru sana hata kwenye taarifa ya *CAG* tumeona na ndio benki iliyofanya vizuri zaidi hata kwenye taarifa za ukaguzi. Kwa hiyo niendelee kuipongeza Menejimenti ya *TADB* pamoja na Mkurugenzi wake

wamefanya kazi kubwa sana, kikubwa tuendelee kuisimamia ili iendelee kuwasaidia sana wakulima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la umeme; Kahama ni mji mkubwa sana na unaokua kwa kasi sana, lakini una changamoto kubwa sana ya umeme pamoja na halmashauri zake, hakuna umeme wa uhakika, unakatikakatika kwa muda wote na ndio mji unaokusanya fedha nyingi pamoja na halmashauri zake Ushetu pamoja na Msalala, lakini ukiambiwa mpaka leo hali ya umeme ni mbaya mno. Hata upande wa *REA* nikiongelea kwenye Jimbo la Ushetu, kata zangu 10 hazina umeme kabisa wa uhakika, umeme ni wa kusuasua na kinachosikitisha sana ni Mkandarasi, haiwezekani Wilaya ya Kahama yenye halmashauri tatu inapelekewa Mkandarasi mmoja. Mkandarasi huyo huyo awepo Msalala, Mkandarasi huyo huyo aweke Ushetu, Mkandarasi huyo huyo awe Kahama Manispaa, haiwezekani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia Kata yangu ya Mapamba, Ulewe, Ubagwe, Ulowa, Idahina, Chambo, Mpunze, Gulungwa, Nyamilangano pamoja na Bhutibu mpaka tunavyoongea havina hata ile kilometa moja moja, ni kidogo mno, ni maeneo makubwa yamesimamishiwa nguzo tu. Kwa hiyo ningeomba suala hili umeme uende lakini maeneo ambayo miji yake inakua kwa kasi Wakandarasi kwani kuna shida gani ya kupeleka Ushetu kuwa na Mkandarasi wake, Msalala kukawa na Mkandarasi pamoja na Manispaa kukawa na mkandarasi wake. Malalamiko mengine ya wananchi tunayasababisha sisi kwa sababu huwezi kupeleka Mkandarasi mmoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye suala la *TARURA* hiyo hiyo Kahama ina Meneja mmoja wa *TARURA* na Halmashauri zake tatu. Meneja huyo Ofisi yake iko Kahama Manispaa lakini huko huko aende kuzungukia kata 20 za Ushetu na vijiji 112 na vitongoji 560, barabara haziwezi kufunguka. Huyo

huyo aende Msalala kwenye kata 18, huyo huyo abaki Mjini kwenye Manispaa ya Kahama kwenye kata 20, Meneja mmoja wa *TARURA*. Tulikuwa na Meneja wetu kwenye halmashauri zetu, lakini wakaondolewa wakarudishwa makao makuu wakapewa kazi ya ku-*survey* tu, meneja akabaki mmoja tu, haiwezekani!

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Mameneja wetu warudishwe, kama tunahitaji twende vizuri kwenye bajeti zetu za upande wa TAMISEMI, Mameneja hawa warudishwe haraka kwenye halmashauri zetu. Hali ni mbaya na tunavyoongea leo hali ya Ushetu ni mbaya mno. Barabara inayotoka Kata ya Ulewe kufanya mawasiliano na Halmashauri ya Ushetu ili wananchi waende kutibiwa kwenye hospitali yao ya wilaya, hakuna barabara, imekatika, wananchi hawapiti kabisa. Pia Kata ya Ubagwe kwenye Daraja la Ubagwe kuja Ulowa kwenda kwenye Hospitali ya Halmashauri ya Ushetu, hakuna mawasiliano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Naibu Waziri wa Ujenzi tuambatane naye kesho kwenda kushuhudia adha hii, kwa sababu mwaka jana hili nililisema kwenye bajeti ya Wizara ya Ujenzi kwamba barabara hizi zimeshatoka *TARURA* zimepelekwa *TANROADS,* zinahudumiwa na Mkoa, lakini hakuna fedha zilizotengwa za matengenezo. Sisi kama Wabunge tunatakiwa tulie kwa nani, tulalamike kwa nani, tumwambie nani ili tuweze kufikishiwa huduma zetu kwa wananchi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunasubiri mpaka tatizo litokee, wananchi waende na maji, akinamama wanaoenda kujifungua hospitalini waende na maji, ndio tukimbie sasa na magari yetu kwenda kuona tukio! Naomba niende na Naibu Waziri au Waziri wa Ujenzi akashuhudie kesho adha ambayo leo wanaipata wananchi wangu katika Jimbo la Ushetu. Barabara hazipitiki, naomba mwaka huu zitengewe fedha ili ziweze kutengenezwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nizungumzie suala la maliasili; jimbo langu ni kati ya majimbo yanayopakana na mapori mengi. Halmashauri yangu kupitia Baraza la Madiwani tulishakaa tukaomba wafugaji wetu watengewe eneo la malisho. Tumepeleka barua kwenye Ofisi ya Maliasili, tukapeleka barua TAMISEMI watutengee eneo kwa sababu ni maamuzi ya Baraza la Madiwani, lakini tunavyoongea ni mwaka wa pili hajaja hata Waziri kuja kushuhudia kwamba ni eneo gani, ni pori gani angalau walete wataalam litengwe kwa ajili ya malisho kwa sababu ni pori la halmashauri. Wafugaji wetu sasa hakuna mahali pa kuchungia, lakini wafugaji wetu hawa hawa wakiingia kwenye hayo mapori wanakamatwa na wanafilisiwa ng'ombe wao, hatuwezi kulikubali hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimwombe Mheshimiwa Waziri twende tukashuhudie wananchi wangu eneo walilolitenga, angalau watoe ushauri kwamba pamoja na kwamba Baraza la Madiwani limetenga eneo hili, lakini ushauri wetu ulikuwa moja mbili, tatu, lakini hawataki hata kwenda. Naomba kupitia Bunge lako Tukufu, Mheshimiwa Waziri wa Maliasili twende akashuhudie wananchi ambapo wametenga eneo la malisho tuwasaidie.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ambalo naomba niliseme, tuna wananchi wenzetu ambao wanahangaika na mikaa, sijajua kwa nini Wizara ya Maliasili inabaki kupitia *TFS* kukamata tu wananchi, kukamata sio suluhu. Tumeanza kukamata wananchi hao na kuwaweka na kuwachomea baiskeli, kuchoma mkaa toka uhuru. Hivi hatuna akili ya kubuni kwamba twende na utaratibu gani sasa? Hivi kwa nini Wizara ya Kilimo imekuja na hoja ya kutenga mashamba ya *block farm* kwa ajili ya wakulima ambao hawana mitaji. Sasa maliasili inashindwaje kutenga maeneo ambayo yatakuwa *special* kwa wananchi wadogo wadogo ambao wanajishughulisha na biashara ya mkaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, watu hawa watengewe maeneo wakapande miti ili waweze kuvuna miti yao badala ya kuwakamata. Wamewakamata miaka mingapi toka uhuru, leo miaka 61 tunakamata wamepata nini? Wameacha kuchoma mikaa? Si wako barabarani na baiskeli kila siku. Kwa nini gharama ambayo wanatumia kukimbizana nao kwenye magari wasiitumie sasa kuwa…

**MWENYEKITI:** Naomba umalizie mchango wako, sekunde tatu.

**MHE. EMMANUEL P. CHEREHANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nikuombe tu, kwanza naunga mkono hoja, lakini niwapongeze sana Wizara ya Fedha kwa kutupelekea fedha nyingi kwenye sehemu ya Kilimo, lakini suala la maliasili na suala la Waziri wa Ujenzi, naomba tuondoke naye akashuhudie hali iliyopo katika Jimbo la Ushetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa. Nimwite Mheshimiwa Stanslaus Shing'oma Mabula, atafuatiwa na Janejelly James Ntate na Mheshimiwa Salma Rashid Kikwete ajiandae.

**MHE. STANSLAUS S. MABULA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia jioni hii na nitumie nafasi hii kumshukuru sana Mungu lakini kukupongeza pia kwa kupata nafasi ya kuaminiwa na Bunge kwa ajili ya kutuongoza sisi wenzako. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa leo napenda kuzungumzia mambo machache yasiyozidi matatu. Ningependa nianze na suala la kwanza ambalo kwenye bajeti ya Mheshimiwa Waziri Mkuu liko jambo ambalo amelizungumza katika ukurasa wa 37 linalohusu masuala ya Maliasili na Utalii pamoja na ukurasa wa 46 linalohusu viwanja vya ndege.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sote tunafahamu namna bora ya kusaidia utalii katika nchi hii ni pamoja na kuunga jitihada kubwa zilizofanywa na Mheshimiwa Rais katika Filamu yake ya *Royal Tour* ambayo imetusaidia sana kuleta watalii wengi nchini. Tumekuwa tukisema kila mara juu ya Uwanja wa Ndege wa Mwanza. Natamani sana kuona bajeti hii tutakapokuwa tunakwenda kuihitimisha Uwanja wa Ndege wa Mwanza uwe umetengewa fedha zitakazokwenda kuujenga na kuukamilisha kwa ujumla wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, zipo sababu nyingi za kwa nini tunahitaji uwanja wa ndege wa Mwanza ukamilike. Hivi tunavyozungumza jana kule Arusha ndege ya *KLM* imeshindwa kutua kwa sababu za hitilafu ya uwanja na kulazimika watalii kwenda kushushwa Entebbe. Mpaka hivi ninavyozungumza inawezekana watalii wote waliokuwa wanakuja Tanzania kwa Ndege ya Shirika la *KLM* wako Entebbe na hawana namna tena ya kurudi hapa mpaka pale Wizara ya Maliasili na Utalii itakapojipanga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maana yangu ni nini? Laiti uwanja uliopo Mwanza ungekuwa umekamilika na kuwa Uwanja wa Kimataifa wa Ndege ingekuwa ni rahisi sana kwa ndege ya *KLM* kutua Mwanza na abiria wote wakaendelea na shughuli za utalii hapa hapa nchini. Kwa hiyo nitoe wito kwa Serikali kwamba jambo hili ni la muhimu na tulitazame upya kuhakikisha kwamba Mwanza ambayo tunaitazama kama *hub* ya utalii kwa kanda ya ziwa, basi iweze kufanikiwa na kutoa matunda ambayo tunayategemea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, nilitamani sana nizungumzie habari ya wafanyabiashara ndogo ndogo, Machinga. Niiombe sana Serikali, nafahamu imekuwa na utaratibu mzuri toka Mheshimiwa Rais alipotoa maelekezo wafanyabiashara ndogo ndogo nchini wote walitii na kwenda kwenye maeneo yaliyopangwa. Bahati mbaya sana ni maeneo machache sana yaliyojengwa kwa nguvu ya

Serikali, maeneo mengi yamejengwa kwa nguvu za wananchi, wale wafanyabiashara wenyewe, lakini wajibu wa Serikali ilikuwa ni kuimarisha maeneo haya ya kibiashara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa niiombe sana Serikali, wafanyabiashara na Serikali itazame, yako mambo hakuna sababu ya kuyaunganisha nchi nzima. Ukizungumza habari ya wafanyabiashara ndogondogo nchi hii iko miji ukiitazama tu unaweza ukaichukua hiyo na ukatengeneza mazingira bora yatakayowasaidia wafanyabiashara, Mkoa wa Mwanza, Mkoa wa Dar es Salaam kwa ujumla wake, Mkoa wa Arusha, Mkoa wa Mbeya lakini na hii sio Mkoa kwa ujumla nikisema Mwanza namaanisha Manispaa ya Ilemela na Jiji la Mwanza *per se*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, watu wamejenga masoko, lakini mpaka leo masoko hayana namna bora ya kuwasaidia hao wafanyabiashara. Tafsiri yake tunaanza kuwaacha holela na wanaanza kufikiria kurudi kule walikokuwa kwa sababu na wao kule waliko wanatafuta riziki na huwezi kuipata riziki kwenye mazingira magumu. Kwa hiyo nitumie nafasi hii kuiomba Serikali, pale Mwanza walitengewa maeneo ya Igoma kule kwa Ukwaju, wakatengewa Dampo kule maeneo ya Buhongwa, lakini wakatengewa eneo moja pale Mjini Igogo ambalo linaitwa eneo la Mchafukoga. Maeneo haya toka wamejenga wenyewe Serikali ikawekeza nguvu kidogo na sasa tulipopata milioni 500 na nimshukuru sana Mheshimiwa Rais kuipeleka pale Mchafukoga, fedha hii ni kidogo.

Kwa hiyo, niombe Serikali itazame upya, kama tumeamua kuwapanga wafanyabiashara na wamekubali kwenda kwenye maeneo tuliyowapanga, basi ni lazima tuchukue makusudi ya lazima kuhakikisha tunapeleka fedha kwenda kuboresha maeneo waliyopo ili waweze kufanya biashara zao kwa uhuru na wale wanaokwenda kununua wawe na amani ya kwenda kununua kwenye yale masoko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukweli ni kwamba masoko yote yako kiholela. Masoko yote hayana ubora wa kumfanya mtu atamani kwenda kununua kwenye yale masoko. Kwa hiyo kwa namna yoyote ile bado tunaendelea kuweka ukinzani kati ya wafanyabiashara na Serikali na tunafahamu halmashauri zetu. Ukichukulia mapato wanayokusanya, ukachukulia fedha inayokwenda kwenye miradi ya maendeleo, hata iweje ukiwaambia wawekeze fedha zingine kwenye kuboresha yale masoko bado haitawezekana na itaendelea kulaumiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ziko hatua ambazo Mheshimiwa Rais alizielekeza na hatua hizi ni mahsusi. Niombe sana tunaposema Mheshimiwa Rais alielekeza maeneo yote waliyopangwa wafanyabiashara, usafiri wa daladala na mwingine utengenezewe mazingira ya kufika pale. Sasa inafika wakati Mbunge unashauri, Mkuu wa Wilaya anashauri, viongozi wengine wanashauri, lakini hakuna utekelezaji, maana yake ni nini? Hawa wafanyabiashara itafika wakati watachoka kwa sababu yale tuliyokubaliana nao hayatekelezeki na kufanya ugumu wa wanunuzi kushuka kwenye yale maeneo na kwenda kununua bidhaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo niombe sana, kwanza zichukuliwe hatua za dharula kuhakikisha maeneo yote tuliyotenga vinajengwa vituo vya daladala kwa lazima na kwa muda mfupi ili kuwarahisishia wanunuzi wafike kwenye maeneo hayo.

Pili, Serikali iwe na uwiano wa kupeleka fedha. Jiji la Mwanza ndio Jiji linaloongoza kwa wafanyabiashara wengi hapa nchini. Tuna wafanyabiashara, machinga, mama lishe na watu wa aina hiyo zaidi ya 12,000. Sasa ukichukua soko na nimshukuru sana Mheshimiwa Rais, tunajenga soko kubwa lakini uwezo wa soko hili utachukua watu takribani 1,400. Kati ya 1,400 ni machinga 200 peke yake ndio wanaweza kukaa humu ndani, lakini Ukwaju kuna Machinga zaidi ya 2,800,

ukienda Buhongwa pale kuna Machinga zaidi ya 3,600, ukienda Mchafukoga kuna Machinga zaidi 2,000, lakini mazingira sio wezeshi kuwafanya watu wafike kwenye haya maeneo. Kwa hiyo, niombe sana kama tuna dhamira njema ile ambayo Mheshimiwa Rais ameikusudia na sisi wasaidizi wake tuwekeze nguvu kuhakikisha mazingira haya yanakuwa bora na yanafanyiwa kazi kwa haraka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo ninaomba sana kama tunayo dhamira njema, ile dhamira ambayo Mheshimiwa Rais ameikusudia, nasi wasaidizi wake tuwekeze nguvu kuhakikisha mazingira haya yanakuwa bora na yanafanyiwa kazi kwa haraka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la tatu ni kuhusu *TASAF;* katika jambo amblao nataka kuishukuru Serikali na kuishauri iendelee kuwekeza nguvu nyingi zaidi ni kwenye mpango mpya wa *TASAF* ambao unawekeza katika miundombinu ya kudumu kwenye sekta ya afya, sekta ya elimu na sekta ya barabara. Kwa kufanya hivi utakubaliana nami, fedha nyingi ambazo tumeshazitoa kwa watu zaidi ya 14,000 tukitafuta uhalisia na thamani yake leo hatutaupata kwa haraka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninamshukuru sana Mheshimiwa Jenista Mhagama na hata ambapo amemuachia Mheshimiwa Simbachawene leo naamini kazi hii itaendelea. Ukienda pale Nyamagana peke yake tumepata ujenzi wa shule mpya pia tumepata ujenzi wa kituo kipya cha afya. Tumejenga barabara zaidi ya kilometa 416. Huu ni mpango ambao kupitia mradi wake wa *OPEC,* kama utaendelea hivi utawakwamua sana wananchi kwa ujumla wao wengi kuliko ilivyo hivi sasa inavyokwenda kwa mtu mmoja mmoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la nyongeza ninaomba sana awamu ya pili ya *OPEC* ilitakiwa ianze mwezi huu wa Nne. Mradi huu unataka kusisitiza na nirudie kusema tena

Mheshimiwa Waziri Jenista ulipopita ziara yako wananchi wa Nyamagana wanakushukuru sana, hata leo umemuachia Kaka yako Simbachawene naamini na yeye atakuja kuhakikisha hii awamu ya pili ya mradi wa *OPEC* ambao tunategemea tupate Shule ya Sekondari kule Kata ya Igoma, tunategemea tujenge barabara nyingine kule ya Mabatini - Kleruu na tunategemea tupate mradi mwingine kwenye eneo lingine…

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Mabula.

**MHE. STANSLAUS S. MABULA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa hiyo nachotaka kusema naunga mkono mapendekezo ya bajeti ya Mheshimiwa Waziri Mkuu lakini tusisitize kupeleka fedha kwenye miradi unganishi ili iweze kuwasaidia wananchi. Nakushukuru sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Stanslaus Mabula, Mheshimiwa Janejelly James Ntate atafuatiwa na Mheshimiwa Salma Rashid Kikwete, Mheshimiwa Iddi Kassim Iddi ajiandae.

**MHE. JANEJELLY J. NTATE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa nguvu za kusimama hapa kuongea, nampongeza Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. Samia Suluhu Hassan hasa kwa masuala aliyoyafanya hapa nchini. Afya, elimu, miundombinu, diplomasia, uchumi lakini mimi nitajilenga kwa aliyofanya kwa watumishi wa Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu ameamua kutoa kwa miaka miwili bilioni 26.3 kwa ajili ya ajira za watumishi nchini, pia akatoa bilioni 23.1 kwa ajili ya kupandisha vyeo Watumishi, zaidi ya hapo akaonesha uungwana wa kutoa msamaha kwa wenzetu waliopata janga la vyeti *fake,* kuachia bilioni 35.2 ziende kuwalipa hawa watumishi siyo jambo dogo ni jambo kubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa kwenye hotuba Wizara ya Kazi mmetuambia wamekwishalipa wahanga 11,896. Ni kweli hata mimi nimeenda kwenye Mifuko ya Jamii na Mheshimiwa Waziri nilikupa taarifa. Hata hivyo kuna 541 ambao bado hawajalipwa. Mifuko iliniambia hawajalipwa kwa sababu gani? Taasisi, Wizara na Idara za Serikali hazijapeleka viambatisho vyao na vielelezo vyao ili walipwe, kupitia kiti chako, hizi taasisi ambazo zinajua hazijapeleka vielelezo hivyo zipeleke ili hawa wahanga walipwe basi lengo la Mama Samia litimie.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninawapongeza mmekuja na *electronic* ya kuweza kutoa vibali vya ajira na mmefanya, maana mnasema mmetoa vibali vya ajira 8,000 lakini nina imani hivi ni vibali vy ajira vya wageni. Hivi kweli vyuo vyetu vinatoa wahitimu kila mwaka, kelele zetu hapa imekuwa kwamba hatuna ajira nchini, tunatoa ajira 8,000 kwa wageni! Hili tunaandaa bomu na bomu kubwa. Yawezekana Sheria inasema hivyo lakini ilikuwa ni wakati ule hatujapata wasomi wa kutosha. Kama ni Sheria ndiyo inatupeleka kule, basi tukaibadilishe hiyo Sheria ili vijana wetu wanaomaliza vyuo vikuu waweze kupata hizo ajira.*(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wameongelea kaguzi za kiafya za usalama kazini niwapomgeze, lakini mmefanya kwa asilimia 99 na mkapata ambao walikosea 173 na mkawachukulia hatua. Mngefanya kwa asilimia 100 mngepata wengi zaidi. Mimi kuna viwanda ambavyo nimevizungukia kwa Wilaya ya Temeke, kiwanda kile hauwezi kuweka watumishi. Sitovitaja majina lakini ninyi muende mkavizungukie muone. Watumishi wamefungiwa mule, hakuna hewa, hakuna nini, unauliza kisa ni nini? Wataibiwa. Pale kuna maisha ya watu na usalama wa watu, ninawaomba Wizara ya Kazi mkazunguke mfike asilimia 100 mtagundua mengi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile kuna suala la kisheria la uanzishwaji wa vyama vya wafanyakazi. Kifungu cha (9) cha Sheria ya Ajira na Mahusiano Kazini Na. 6 ya Mwaka 2004, inatoa haki ya wafanyakazi kuunda vyama vya wafanyakazi sehemu zao za kazi na hili ni haki ya Kikatiba. Utaratibu wa kutumia haki hiyo kwa wafanyakazi unasomwa kwenye Sheria Na. 6 ya Mwaka 2004 upo kwenye Kifungu cha 45, ambao unasema sisi tukishaanzisha chama chetu kwa miezi Sita tuna haki ya kuomba kwa Msajili wa Vyama vya Wafanyakazi ili atusajili lakini pale kumekuwa na mgogoro na Mheshimiwa Waziri tumeshaongea mara nyingi na wengine nawazuia wasiende sehemu zingine nawambia tutaongea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bahati nzuri Waziri ninakushukuru sana nilipopiga simu ulipokea kwa haraka sana lakini ukija kuuliza wanasema vyama vitakuwa vingi, si Sheria mmeitunga nyie kwamba vyama kila mmoja ana hiari wakiwa watu Kumi wanaweza wakaanzisha chama chao sehemu ya Kazi? Majibu yanakuwa vyama vitakuwa vingi sehemu za kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukienda kwenye Halmashauri unakuta kuna *TALGWU*, CWT na *TUGHE* sehemu moja ya Kazi. Tunachofanya vyama vikiwa zaidi ya kimoja, viwili, vitatu tunaangalia chenye *majority* ndicho kinaingia kufunga mkataba kuanzisha Baraza la Wafanyakazi. Kwa hiyo, hii haijakatazwa. Ninashauri tu wale walioomba kawapeni. Hivi mtu anaomba kuanzisha chama chake cha wafanyakazi ninyi mnasema lazima muulize chama kilichopo, nani atakubali kije chama kingine? Hakuna atakayekubali! Sasa mkisema mnawauliza hamtapata lakini mtakuwa mnataka kuibua migogoro ya vyama vya wafanyakazi na kwa watumishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilitegemea hapa walipomaliza ukagazi wa afya na usalama, mlitakiwa mtuwekee ukaguzi wa Mabaraza ya Wafanyakazi ambayo sasa hivi

yanakaguliwa na CAG lakini sina mahali ninapoona. Ninapozunguka kuna mahali bado Mabaraza ya Wafanyakazi hayafanyiki, na tunajua mabaraza ya wafanyakazi ndilo Bunge la wafanyakazi sehemu ya kazi, ndilo daraja la kujenga mahusianao. Sasa hapa hamjatuonesha kabisa. Sasa niwaombe wakati mnahitimisha mtuambie Mabaraza mangapi yamefanyika? Wangapi hawakufanya kihalali? Pia ni wangapi mmewachukulia hatua kama mlivyosema huku kwenye kukagua usalama na afya kazini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, niende sasa kwenye asilimia 10 ya Halmashauri. Asilimia 10 ya Halmashauri tumeamua Maafisa Maendeleo ndio wawe wafanyaji wa kuangalia mikopo ile na kuwapa watu mikopo Baraza la Madiwani wakishapitisha. Halmashauri zote nilizozunguka, kilio cha Maafisa Maendeleo wanasema waondolewe hiyo kazi, inawafanya wasitende kazi zao, kwanza wanaifanya bila utaalam. Pili, inawajengea mahusianao yasiyo sahihi kwa chini wakirudi kwenda kufanya kazi yao ambayo ni ya kuelimisha jamii, malezi, mahusiano sasa hawawezi kwenda kwa sababu wakienda wanaenda kudai ile mikopo waliyowapa wale wakopaji, kwa hiyo inawaweka kwenye wakati mgumu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ifike wakati sasa tuunde vitengo ambavyo vina wataalam, vina Maafisa Mikopo, vinavyo Wahasibu wa kuweza kuwapa hii mikopo. Yawezekana ndiyo maana hizi hela zinapotea, huyu anaetoa hii mikopo hana utaalam wowote wa ktoa hiyo mikopo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashauri tu kwenye Menejimenti ya Utumishi wa Umma. Mmefanya mengi sana Mheshimiwa Jenista nakupongeza na najua ambaye amechukua kiatu chako nae ataenda kufanya hivyo lakini kuna tatizo moja la kutokutoa taarifa. Wasaidizi wenu

hawatoi taarifa kumbe *communication is power!* Leo hii Mheshimiwa Rais alikubali kwenye bajeti ijayo hii tunayoijadili sasa iwekwe bajeti ya kufungua barua za *promotion* za 2016/2017 lakini nilikozunguka kote watumishi hawajui. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa nawauliza Maafisa Utumishi sasa kama watumishi wenyewe hawajui, rekodi mmezipata wapi za kuwafanyia bajeti hawa ambao walipewa barua zao wakanyang'anywa? Sasa ni jambo zuri Mheshimiwa Rais amefanya lakini hatulitangazi kuonekana ni suala zuri amelifanya likamjengea mahusiano yeye na watumishi. Ninaomba tukafanye hizo nyaraka zisiwe siri, nadhani nyaraka ikishatoka siyo siri. Zamani tulikuwa tunabandikiwa kwenye kuta mnasoma kilichotolewa kwa sababu ikishakuwa wamei – *undergrade* siyo siri tena lakini unakuta wanakaa nazo kama siri watumishi hawajui.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile kuna mikopo ambayo imepelekwa kwenye Manispaa zamani ilikuwa ni kwa Serikali Kuu, mikopo ambayo watumishi hukopeshwa kununua magari (vyombo vya usafiri) lakini hizi Milioni 300 zinazokwenda kwenye Manispaa watumishi hawajui. Unawambia Mheshimiwa Rais na ninyi amewaletea mikopo mkope mnunue vyombo vya usafiri wanaona kama uinawaletea nahau, hawajui! Sasa unamuuliza Mkurugenzi, unawauliza Maafisa Utumishi mnagawaje hizi hela kama Watumishi hawajui? Hizi kawaida yake hufanywa na Kamati inayoingizwa vyama vya wafanyakazi na Wawakilishi kila Idara kuweza kugawiana hizo hela lakini hawajui. Sasa kwa tafsiri iliyopo ina maana zinafika wakubwa wanagawiana wao mikopo, watumishi wa kawaida hawajui.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba hili iende ikafunguliwe. Baada ya hapo naunga hoja mkono. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Janejelly, Mheshimiwa Salma Rashid Kikwete atafuatiwa na Mheshimiwa Iddi Kassim Iddi Mheshimiwa Nusrat Shaban Hanje ajiandae.

**MHE. SALMA R. KIKWETE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa hii fursa. Sambamba na hilo naomba nikupongeze kwa kukalia hicho Kiti ili kuweza kuliongoza Bunge letu la Jamhuri ya Muungano wa Tanzanaia, Mwenyezi Mungu akubariki sana, *Allahu zidna I'lmi wa Ruzukna fahma.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo nichukue fursa hii kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri Mkuu Kassim Majaliwa Majaliwa, kwa hotuba yake nzuri ambayo ameitoa kwenye Bunge letu la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ni hotuba nzuri ni hotuba ambayo imeeleza mambo mengi ambayo yanawagusa Watanzania wote. Hongereni sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nimpongeze Mheshimiwa Rais wetu, Mama Samia Suluhu Hassan kwa kazi kubwa na nzuri anayoifanya ni kazi iliyotukuka, kazi hii anaifanya ndani ya nchi yetu ya Taifa letu la Tanzania na nje ya mipaka yetu Afrika na Duniani kote kwa ujumla. Hongera sana Mama tunakuamini, tunakupenda sana tuko bega kwa bega na wewe kuhakikisha kwamba kila dhamira uliyokuwa nayo tunakuunga mkono.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, katika Bunge hili au katika nchi yetu ya Tanzania hasa Wabunge ambao ndiyo wawakilishi wa wananchi, hakuna Mbunge yeyote humu ndani atakayesimama bila kueleza mazuri aliyoyafanya Mheshimiwa Rais katika Jimbo lake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukienda kwenye elimu amefanya makubwa, ukienda kwenye maji amefanya

makubwa, ukienda kwenye maji amefanya makubwa, ukienda kwenye barabara amefanya makubwa, ukienda kwenye michezo ndiyo funga kazi amefanya makubwa sana. Kwa hiyo, tunakupongeza sana Mama yetu Samia Suluhu Hassan. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa muktadha huo nataka kuchangia kwa kuanzia na eneo lifuatalo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, unyanyasaji wa watoto, ndoa za jinsia moja, malezi na makuzi ya watoto wetu. Kwa nini nimeanzia katika eneo hili? Nina sababu kubwa ya msingi. Bila watoto hakuna Taifa, watoto ndiyo Taifa letu na ndio tegemeo letu. Watoto ndiyo baraka ambayo Mwenyezi Mungu ametupatia wanadamu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tutasema Mama amefanya kila kitu katika Taifa letu, shule nani anatakiwa aende? Anatakiwa aende Mtoto! Hospitali watoto wanatakiwa waende, barabara watoto wanatakiwa wazitumie, kila kitu kinatutegemea sisi na kinawategemea watoto hawa. Leo sisi ni Wabunge ambao tuko humu ndani, tufikirie kwamba una mtoto wako umemuacha huko nyumbani unaambiwa mtoto huyu sasa hivi ameingia kwenye kulawitiwa, kama mzazi kama mlezi unajisikiaje?

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumepewa dhamana ya kuwalinda, kuwatetea na kuwasemea. Kwenye hili ni jambo ambalo hatukubaliani nalo kama Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwenye jambo hili tusiletewe vitu kutoka huko, sisi kama Watanzania tunao utamaduni, mila na desturi zetu ambazo ndizo zinatuongoza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa muktadha huu Wabunge hili ni jambo la kulaaniwa. Ni lazima kama Wabunge tuwe na azimio la kulikataa hili jambo sisi ndiyo waamuzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, inaniuma sana na Watanzania inawauma sana. Nikiwa Mke wa Rais siyo sasa hivi nimeondoka kwenye kuwa Mke wa Rais isipokuwa sasa hivi ni Mstaafu, nilikuwa na Taasisi yangu na inaendelea Taasisi ya Wanawake na Maendeleo kauli mbiu ilikuwa 'Mtoto wa Mwenzio ni Mwanao'. Maana yake ni kwamba Mtoto wa Mwenzio akiwa mwanao utamtendea vitendo viovu? Huwezi kumtendea, utamlinda na katika kumlinda kule utamtengenezea maisha ya baadae. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo dunia kuna baadhi ya watu wanatengeneza utaratibu wa kuzaa watoto wawili. Sisi tulikuwa tunazaa watoto wengi, dunia hiyo hiyo leo wanatuletea ndoa za jinsia moja, hivi tutakuwa na kizazi sisi? Mwanaume akishafanyiwa kitendo cha namna ile basi hawezi kufanya kazi, atapata wapi watoto? Hawezi kupata watoto. Kwa muktadha huo ni lazima jambo hili tulikemee vikali kadri inavyowezekana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuyasema hayo kwa sababu wenzangu wengi wamesema na mimi niishie hapo. Hili jambo hatulitaki sehemu yoyote nitakayosimamishwa duniani nitasema hili jambo silitaki na silitaki kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu elimu, ninampongeza sana Mheshimiwa Rais. Mheshimiwa Waziri Mkuu wakati anatoa taarifa yake alizungumzia suala la shule 26. Miongoni mwa shule 26 shule 10 ziko tayari na ziko ndani ya Mikoa 10. Mikoa hiyo ni pamoja na Mkoa wa Dar es Salaam, Mkoa wa Lindi, Mkoa wa Morogoro, Mkoa wa Pwani na Mikoa mingine ambayo inafanya idadi kuwa shule 10.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachopenda kusema shule hizi ziko kumi na kila shule ni bilioni nne. shule hizi ni pesa za walipakodi wa nchi nchi hii ninachokiomba au ninachoshauri au kabla ya hapo mwezi wa saba mwaka huu zinaanza kuingiza wanafunzi wa kidato cha tano lakini katika

uwasilishaji sikuona hata shule moja ambayo tungeona tu kwa mfano wakati wanatoa taarifa wanaonesha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba, nilikuwa kwenye Kamati ya Kudumu na Maendelaeo ya Jamii, sasa hivi niko katika kamati nyingine. Tulikuwa na lengo la kwenda kuzitembelea shule hizi hatujaweza kuzitembelea. Siamini kama kuna kamati imekwenda kuzitembelea. Ushauri wangu kamati hatawakiwa watu wachache waende wakazitembelee shule hizi kabla ya mwezi wa saba kuona je zina ubora? Ubora upo, je inawezekana mwezi wa saba au laa! Ushauri wangu waende wakazitembelee

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pamoja na hizi shule tunaambiwa zimeisha ni kweli, mimi kwenye jimbo langu shule hii ipo ndani ya Jimbo langu la Mchinga. Ninachoshauri waweke ukuta yaani uzio kwa ajili ya kuwalinda mabinti hawa kwa sababu tunataka wasome vizuri na mabinti hawa ni mabinti wenye vipaji maalum lakini kwenye eneo la sayansi tunawahitaji wanasayansi wengi zaidi katika Taifa letu la Tanzania kwe sababu hii ni Tanzania ya Viwanda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo nataka nizungumze kidogo kwenye suala la uvuvi, na uvuvi huu unawahusu sana vijana, wanaovua ni vijana, Ukanda wa Pwani una vijana wengi zaidi hata kwenye Jimbo langu la Mchinga kuna upande mzuri haujawahi kuokea nafikiri ni eneo la kwanza hata katika nchi yetu ya Tanzania, kuna *beach* nzuri sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachoomba au ninachoshauri hao vijana uchumi wao mkubwa wanategemea Bahari, kule kuna Bahari hakuna mito, sasa vijana hawa wakopeshwe aidha maboti kwa ajili ya kujenga uchumi wao kwa ajili ya kipato chao, na si maboti tu na vitendea kazi vingine wakopeshwe watakuwa na uwezo wa kulipa kwa sababu watakwenda eneo la mbali kutafuta riziki

lakini ukiwa na kile kimtumbwi hauendi mbali na unachokipata siyo kikubwa huo ndio ushauri wangu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho nataka nizungumzie maliasili na utalii nilisimama hapa nikazungumzia suala la kuongezeka kwa tembo, na nilichangia hiyo hoja kuhusu tembo nikasema tembo ni wazuri sana tembo ni Wanyama ambao wanatuongeza fedha za kigeni tembo hao. Lakini watu wengi wanaopitiwa na tembo tembo siyo rafiki, tembo hii njaa ambayo sasa hivi inazungumzwa tumeletewa mahindi, ni kwa sababu maeneo mengine ni kwa sababu ya tembo wanakula vyakula. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo tunaishukuru Serikali kwa kutuletea mahindi kupunguza ile njaa. nitakuwa ni mchoyo wa fadhila nisipoweza kuipongeza Serikali, Serikali imenitendea mambo mengi makubwa na mazuri miongoni ni kwenye hilohilo la hao Wanyama tembo hao, niliwaomba gari, wameniletea gari jipya Jimbo la Mchinga, niliwaomba kile kituo ambacho maaskari watakaa kwa ajili ya kuwadhibiti tembo na kuwafukuza wamenijengea kituo kizuri ajabu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo wakati huo kulikuwa na maaskari wawili nikasema maaskari wawili watawezaje kudhibiti tembo 30 sasa hivi wameniletea maaskari zaidi ya 20. Kwa hiyo, ninawashukuru sana. Lakini sambamba na hilo kwa wale ambao watanzania wale ambao wanapitiwa na yale maeneo ambayo tembo wapo wasaidieni watanzania wanashida tena shida yao siyo ndogo shida kubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuyasema hayo niwashukuruni sana nimshukuru sana Mheshimiwa Rais nina mambo mengi nitakuja kuyasema nitakapo changia Wizara nyingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Salma Kikwete nimuite Mheshimiwa Iddi Kassim Iddi atafuatiwa na Mheshimiwa Nusrat Shaban Hanje Mheshimiwa Aida Khenan ajiandae.

**MHE. IDD K. IDDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. kwanza nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema kwa kuniweesha kunipa afya njema leo kusimama katika Bunge hili Tukufu na mimi leo kuchangia kwenye hotuba ya Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Rais wetu mpendwa Mama Daktari Samia Suluhu Hassan kwa kazi kubwa anayoendelea kuifanya kwa nchi yetu hii ya Tanzania. Nitakuwa mchoyo wa fadhila kama sitampongeza Mheshimiwa Mama Daktari Samia Suluhu Hassan kwa fedha nyingi ambazo ametutunuku wana Msalala. Mama Daktari Samia Suluhu Hassan ametupatia fedha nyingi katika miradi mbalimbali ikiwemo Huduma za Afya, barabara, umeme, maji, na maeneo mengine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukianza na afya. Mama Samia Suluhu Hassan ametupatia fedha ambazo zimetupelekea kujenga kituo cha afya katika kata ya isaka kiasi cha shilingi milioni 500 hajaishia hapo akatuongeza fedha nyingine kujenga Kituo cha Afya Kata ya Morogoro milioni 500, hajaishia hapo ametupatia fedha nyingine kujenga Kituo cha Afya Kata ya Burige milioni 500, hajaishia hapo akatupatia fedha nyingine milioni 400 kujenga Kituo cha Afya Kata ya Segese. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulikuwa na uhaba wa zahanati katika maeneo mbalimbali ya maboma lakini Mama Daktari Samia Suluhu Hassan ametupatia fedha kwa

ajili ya kukamilisha maboma zaidi ya 18 ya zahanati ambayo yote yamekamilika mpaka sasa hivi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambambamba na hilo, ili kuhakikisha ya kwamba tunaondoa upungufu wa watumishi katika maeneo hayo Mama Daktari Samia Suluhu Hassan ametupatia fedha ambayzo fedha hizo tumeenda kujenga chuo cha *nursing* na sasa kipo katika hatua ya mwisho ili kianze kutoa hudumahajaishia hapo ametupatia fedha kwenye sekta ya barabara. Mambo mengi sana kwa niaba ya wana Msalala nichukue fursa hii kumpongeza Mama Daktari Samia Suluhu Hassan kwa wema aliotutendea sisi wana Msalala. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niendelee kumpongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa kazi kubwa ambayo anaendelea kuifanya lakini kwa hotuba hii ya leo ambayo amewasilisha hapa bungeni. Katika hotuba hii ya Waziri Mkuu imeanisha kwamba ataenda kuboresha miundombinu ya barabara na niseme katika suala langu la barabara hasa niliouliza hapa asubuhi kwenye swali la nyongeza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna fedha ambazo zimetolewa kwa ajili ya ujenzi wa barabara inayotoka Buliankhulu inaenda mpaka Kahama lakini pia barabara hiyo inaunganisha kutoka Ilogi kwenda mpaka Geita lakini hivyohivyo inatoka hapo inaenda Nyang'wale inaenda mpaka kuunganisha daraja ambalo linajengwa la Kigogo Busisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara hii na leo niizungumzie kwa uchungu mkubwa sana kwa sababu Mheshimiwa Naibu Waziri leo wakati ananipa majibu yake pia alinipa majibu ambayo hayakuridhisha kabisa. Fedha hizi Mama Dkt. Samia Suluhu Hassan ameidhinisha kiasi cha Shilingi dola milioni 40, takribani bilioni karibia bilioni 100 kwa

ajili ya ujenzi wa barabara hii na fedha hii ipo na toka mwaka jana barabara hii ilikuwa ianze kujengwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na kuwa na milolongo mingi ya manunuzi, vikao vingi ambavyo havikamilishi ajenda zao bado mpaka tunavyozungumza hivi hakuna mpaka leo tunaambiwa bado makabrasha yanaandaliwa ili mkandarasi watangaze tenda hiyo. Sasa niseme fedha hii tumepatiwa na Mgodi wa Bulyankhulu na niwapongeze sana mgodi wa Bulyankhulu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mahusiano ya sisi tunaoishi karibu na migodi na wananchi yalikuwa ni mabaya mno lakini niwapongeze sana Mgodi wa *Barrick* na hasa kupitia maafisa wao wa mahusiano akiwemo Agapiti anafanya kazi kubwa sana. Wameona kuna haja ya kutupa fedha ili tujenge barabara hii kwa kiwango cha lami ili tuondoe vumbi ambayo itapitika kila leo na makinikia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi wanaathirika na vumbi, wameamua kutenga fedha kwa ajili ya kujenga barabara hii, lakini leo kumegeuka sasa Wizara ya Ujenzi kumegeuka kuwa ni sehemu ya kutafuta sijui ni nini lakini kila siku ni vikao wameanza vikao vya kwanza tumekaa kila kata tukamaliza wakaja wakafanya tathmini wamemaliza, wamerudi tena wanasema wanataka warudie wafanye *review* ya upembuzi yakinifu wamemaliza na wenyewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hii hawataki kutangaza Barabara hii na fedha ipo, mgodi huo madini yakipotea tutapata wapi fedha? Tumepewa fedha za wahisani tujenge barabara Mheshimiwa Naibu Waziri unakuja kusimama hapa majibu rahisi kabisa mpaka leo hamjatangaza nini ambacho kimewafanya ninyi msitangaze barabara hii? Fedha zipo siyo kwamba hazipo hata leo mkileta *certificate* wanalipa wale watu. Fedha zipo *cash* kwa nini hamjengi Barabara hii wananchi wanaendelea kuumia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Barabara hii ni nguzo ya uchumi katika kuunganisha Geita toka Mkoa wa Geita mpaka shinyanga lakini leo nimezungumza hapa nikasema kahama ndio kitovu cha uchumi kanda ya ziwa. Unapozungumzia kanda ya ziwa huwezi kuiacha Kahama. Kuna wafanyabiashara wakubwa wanahitaji kusafirisha watu wanahitaji kuleta mali kutoka geita wanahitajikuleta mali kutoka Kagera na maeneo mengine. Barabara hii fedha zipo leo mtatuambia nini nani kachelewesha? Leo mnaniambia dakika ya mwisho naulizia wanabadilishana kukaa vikao naambiwa leo wameitana tena wanataka kwenda kukaa Dar es salaam kikao cha nini? kila siku mnakaa vikao kama vikao vya harusi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, inauma, vikao vimekuwa ni vingi sana. Vikao vile vinatumia posho fedha ile itajenga Barabara lini?  Fedha ipo wananchi wanaumia niombe Mheshimiwa Waziri Mkuu atakaposimama hapa kufanya *windup* ya hili atueleze ni lini hasa barabara hii itaanza kujengwa kwa sababu fedha zipo hakuna kinachoshindikana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, inauma sana leo nimezungumza kwa uchungu sana kwa sababu ninaona kuna uzembe mkubwa unafanyika kwenye maeneo haya hasa Wizara ya Ujenzi. Barabara nyingi ukiangalia, kuna barabara zinachelewa kujengwa na ukiuliza tatizo ni nini wanakuambia tatizo ni eidha ni hatua za manunuzi kwa nini tusizipitie upya hizi hatua za manunuzi? Ukiuliza unaambiwa bado kuna changamoto ya kupata *tax exemption* kwa nini hawa watu wa *TRA* wasikae pamoja na watu wa ujenzi wakaorodhesha barabara zote kama kikwazo kama ndio kupewa msamaha wa kodi wangalie ni namna gani wanaweza wakafanya ili kutoa msamaha wa kodi haraka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, inauma sana kuona watendaji wanakuwa wazembe kiasi hiki. Mheshimiwa Rais anapambana kutafuta fedha, anaenda nje kutafuta fedha anatuletea fedha, anajitoa kuzungumza na wahisani mbalimbali leo watu wanakuja wanataka kutusaidia lakini watendaji wanamwangusha Mheshimiwa Rais. Ni katika shilingi nitakapokuja kuchangia Wizara nitashika mshahara wa Mheshimiwa Waziri mpaka atuambie ni lini barabara hii itaanza ujenzi kwa sababu fedha hizo tunazo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumze pia kwenye suala zima la *TARURA* amezungumza Mbunge mwenzangu hapa. Wilaya ya Kahama ndio wilaya kubwa inawezekana kuliko wilaya zote hapa Tanzania. Ukiangalia Mkoa wa Shinyanga ndio unaweza kuwa ni mkoa mkubwa lakini una wilaya chache kuliko zote hapa Tanzania. Mkoa wa Shinyanga una wilaya tatu tu lakini una halmashauri sita, sasa niombe *TRA* wamefungua Mkoa wa Kikodi Kahama, watu wa amdini wamefungua Mkoa wa Kimadini Kahama, niombe kwa nini hawa watu wa *TARURA* nao wasifungue Mkoa wa Ki-*TARURA* Kahama? Lakini pia tulikuwa na hawa Mameneja kwenye halmashauri zetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wilaya ya Kahama ina vijiji zaidi ya mia tatu na ishirini na kitu, leo kama Mkuu wa Wilaya akianza kutembelea kila Kijiji maana yake ni kwamba mwaka mzima yeye asifanye shughuli nyingine wala kwenda likizo anatembelea tu vijiji. Kwa nini hawa Mameneja wasirudishwe ili waweze kutoa huduma?

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hii mvua zinaendelea kunyesha tunapokea malalamiko kwenye maeneo yale utaona barabara zinakatika, watu wanataka kurekebisha barabara lakini ukiuliza hatua za manunuzi hivi haya manunuzi hamuwezi mkayaleta hapa tukayapitia tukaona njia rahisi ya kurekebisha? Leo utaanza kuona tunapitisha bajeti mwezi wa saba mwezi saba akaunti zimefungwa

mfumo bado tunaenda tunatangaza tenda, tunatangaza tenda hatua za manunuzi, manunuzi, manunuzi, mpaka mkandarasi anaenda *site* mwezi wa pili mvua zinanyesha barabara haitengenezwi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hii Mama Dkt. Samia Suluhu Hassan anatafuta fedha nyingi anatuletea, changamoto siyo fedha kwenye maeneo yetu kwa sasa fedha zipo lakini changamoto utaambiwa tulitangaza barabara hii mkandarasi hakupatikana, hakupatikana alienda wapi? Wanasema tumetangaza barabara hii hatua za manunuzi bado, bado kivipi? Wakati meza zipo? Niombe sana Wizara ya TAMISEMI hebu oneni namna ya kuweza kuona namna ya kurudisha mfumo ambao uliokuwepo wa Mameneja Wilaya ya Kahama ni wilaya kubwa mno.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyohivyo niendelee kuomba ikiwezekana basi tuone namna ya kugawa utawala mtuongezee hizi halmashauri, Halmashauri yangu ya Msalala, Halmashauri ya Usheto na Halamashauri ya Manispaa ya Kahama hizi zote zinajitegemea kiuchumi na uchumi wao ni mzuri, kwa nini tusipatiwe wilaya kila sehemu tukajitegemea? Kwa sababu halmashauri yangu ni halmashauri lakini ukilinganisha na wilaya zingine inawezekana kiuchumi Halmashauri ya Wilaya ya Msalala ikawa iko vizuri kuliko wilaya zingine ambazo zinaendelea hasa niazoziona za Jirani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimezungumza sana kwenye suala zima la barabara naumia sana, kwenye umeme nitakuja nizungumze kwenye Wizara ya umeme lakini niombe hii barabara ni changamoto kubwa sana na narudia tena kwa sababu ni barabara ambayo kuna uzembe na ikiwezekama watu wawajibike kwenye hili, nani amekwamisha? Nani kashikilia? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, inaniumiza sana kuona fedha tunazo kwenye maeneo mengine wanalia kila siku Mheshimiwa Naibu Waziri anatuambia ikipatikana fedha Serikali itajenga sasa fedha imepatikana kwa nini hamjengi? Kama fedha ikipatikana leo ipo Mheshimiwa Naibu Waziri na Mheshimiwa Waziri wa Wizara hii na Katibu Mkuu niwaombe sana punguzeni vikao. Ikiwezekana *CAG* nimuombe kwenye ripoti inayokuja achunguze hivyo vikao vinavyo kaa kaa hivyo vikao vinatumia fedha kutoka mfuko gani? Kwa sababu vikao vimekuwa vingi haviishi kutangaza barabara mbona barabara zingine hazina vikao vingi kama hii barabara? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi tunaozalisha dhahabu ukiangalia mgodi wa Buliankhulu na jimbo langu la Msalala ndio jimbo ambalo linachangia kwa kiasi kikubwa sana kwenye mfuko wa taifa. Leo hii utaona kwenye wizara ya madini tunalipa *reality* asilimia saba na niendelee kuomba Mheshimiwa Waziri yupo hapa ananisikia Mheshimiwa Waziri Mkuu nikuombe sana watu tunaotoka kwenye maeneo ya madini maisha yetu ni duni, hayafanani na vile ambavyo tunazalisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niombe ikiwezekana kwenye asilimia saba ambayo tunalipa mrabaha asilimia saba ambayo makampuni yanalipa mrabaha niombe asilimia mbili iweze kubaki kwenye maeneo hayo ili tuweze kujenga miundombinu yetu wenyewe kwenye maeneo yale bila kutegemea fedha kutoka Serikali kuu, uwezo huo tunao kwa sababu fedha zipo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeongea kwa uchungu sana nafikiri nisiharibu niishie hapo lakini niombe na niombe nitashika shilingi kama barabara hii haitaanza kujengwa kwa sababu fedha zipo, ahsante *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa namwita Mheshimiwa Nusrat Shaban Hanje atafuatiwa na Mheshimiwa Aida Khenan Mheshimiwa Seif Gulamali ajiandae.

**MHE. NUSRAT S. HANJE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia Ofisi ya Mheshimiwa Waziri Mkuu na nitachangia fungu 65, Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Vijana, Ajira na Watu wenye Ulemavu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na majukumu ya msingi ya kuanzisha Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Vijana, Ajira na Watu wenye Ulemavu. Miongoni mwa majukumu ya msingi ilikuwa ni kuandaa, kuratibu na kusimamia sera kanuni sheria na miongozo mbalimbali ya kitaifa na kimataifa yanayohusiana na masuala ya maendeleo ya vijana, kazi ajira, watu wenye ulemavu na hifadhi ya jamii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu randama na *document* zote zinazohusiana na Ofisi hii upande wa maendeleo ya vijana wamezungumzia shughuli ambazo zinaitwa shughuli za maendeleo ya vijana ni pamoja na wiki ya vijana kitaifa, pamoja na kumbukumbu ya Baba wa Taifa lakini na Mbio za Mwenge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, haitoshi kwa sababu ukiangalia *Integrated Labour Force Survey Review* ya mwaka 2021 utaona vijana ni asilimia 57 ya *labour force* ya nchi yetu. Haitoshi kuzungumza vijana kwa nusu *paragraph* kwa kutaja hizi ndio shughuli zao ambazo zinaitwa shughuli za maendeleo ya vijana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, zipo changamoto nyingi hatuwezi kuacha kuzungumza tatizo la ajira lakini siyo kwa ujumla wake ni tatizo la ajira kwa vijana kwa sababu ndio *labour force*, lakini pia tatizo la ajira kwa vijana wasomi hatuwezi kuacha kuzungumza hilo. Ukiangalia *rate* za

*graduate unemployment* zinakua kila mwaka na tunatengeneza bomu bila kulielezea tunalitatua vipi, hatuwezi kuzungumza jumla jumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ninasikitika sana kwa sababu hawa wanaozungumza hapa ambao ndio wanaoshiriki kwenye wiki ya vijana kitaifa, wanaoshiriki katika mbio za mwenge, na wanaoshiriki katika maonesho na kujitolea na midahalo ndio Ofisi ya Waziri Mkuu inazungumza kwamba ndio shughuli za vijana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bahati mbaya sana hata hicho kimfuko cha vijana kidogo ambacho kimetengewa bilioni moja. Ilitengwa bilioni moja mwaka 2022/2023 na haijapelekwa mpaka sasa hivi imepelekwa ziro haijapelekwa hata senti moja lakini hata mwaka wa fedha uliopita ambao ndio tuna malizia sasa hivi hata *the previous year* bado walipelekewa milioni 200 na wakaambiwa hawana vigezo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa Ofisi ya Waziri Mkuu ina programu za kuwajengea uwezo vijana, uanagenzi na vitalu nyumba *vinaus* na wana - *graduate* kwa *qualifications* za Ofisi za Waziri. Hata hawa ambao mmewa-*train* wenyewe hawana vigezo kiasi kwamba hamuwapi hizo pesa. Vijana hawatuelewi kwa sababu hawatuelewi tukisema wamekosa vigezo kwa sababu wana *qualify* kwa *qualifications* ambazo tumeziweka sisi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hizi ambazo mmezungumza lakini kuna changamoto nyingine. Kwa mfano vijana hawana jukwaa la kukutana ambako wanazungumza mambo yao, lakini pia vijana hawana sera ambayo inaendana na mabadiliko ya sasa hivi. Mabadiliko ya sayansi na teknolojia, masuala mbalimbali ambayo yanaendelea kwa sababu sera yetu ya vijana ni ya mwaka 2007 ambayo ina miaka 16 na iko *outdated*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiingiza hii taarifa kwenye *tablet* yako, ukiingiza taarifa zote zinazosomwa ukaandika sera ya maendeleo ya vijana uka-*enter* hautapata *information* yoyote. Huwezi kuzungumza maendeleo ya vijana usizungumze sera yao ambayo ni *outdated*, haiwezekani. Kwa sababu sera ndiyo inatoa muongozo na inatoa utaratibu wa namna ambavyo masuala ya vijana *updated* kutokana na sayansi na teknolojia na mambo yanavyoendelea, kwa sababu inawezekana nyie mnazungumza lugha nyingine na vijana wanazungumza lugha nyingine, kwa sababu hamzungumzi lugha moja sera haipo *updated*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kwa uchache sana naomba nizungumze kuhusiana na jukwaa la vijana kukutania. Mwaka 2015 Bunge hili lilitunga Sheria namba 12 ilioitwa Sheria ya Baraza la Vijana la Taifa ambayo mpaka leo ni miaka nane tangu tumetunga sheria. Tumetumia rasilimali za Serikali kutunga sheria ambayo haijawahi kutekelezwa tuna kigugumizi, lakini mpaka leo imepitia mwaka moja na miezi tisa tangu Mheshimiwa Rais atoe maelezo ya mwisho alivyokutana na vijana Mkoa wa Mwanza, Mwezi wa Sita 2021. Akaiambia Wizara inayohusika na masuala ya vijana waangalie nini kinaendelea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kama hiyo haitoshi, naomba nisome Sera ya Vijana ya Mwaka 1996, kwa kunukuu naomba ninukuu. Sera inaelezea sura ya 4, Ibara ndogo 4 (1) (8) inaelezea kwamba kuwe na mtandao wa kupeana na kubadilishana habari kuhusu shughuli za maendeleo ya vijana, hiyo ni Sera ya Vijana ya Mwaka 1996. Sera ya Maendeleo ya Vijana Mwaka 2007 inatamka katika tamko la sera inasema Serikali itasimamia zoezi la kuundwa kwa baraza la vijana la Taifa na kutengeneza kanuni za usimamizi wa shughuli za baraza. Hiyo ni sera ya vijana, lakini *African Youth Charter* 2007 Ibara ya 11 inasema nchi wanachama watapaswa kuhakikisha ushiriki wa vijana katika Bunge na

vyombo vingine vya maamuzi ipasavyo kama sheria inavyoelekeza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kuratibu uanzishwaji au uimarishwaji wa majukwaa kwa ajili ya vijana kushiriki kufanya maamuzi ngazi ya chini kitaifa, kikanda na katika ngazi mbalimbali za kimataifa za kiutawala, lakini Katiba inayopendekezwa hii sio muhimu kwa sababu haijapitishwa; lakini pia Katiba inayopendekezwa *well enough* vijana walitoa mapendekezo kwamba jambo la vijana au baraza la vijana liingie kwenye katiba ya mapendekezo na yenyewe ilisema Serikali itaanzisha Baraza la Vijana la Taifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini tamko la Mheshimiwa Waziri Mkuu mwaka 2016 wakati anasoma Bajeti ya Serikali mwaka 2016/2017 alisema katika hotuba yake "ili kuimarisha dhana ya ushiriki na ushirikishwaji wa vijana katika shughuli za maendeleo, Bunge la Kumi lilitunga sheria namba 12 ya Baraza la Vijana la Taifa ya Mwaka 2015, napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kwamba sasa kanuni za utekelezaji wa sheria hiyo zimekamilika. Hivyo katika mwaka 2016/2017 Serikali itaendelea kuratibu uanzishwaji wa Baraza la Vijana la Taifa na kuhimiza ushiriki na ni uanzishaji na uimarishaji wa *SACCOS* za vijana katika halmashauri zote ili vijana waweze kushiri katika shughuli za maendeleo". *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hayo yote kuna kigugumizi gani kwenye Serikali kuhusiana na baraza, tunaenda kwenye mikutano ya nje ya nchi, nchi za wenzetu vijana wanaowakilisha vyombo vya vijana kwenye nchi zao wanakaa. Sisi kila mwaka tunasema tupo kwenye mchakato, tupo kwenye mchakato mpaka leo tupo kwenye mchakato, walikuwa vijana kipindi hiko wameshazeeka bado hatupati. Ninajua kuna vitu ambavyo vinasabaisha kwa nini hatuleti baraza, lakini ukisoma Sheria ya Vijana ina *solution* kwamba chombo kitakuwa cha kisiasa? Kuna utaratibu wa kinidhamu

kwamba chombo kitakuwa hakina pesa? Sheria inasema vijana wataweza kupata ruzuku. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kiufupi ninatamani kujua nini kinaendelea kuhusiana na Sera ya Vijana ya Taifa, Sera ya Maendeleo ya Vijana lakini pia Baraza la Vijana la Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho kabisa nimalizie, Mwenge wa Uhuru; kwanza ni miongoni mwa *champions* wa hicho kwa uzalendo na kwa ukubwa wa Mwenge wa Uhuru. Nilikuwa miongoni mwa watu waliotoa maoni kwamba mwenge uingie katika urithi wa utamaduni wa dunia usioshikika; na tunaendelea ku-*champion* mwenye uingie pale na tunaheshimu mno, lakini Mwenge wa Uhuru *was a political instrument design to propagates brotherhood* and *self-reliance brotherhood philosophy*. Ulikuwa ni nyezo ya kisiasa kupropagandisha falsafa ya ujamaa na kujitegemea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo tunazungumzia Diplomasia ya Uchumi na tumesema nchi imefunguka bado tunakimbiza mwenge tena *very unfortunately*. Nakuomba nisome barua ambayo inatoka kwa Mkurugenzi wa Mji wa Ifakara. "Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Halmashauri ya Mji wa Ifakara, Mchango katika kufanikisha Shughuli za Mwenge wa Uhuru Mwaka 2023". Nitasoma *para* ya pili, "kwa barua hii napenda kukujulisha kuwa unapaswa kuhamisha walimu katika shule yako kufahamu falsafa ya Mwenge wa Uhuru ili kushiriki na kuchangia fedha za kufanikisha shughuli ya Mwenge wa Uhuru 2023 kwa mchanganuo wa shilingi 50,000 kwa wakuu wa shule na 5,000 kwa waalimu wa kawaida", sasa mwenge? *Look at this! (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaenda vizuri, nchi imefunguka Mama anafanya mambo makubwa wasaidizi wake wapo ambao wanamsaidia, *what is this?* Hii inawashushia *credit*, mbona sisi hatujawahi kuchangishwa

hapa Bungeni hata 100 kuchangia mwenge, sijawahi kuona barua kwa sababu na sisi tuletewe Mwenge wa Uhuru, Waheshimiwa Wabunge kupitia Bunge lako changieni milioni kumi kumi tukakimbize mwenge. Mimi nafikiri sasa kama ni msingi…

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU (MHE. PASCHAL P. KATAMBI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MHE. NUSRAT S. HANJE**: Mheshimiwa Mwenyekiti, … ni kitu cha msingi the *you don't have to do this, why are you doing this?*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Nusrat kuna taarifa. Mheshimiwa Naibu Waziri.

**T A A R I F A**

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU (MHE. PASCHAL P. KATAMBI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru kwa nafasi hii. Pamoja na mchango mzuri wa Mheshimiwa Mbunge, naomba kumpa taarifa kwamba katika suala la Mwenge wa Uhuru, kwanza ni tunu ya Kitaifa ambayo mwenge ukizungumzia suala la mwenge ni falsafa. Usione kama kile chombo, falsafa inayobeba ni kuhusiana na Utanzania wetu, Utaifa wetu, uzalendo wetu, mafunzo kwa ajili ya vijana lakini zaidi ya hapo ni chombo ambacho kinapita nchi nzima kuangazia na kumulika kwa sasa kuangalia *value for money* katika miradi ya maendeleo ambayo fedha nyingi zinaenda kwa ajili ya Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini zaidi ya hapo masuala ya uadilifu yanaangaziwa na mwenge. Sasa ukisema kuhusiana na suala la michango, michango ni hiari ni uzalendo wa watu hakuna utaratibu wala kanuni zinazoelekeza watu

wachangishwe fedha kupitia mwenge wa uhuru. Kwa hiyo, kama aliandika huyo Mkurugenzi ni kwa utashi wake lakini sio kwa utaratibu ambao upo kwa mujibu wa sheria na utaratibu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini zaidi ya hapo nipende pia kutoa taarifa kuna eneo amelieleza mchango ni mzuri, lakini si vyema sana ikienda tofauti huko nje, kwamba katika fedha alizosema za vijana ile bilioni moja katika mwaka huo wa fedha tulitoa bilioni 1.8 ambayo imekwenda na sasa tayari Wizara ya Fedha imeji-*commit* kwamba tutapata fedha hizo awamu ya pili ya mwaka ule wa fedha kutoa ile bilioni 1 kwa ajili ya vijana hawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, na kuhusu masuala ya vijana kwa ujumla, hata bilioni tisa nyingine zilitolewa kwa ajili ya kutoa mafunzo ya ukuzaji ujuzi kwa ajili ya vijana. Kwa hiyo, Mheshimiwa Rais, Mama Samia Suluhu Hassan, yupo makini na vijana wake, anajua wakati gani anawapa fedha na wakati gani anatengeneza utaratibu wa kuwasaidia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vijana sisi ni kipaumbele katika Taifa hili na Mama amesema ukichezea vijana wake basi utaweza kumuona kwenye sura zote. Mheshimiwa Rais anawaangalia vijana, nikuhakikishie Mheshimiwa Hanje hata wewe ni mmoja wa vijana ambao Mheshimiwa Rais anakuangalia kwa jicho kama kiongozi mzuri wa baadaye. Tuendeleze uzalendo wetu, tutunze Tunu zetu za Taifa na tujisimamie katika kuhakikisha kwamba Tanzania yetu tunabaki kuwa salama, ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Nusrat unaikubali taarifa.

**MHE. NUSRAT S. HANJE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, barua imeandikwa unapaswa kuchangia na kama ni uzalendo

tunatakiwa tuanze sisi kwa sababu mimi mwenyewe ni mzalendo. Tuanze humu tuchange milioni 20, milioni Hamsini Hamsini. Mwenge unaenda kumwaga gongo. Kuna Kamati ya Bunge inaenda kukagua miradi, tuna *CAG* anakagua miradi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naendelea…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ishaisha malizia. Ahsante sana, Mheshimiwa Nusrat. Mheshimiwa Aida Khenani atafuatiwa na Mheshimiwa Seif Gulamali, Mheshimiwa Cosato Chumi ajiandae.

**MHE. AIDA J. KHENANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa nafasi niweze kuchangia Hotuba hii ya Waziri Mkuu iliopo mbele yetu, lakini niombe Mawaziri wanapokuwa wanatoa taarifa wakati wana muda wa kujibu wanatuchukulia muda wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kwanza kwa kutoa pole kwa wananchi wangu wa Kata ya Kilando na Itete ambao wamepata mafuriko nikiwa hapa, zaidi ya kaya 500 na hatujui leo wanachi wangu watalala wapi. Niwape pole sana wananchi wangu lakini nianzie kwenye hilo hilo. Kumekuwa na uzito sana kwenye Ofisi ya Waziri Mkuu kunapotokea majanga kuchukua hatua. Hilo jambo limekaa kinadharia sana kwenye Ofisi ya Waziri Mkuu na ni vizuri kama Bunge tukajua utaratibu mwingine ambao unatumika inapotokea majanga na namna ya kuwasaidia Watanzania, kuliko ambavyo ipo sasa kwenye maandishi lakini kwenye utekelezaji haipo ni sifuri kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nianze na kwenye sekta za uzalishaji. Sekta za uzalishaji nitajikita kwanza kwenye suala la uvuvi. Mkoa wetu wa Rukwa uvuvi kwetu ndio

uchumi na kilimo ni uchumi. Kwenye sekta pekee yake ya uvuvi ukitilitazama Ziwa Tanganyika tuna-*share* zaidi ya nchi tatu lakini taarifa tulizonazo mpaka sasa ni kwamba wanategema kufunga Ziwa Tanganyika na hili jambo limeleta *tension* kubwa sana kwa Watanzania ambao wako kwenye mikoa ambayo ipo kwenye Ziwa Tanganyika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kufunga ziwa kwa sababu ambazo Wizara wamefanya tafiti sio jambo baya. Mara zote tumekuwa tunapishana na mitazamo ya wasimamizi au Mawaziri waliopo kwenye sekta hizi kwa mambo yafuatayo; kwa sababu kuna watu ambao wamekopa mikopo leo kwa sababu ya shughuli ya uvuvi ukifunga Ziwa Tanganyika wakati hao wavuvi wamekata leseni ya mwaka mzima, hao wavuvi mikopo hiyo wanategemea wavue ili waweze kulipa hiyo mikopo, ukafunga ziwa bila kutengeneza njia mbadala ya wao kupata fedha na kuendesha Maisha yao, unakwenda kutengeneza vibaka kwa makusudi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili suala la kufunga ziwa kwa taarifa ambazo zinasikika kwa sababu hata Mbunge sijaambiwa wala sijashirikishwa. Wanasema eti samaki wamepungua, ukifunga ziwa kwa miezi mitatu, Samaki wanaenda kuongezeka? Kwa nini Serikali isije na mkakati wa makusudi wa kuzuia uvuvi haramu uliosababisha samaki kupungua? Mnakuja na sababu nyepesi ya kufunga ziwa kwa miezi mitatu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilitegemea kama nia ni njema ya Serikali ya kusaidia haya maziwa yawe endelevu kwa vizazi na vizazi. Cha kwanza wangeanza kuwapa elimu na kuwasaidia nyenzo wavuvi wetu kuanza kufuga samaki ili hata kwa kipindi hiki angalau cha hiyo miezi mitatu cha mpito wawe na njia mbadala.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili kama ndivyo tunataka tutekeleze hili jambo vizuri Serikali kwamba ikatoe elimu kwa

wavuvi hawa, hii kazi sio haramu na ndio maana wamelipa leseni. Lazima muende kule muwaambie wavuvi kwa nini mnafunga ziwa? Na kwa sababu mnafunga ziwa mmewaandaliaje mazingira ya wao kuishi na kulipa mikopo yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tofauti na hapo ni jambo la ajabu sana ambalo linakwenda kufanyika hivi sasa. Leo watu wa Mwambao wa Ziwa Tanganyika, wale uchumi wao, maisha yao ndio uvuvi kwa hiyo ukifunga hilo ziwa hawana eneo lingine la kuweza kujisaidia na kusaidia watoto wao. Naomba sana kama hilo jambo ndivyo lilivyo basi Serikali itafakari kwanza athari ya hili jambo ambalo wanaenda kuchukua. Kwa sababu hata ukifunga miezi mitatu kama umeshindwa kudhibiti uvuvi haramu baada ya miezi mitatu watakuja tena wavuvi haramu utakuwa umefanya nini? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niombe wataalamu wetu wasiwe wanatoa sababu nyepesi kwenye mambo magumu. Waje na mikakati ambayo itawasaidia Watanzania wote, ni kweli tunatambua faida watapokuwepo Samaki wengi hata wale wavuvi watanufaika. Lakini hii miezi mitatu hii fedha ambayo mnaenda kuitumia kufanya *patrol*, kwa nini msiitumie kufanya *patrol* ku - *control* huo uvuvi haramu badala ya kusubiri hicho kipindi ambacho hamtaki wavuvi waende. Lakini mtuambie kama mtafunga kwa hiyo miezi mitatu ile leseni ambayo wamelipia mwaka mzima itakuaje? Mtawalipa fidia? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niishauri Serikali kwa kuwa wavuvi wanapoambiwa wanaelewa, waende kwanza wakazungumze na wavuvi, wakishazungumza na wavuvi wavuvi nao watawaambia kwa nini miaka yote huko nyuma hawajawahi kufunga ziwa. Ziwa Tanganyika linajifunga *automatically* muda wa Samaki wanakwenda wanavuliwa…

**WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MHE. AIDA J. KHENANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kipindi ambacho sio cha msimu wa kuvua samaki wanaondoka…

**WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri wa Mifugo na Uvuvi.

**T A A R I F A**

**WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru lakini nilikuwa nataka, moja nimpe *comfort* Mheshimiwa Aida Khenani, kwamba alishalizungumza hili jambo na Ofisi yangu na baada ya kulizungumza tumekubaliana ya kwamba ziko hatua tunazokwenda kuzichukuwa. Miongoni mwa hatua ambazo tunakwenda kuzichukua ni pamoja na kukaa na Waheshimiwa Wabunge wa mwa mwambao wote wa Kanda ya Ziwa Tanganyika, Mikoa mitatu yote Kigoma, Rukwa na Katavi, lakini pia vile vile tutakaa na wawakilishi wengine wa wananchi ili tuelewane na dhumuni la Serikali kwenye jambo hili si baya lakini kama anavyosema nia ni kupata uelewa wa pamoja na tukienda twende kwa pamoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hivyo namuomba katika mchango wake pamoja na kwamba anatoa mchango mzuri wa kutukumbusha juu ya umuhimu wa wananchi kuendelea na shughuli yao lakini pia ajue kwamba ziko hatua Serikali inaendelea nazo ili kutokuleta taharuki kwa wananchi. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mheshimiwa Khenani unapokea taarifa?

**MHE. AIDA J. KHENANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napokea ni taarifa njema kwa sababu amesema na nasubiri utekelezaji wa hayo maneno yake na ni kweli tumeshazungumza na ofisi yake lakini mpaka sasa hatujaona chochote kinachoendela na presha ni kubwa sana kwa wananchi wangu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama ndivyo basi nishauri ushirikishwaji uwe wa kutosha, yaani ushirikishwaji kikamilifu sio wa juu wa juu najua wananchi wakielewa hata utekelezaji wake utakuwa ni mzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niendelee, Serikali imejenga bandari, imejenga Bandari Kalema, Kabwe, Kasanga, Kigoma ukitazama hizo bandari Serikali ilikuwa inategemea kupata matokeo chanya kupitia hizo bandari na kama ndivyo hatuwezi kuwa na bandari wakati mazao ambayo yanatakiwa yasafirishwe kwenda Congo hatuna meli. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna vitu ambavyo ndio uwekezaji ambao tunauzungumza leo ni uwekezaji gani huu? Unawekeza bandari huna meli unategemea meli ya nani sasa iwezekuja kubeba hiyo mizigo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu Mheshimiwa Waziri alichukuwa muda wangu nimalizie kwa dakika mbili.

**MWENYEKITI:** Sekunde 30 Mheshimiwa malizia.

**MHE. AIDA J. KHENANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa nashauri suala la MV Liemba imeshabaki ni historia, tupewe majibu ya meli ya mizigo na abiria si hizi stori ambazo zimekuwepo muda wote na hili jambo litawasaidia wananchi wa Mkoa wa Rukwa na itainua uchumi Mkoa wa Rukwa na mikoa yote ambayo inazunguka Ziwa Tanganyika, ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Aida, Mheshimiwa Seif Gulamali atafuatiwa na Mheshimiwa Cosato Chumi, Mheshimiwa Joseph Zacharius Kamoga ajiandae.

**MHE. SEIF K. S. GULAMALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kunipa nafasi hii kwa siku ya leo niweze kuchangia taarifa iliyowasilishwa na Mheshimiwa Waziri Mkuu ndani ya Bunge letu. Kwanza binafsi nipende kupongeza Serikali ya Mama Samia Suluhu Hassan, kwa kazi nzuri ambazo imekuwa ikiendeleza kufanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pongezi hizi haziende bure, Mama samia ameonyesha kweli ni Mama jasiri, Mama shupavu, jemedari, Mama Hangaya, Mama kweli kweli kama kuna watu walikuwa wakidhani labda wanamjaribu Mama hajaribiwi na hili limedhihirika katika miaka yake miwili aliofanya kazi. Sisi kama Wabunge ni mashahidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeweza kuwa na miradi mikubwa kama Taifa, tuna mradi mkubwa wa Bwawa la Mwalimu Nyerere kuna mradi mkubwa wa ujenzi wa *SGR,* lakini pia kuna miradi ya ununuzi wa ndege na viwanja wa ndege, tuna ujenzi wa *REA*, vyote hivi amevikuta na amevipokea vikiwa katika asilimia ya chini lakini Mama huyu jasiri, shupavu, amesimama imara na kuonyesha dunia au kuonyesha Watanzania kwamba wakina mama wanaweza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bwawa la Mwalimu Nyerere wakati Mheshimiwa Rais anachukua nchi, bwawa hili lilikuwa limefikia asilimia 42 toka ujenzi wake uanze, lakini leo hii tunazungumza bwawa hili limeshafikia asilimia 83, maana yake zaidi ya nusu ya kazi imeshafanyika. Hata ujazo wa maji, maji yanayohitajika pale inatakiwa maji mita 164, mpaka leo tunazungumza kuna ujazo wa maji mita 134 maana yake kama hali ya hewa ikienda vizuri na mvua ikaja tuna hakika mita 29 zilizobakia tunaweza tukazipata na tukaanza

majaribio ya umeme kutokana na bwawa lile la Mwalimu Julius Nyerere.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bwawa hili linaenda kuongeza umeme kwenye gridi ya Taifa kuwa na umeme *megawatt 2115.* Kwa hiyo, ni kazi nzuri ambazo ameendeleza kuzifanya, ambapo watu wengine walidhani kwamba bwawa lile lisingeweza kufika mwisho. Tunampongeza na kumtia moyo Mheshimiwa Rais kwamba aendelee kufanya kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine kubwa ambalo ameendelea kulifanya ni ujenzi wa reli. Tumeweza kuona ujenzi wa reli kutoka Dar es Salaam - Morogoro umeshafikia asilimia 97. Ujenzi wa reli ya Morogoro kuja Makutupora umeshafikia asilimia 92. Hii ni kazi nzuri na kubwa na ni kazi za kupongezwa, hizi kazi zimefikia asilimia hizi fedha zimelipwa, maana yake kazi zinazofuata zitakapokuwa zinaletwa *certificate* tunaweza kumalizia fedha zingine lakini kwa hizi kazi zinazofanyika hatudaiwi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine tumeona kazi ya ujenzi wa reli kutoka Makutupora kwenda Tabora asilimia nne tayari, tumeona ujenzi wa treni ya umeme kutoka Mwanza kuja Isaka umeshafikia asilimia 25, kwamba kazi inaendelea na tunampongeza sana Mheshimiwa Rais aendelee kufanya kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo ameendelea kulifanya Mheshimiwa Rais ni ununuzi wa Ndege na ujenzi wa viwanja vya ndege. Hivi karibuni tutapokea ndege zingine Tano ikiwemo moja kubwa ya kubeba mizigo. Ninampongeza sana Mheshimiwa Rais, Wabunge tunaedelea kumuunga mkono na kumtia moyo kwamba aendelee kuchapa kazi. Mama anaupiga mwingi kweli kweli. Kwa wapenzi wa mpira tunasema Mama anaupiga kama Mayele vile, anaupiga kama Mayele maana yake sasa hivi Mayele ni maarufu duniani, ni maarufu Afrika kwa sababu jinsi

anavyoweza kutupia magoli, ndivyo Mama anavyoweza kufanya kazi nzuri kwa Taifa letu. Tunampongeza sana Mama yetu Samia Suluhu Hassan kwa kazi nzuri anazozifanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tusiishie hapo, ameweza kutoa fedha nyingi za barabara wewe ni shahidi.

**MHE. STANSLAUS S. MABULA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

**MWENYEKITI:** Taarifa Mheshimiwa Mabula. Ahaa muda umekwisha.

**MHE. SEIF K. S. GULAMALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, muda umenipa dakika tano bado.

**MWENYEKITI:** Muda umeisha Mheshimiwa.

**MHE. SEIF K. S. GULAMALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, haya ahsante.

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Gulamali. Namuita Mheshimiwa Cosato Chumi, Mheshimiwa Joseph Zacharius Kamonga ajiandae.

**MHE. COSATO D. CHUMI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi japo sijafahamu ni dakika ngapi natakiwa kuchangia lakini itoshe tu kusema kwamba nami napongeza Ofisi ya Waziri Mkuu na Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa hotuba nzuri na kwa utendaji mzuri, pia kwa kwake Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa jinsi alivyokuwa mtu rahimu na mtu ambae anafikika hata ukiwa na jambo kwa ajili ya wananchi wako anakusikiliza na linapata ufumbuzi pale ambapo kuna changamoto. Kwa hiyo nawapongeza sana yeye na Mawaziri wanaofanya kazi katika Ofisi yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nitakuwa siyo mwingi wa fadhila kama sitampongeza Mheshimiwa Rais kwa kazi nzuri ambayo inafanyika katika sekta zote muhimu za afya, elimu maji na barabara, kama alivyosema Mheshimiwa Seif kweli kabisa Mheshimiwa Rais anaupiga mwingi. Anaupiga mwingi kama Mayele lakini pia anaupiga mwingi kama Clatous Chota Chama. Sasa ukichanganya hapo unaweza kuona ni jinsi gani mambo, yaani unajaribu ku-*imagine* Chama na Mayele mambo yanavyoweza kuwa mazuri. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kwa sababu mimi ni mwanamichezo naomba pia nitumie nafasi hii kuwapongeza Simba na Yanga kwa kufika hatua ya robo fainali, kwa sababu tumesema kwamba mpira na michezo kwa ujumla ni ajira ni biashara ni uchumi. Ninapenda pia nitumie nafasi hii kuwakumbusha tu Watanzania kwamba Simba hii ambayo imepangiwa na mabingwa watetezi wa Klabu Bingwa Afrika ilishawahi kupangiwa na mabingwa watetezi Zamalek mwaka 2003 na ikawatoa pale pale Cairo – Misri kwa mikwaju ya penati tatu kwa mbili baada ya kuwa wametoka moja bila Simba wameshinda kwa goli lililofungwa na Ndugu Emmanuel Gabriel dakika ya 56 lakini walipoenda kule Simba wakafungwa moja ikabidi waende kwenye changamoto ya mikwaju ya penati na Simba wakawang'oa Zamalek. Kwa hiyo, kama ambavyo tumepangiwa Mabingwa Watetezi vilevile watu waweze kujua kwamba tumejipanga vizuri tunaweza tukalitangaza Taifa na tukatangaza utalii wa nchi yetu.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Ester Bulaya taarifa.

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa nampa taarifa mchangiaji anatueleza historia sana lakini ninataka kumwambia ukizungumzia kikosi bora ni cha Young Africa na nimhakikishie kwenye mechi tunayokutana na Simba tutawafunga nasi kama tunaongoza *group* Nigeria

tunaenda kushinda. Tunaenda kuwaonesha, tunaenda kushinda ugenini.*(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Chumi taarifa unaikubali?

**MHE. COSATO D. CHUMI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naipokea kwa muktadha ufuatao, kwamba maisha ni historia, leo yetu imetengenezwa na jana na kesho yetu itatengenezwa na leo kwa hiyo nakubaliana nae. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo napenda kutumia nafasi hii kuipongeza sana Serikali katika suala zima la mbolea na ruzuku ya mbolea, kwa kweli Serikali imetusaidia sana. Serikali ilikuwa sikivu tulijenga hoja na kwa kweli wakatuwekea ruzuku. Hata hivyo, kumekuwepo na changamoto ya hapa na pale katika upatikanaji wa mbolea ile ya ruzuku. Kwa mfano, mbolea kutofika vijijini kwa wakati, pia changamoto za stika watu wanaenda stika zinakuwa bado, wakati mwingine wanaenda wanaambiwa kwamba *stock* haijasoma na kadhalika, lakini ni changamoto ambazo ni *manageable* tunaamini kwamba msimu ujao tutafanya vizuri zaidi. Kwa hiyo, ili tuboreshe suala zima la upatikanaji wa mbolea nina mambo machache ya kushauri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la kwanza nashauri ule usambazaji walau uende mpaka ngazi ya Kata. Pili, ninashauri ujazo wa mbolea iwe na ujazo tofauti tofauti. Wapo wakulima wengine wanahitaji ujazo wa kilo tano, wengine kilo 10, wengine kilo 20. Isiwe tu mbolea ya ruzuku mifuko iwe ni ya kilo 50 tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia ninaomba upatikanaji wa mbolea uwe ni kwa mwaka mzima. Nikisoma hapa katika taarifa ya Bajeti ya Mheshimiwa Waziri Mkuu ukurasa wa 31, kiasi cha takribani shilingi bilioni 284 zimetengwa kwa ajili ya ujenzi na ukarabati wa *scheme* za umwagiliaji. Maana yake ni kwamba, sasa tunaenda kujidhatiti katika kilimo ikiwemo

kule Mtula kwamba tutalima mwaka mzima. Kwa hiyo, kama tutalima mwaka mzima maana yake ni kwamba nashauri mbolea ya ruzuku pia ipatikane mwaka mzima, tusisubiri tu wakati ule ambao msimu unaanza, kwa sababu tume-*encourage* wananchi wetu walime mwaka mzima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, watu wa Iringa, Njombe tunalima kile kilimo cha mabondeni, kilimo cha vinyungu ni mwaka mzima. Tukimaliza sasa hivi kulima hichi kilimo cha kawaida tutarudi kilimo cha mabondeni pamoja na kuwa tunazingatia kutunza vyanzo vya maji. Kwa hiyo, ushauri wangu mbolea ipatikane mwaka mzima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kama ambavyo tumetoa ruzuku kwenye mbolea, Wananchi wa Mafinga nilipofanya ziara wameshauri kwamba pia mbegu nazo zipatikane mbegu za ruzuku ili kusudi vyote hivi viweze kusisimua kilimo chetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine tumeelezwa hapa kuhusu usalama wa chakula, lakini usalama wa chakula unaendana pia na usalama wa upatikanaji wa mbegu. Mimi nilikuwa nashauri hebu pamoja na taasisi yetu ya utafiti wa mbegu tuvishirikishe vyombo vyetu vya ulinzi na usalama hususan Jeshi la Kujenga Taifa katika kufanya tafiti za mbegu. Kwa sababu baadhi ya mbegu ambazo tunaletewa ni zile mbegu ambazo mwaka huu ukipanda mwakani haiwi kama zamani ambavyo tulikuwa tunatumia lilelile zao umepanda mwaka huu mwakani ukivuna baadhi ya sehemu ya mazao unatumia kama mbegu. Kwa hiyo, nilikuwa napenda kushauri hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la mwisho kwa sababu ya muda ni suala la *TARURA*. Kweli tunawapongeza kabisa kunatengwa bajeti, kama mimi hapa Mafinga mwaka 2021 tulikuwa tunapata shilingi milioni kama 900 lakini 2022/2023 tunapata mpaka shilingi bilioni 2.3 na tunatarajia itaenda

kuongezeka. Kama alivyosema Mheshimiwa Iddi kumekuwa na shida kubwa sana na changamoto ya Wakandarasi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pale Mafinga kwa mfano, kuna barabara ambayo Mkandarasi ilikuwa atukabidhi Tarehe 04 mwezi Machi lakini mpaka hapa ninapozungumza ameshakamatwa na TAKUKURU, ameshahojiwa na Mkuu wa Wilaya, ameshaitwa kwa Mkuu wa Mkoa, ameshaitwa mpaka kwa viongozi wa chama, *nothing is going on*. Kwa hiyo, nashauri wakati Mheshimiwa Rais na Serikali kwa ujumla inatenga fedha kwa ajili ya kuwaletea wananchi maendeleo, wako watu au baadhi ya Wakandarasi ambao siyo waaminifu wanapewa kazi lakini hawazifanyi kwa wakati, ambapo kimsingi wanakwamisha au kuchelewesha maendeleo ya wananchi. Kwa hiyo, ninashauri Serikali tutafute namna ikiwezekana tuwe na Wakandarasi wachache au kama hawana nguvu ya kifedha basi tuwatafutie *mechanism* ya kuwapa mikopo kwa namna ambayo itawezesha wao kufanya kazi kwa wakati na kwa ufanisi ili kusudi zile fedha na zile shughuli ambazo zimepangwa ziweze kufanyika, kwa sababu *it is very embarrassing* kwamba mtu kapewa kazi anatakiwa akabidhi Tarehe 04, Machi, mpaka leo ninavyozungumza tarehe 06 Aprili, amefanya kazi asilimia 18.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vyombo vyote vya Kiserikali *including* Chama cha Mapinduzi kimechukua kila hatua, *nothing is going on*. Sijui tunafanyaje maana sasa tunasema tusije tukawa tu Taifa la kulalamika ndiyo maana nashauri tutafute namna ambayo Wakandarasi wa namna hii pamoja na kuwachukulia hatua, tuone Je, kuna namna gani kama Taifa tunaweza kuwajengea uwezo Wakandarasi wetu wanaopewa kazi za ndani ili fedha ile tunayopitisha hapa Bungeni ikafanye kazi ambayo imekusudiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hilo naomba kuunga mkono hoja, nikisisitiza na kurudia kwamba

kuhusu suala la mafuta ya kula bado nasisitiza na kushauri tufanyeni kama *trial* tuwape JKT miaka miwili tuwawezeshe, tuone kama hatujajitosheleza kwa mafuta ya kula tukaokoa fedha za kigeni hizi ambazo kila mwaka tunatuma kununua mafuta ya kula hapa nchini, huo ndiyo ushauri wangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mungu atubariki wote, aibariki Simba na Yanga na awabariki Watanzania kwa ujumla. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Chumi kwa mchango wako. Mchangiaji wetu wa mwisho ni Mheshimiwa Joseph Zacharius Kamonga.

**MHE. JOSEPH Z. KAMONGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa kunipa ruhusa nami niwe mchangiaji wa mwisho siku hii ambayo na wewe umekaa kwenye Kiti hicho kwa mara ya kwanza, kama Mwenyekiti wangu wa Kamati ya Bajeti ninakupongeza sana kwa nafasi hiyo, nina imani kubwa na wewe kwamba utafanya vizuri na tunakutakia kila la kheri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hapo niende moja kwa moja kwenye mchango wangu. Mosi, nianze kumpongeza sana Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kazi nzuri sana anazozifanya kwenye taifa letu ikiwemo Jimbo langu la Ludewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, siku Mheshimiwa Rais anapokea ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali alitaja mashirika ambyo yanamkera likiwemo Shirika la *NDC*. Wakati ametaja Shirika hili la *NDC* wananchi wa Ludewa walifurahi sana na walishangilia sana na kumpongeza sana Mheshimiwa Rais, kwa sababu *NDC* wamechukua vitalu Ludewa miaka mingi sana vya makaa ya mawe, chuma lakini hakuna ambacho kinafanyika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo ninamshukuru Mheshimiwa Rais kwa kumteua huyu Mkurugenzi wa sasa kwa kweli anajitihada kubwa sana, naamini akimpa muda Dkt. Nicholaus atafanya mambo yale yaende kwenye vitendo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuliambiwa na watu wa *NDC* kwamba mwezi Oktoba wananchi wale wa Mchuchuma na Liganga wangeweza kulipwa fidia yao ya shilingi bilioni 15. Tunawashukuru walikwenda walihakiki wananchi wote, lakini Mheshimiwa Mkuu wa Mkoa alikwenda pale, Mheshimiwa Antony Mtaka nami nikiwepo akawahakikishia wananchi kwamba fidia zinalipwa mwezi Oktoba, bahati mbaya uhakiki umekamilika bado mpaka leo tunaenda Aprili ile fidia ilikuwa bado haijalipwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, juzi wananchi walikusanyika vikundi vikundi na kuanza kuhangaika kutaka kutafuta Waandishi wa Habari waweze kufikisha hisia zao kwa Mheshimiwa Rais kuonesha kwamba agizo lake halijatekelezwa la kuwalipa fidia wale wananchi wa Liganga na Mchuchuma. Katika ile taharuki bahati nzuri waliponipigia simu nami nilikwenda Wizara ya Fedha kufuatilia, nikabaini kwamba kibali cha kulipa ile fidia kilishatoka. Mheshimiwa Rais alitoa kibali kilitoka mwezi ule ambapo Mkuu wa Mkoa alikwenda kutoa ile ahadi kwa wananchi, bahati mbaya tu hapa katikati kuna vitu vingine ambavyo wale Wasaidizi ambao wanaikwamisha hata *NDC* ionekane ni taasisi ambayo haina uwezo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitumie nafasi hii kumshukuru Mheshimiwa Waziri wa Fedha, jana nilivyofuatilia pale Hazina nikaona kwamba ile *exchequer* leo ndiyo ilikuwa inatoka ili baada tu ya sikukuu wananchi wale waweze kwenda kulipwa fidia. Kwa hiyo, niliweza kuwashawishi wale wananchi kwamba waniamini na kitendo cha Mheshimiwa Waziri wa Fedha kukamilisha ile *exchequer* siku ya leo, naamini baada

ya sikukuu hii wananchi wale watakwenda kulipwa fidia na atakuwa ametuondolea aibu mimi na Mkuu wangu wa Mkoa ambao tulikwenda kuwahakikishia wale wananchi kwamba fidia watalipwa lakini mpaka leo miezi karibia minne, mitano imepita bila kulipwa fidia. Kwa hiyo, naomba sana Serikali iweze kusimamia jambo hili tuweze kuhitimisha fidia za wananchi hawa ambazo wamezisubiri toka 2015 na tuende mbele, mpaka sasa makaa ya mawe yana soko kubwa sana duniani kwa wafanyabiashara ambao wataweza kusafirisha makaa ya mawe waweze kuongeza Pato la Taifa na uchumi wa Wilaya yetu ya Ludewa uweze kukua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninamshukuru pia Mkurugenzi wa *NDC* kwa kukubali ushauri wetu tulioutoa kwamba vile vitalu walivyovihodhi kwa muda mrefu wafanye *apportionment,* wavigawe katika vipande vidogovidogo, wavitangaze, waweze kukaribisha wawekezaji wengi zaidi waweze kuchimba mkaa na kuuza sasa hivi ambapo una thamani kubwa duniani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri ule ameufanyia kazi na wamekwenda kugawa vitalu vile, tunawaomba sana katika kugawa vile vitalu wasiangalie tu matajiri wengine wa maeneo ya nje ya Mkoa wa Njombe, waangalie pia wale wachimbaji wadogo ambao wako maeneo yale ili nao waweze kushiriki kwenye uchumi. Waangalie Halmashauri iweze kushiriki uchumi huu na wawekezaji wengine wa ndani ya Mkoa. Namna hii itawezesha wananchi wale waweze katika kushiriki katika uchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile ikiwezekana hawa wachimbaji wanavyokwenda haya maeneo mengine ya sasa, waweze kuwaruhusu wananchi wale wakilipwa fidia waweze kununua hisa kwenye haya makampuni ili nao waweze kupata manufaa yatakayodumu vizazi na vizazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na uwekezaji huu wa Liganga na Mchuchuma kuna ile reli inayotoka Mtwara mpaka Mbamba Bay na tawi lake Mchuchuma na Liganga. Kuna wawekezaji ambao wanataka kujenga kwa mfumo wa *PPP*. Niliwasiliana na Ndugu Kafulila, Mkurugenzi wa *PPP* anaendelea nao kuwasikiliza. Kwa hiyo, ninaomba sana ikionekana wanao uwezo wa kujenga ile reli waweze kupewa nafasi hiyo ili waijenge na iweze kubadilisha kabisa uchumi wa ukanda huu wa Kusini miaka na miaka na kuongeza Pato la Taifa. Itatupunguzia hata kwenda kutegemea mikopo ambayo mingine ina masharti yasiyo mazuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, reli hii ikikamilika inaweza kuchangamsha hata shughuli zingine za kiuchumi. Sambamba na hili nilikuwa nazungumza na Waziri wa Ujenzi. Changamoto kubwa ya makaa ya mawe kule yaliko mpaka kwenye Bandari ya Mtwara, kuna changamoto kubwa ya *logistics,* usafirishaji kuyatoa pale mpaka kufikisha bandarini. Kwa hiyo, ni muhimu sana reli hii ikajengwa ili iweze kusafirisha malighafi za chuma na makaa ya mawe mpaka bandarini na kwenda mpaka kwenye masoko ya Kimataifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hili kutoka pale Ludewa kuna daraja moja ambalo lipo Kata ya Ibumi linaunganisha Wilaya ya Mbinga na Wilaya ya Ludewa. Daraja hili likijengwa itakuwa ni njia nzuri na ya mkato ya kuweza kupeleka makaa ya mawe bandarini Mtwara kuliko wakizunguka kilometa nyingi gharama za usafiri zitakuwa zimeongezeka sana. Kwa hiyo, naomba sana daraja hili liweze kujengwa ili lirahisishe usafirishaji wa makaa ya mawe vilevile shughuli za wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo hili lina ekari ambazo Halmashauri wamezitenga 3,500 ambazo zinafaa sana kwa kilimo cha umwagiliaji, kwa hiyo daraja hili likijengwa litarahisisha sana hata ajira kwa vijana katika sekta ya kilimo, mfumo ambao Waziri wa Kilimo ameuanzisha wa *BBT* ni

mfumo mzuri sana ambao utapunguza kero ya ajira. Tutafute sasa mfuko maalum ambao utaweza kuwakopesha vijana fedha wale wanaotoka JKT na wale wanaomaliza vyuo vikuu hasa vya kilimo na vyuo vingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa nasoma ripoti ya Mkaguzi inaonesha kwamba kuna Halmashauri 106 zilikuwa na Idara na Vitengo ambavyo vinaongozwa na watumishi 747 wasio na sifa. Wabunge wengine wamezungumzia hapa kwamba kuna tatizo kubwa sana la ajira, ninaamini Wabunge wengi wana vijana na wazazi wao kutoka kule Majimboni wanatutumia *message* kila siku na kutupigia simu. Kwa hiyo, naomba vilevile hizi nafasi za ajira ambazo zinaonekana zina matatizo ziweze kufanyiwa uchambuzi na kutangazwa. Kule wazazi wamesomesha vijana wao wako kijijini hawana shughuli. Kwa hiyo, maeneo kama haya ya miradi ya kilimo cha umwagiliaji wakipewa mikopo vijana wale wanaomaliza Chuo Kikuu cha Sokoine *(SUA)* wanaweza wakatengeneza ajira na wakalisha hata nchi hii kwa kutumia haya maeneo ambayo yanafaa kwa kilimo.*(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine….

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa muda wako umeisha naomba umalizie.

**MHE. JOSEPH Z. KAMONGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, namalizia. Kwa hiyo, baada ya kusema hayo machache kwa sababu nitapata nafasi ya kuchangia kwenye Wizara nyingine ninashukuru sana kwa kunipa nafasi naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Joseph Zacharius. Waheshimiwa Wabunge tumefika mwisho wa ratiba yetu ya jioni ya leo. Orodha ya wachangiaji wote walioletwa mezani imeshakamilika na niwakumbushe mambo machache:-

Waheshimiwa Wabunge, jambo la kwanza tunakumbushwa *Iftar* hapo kwenye viwanja vya Bunge ambayo imeandaliwa na Mheshimiwa Toufiq Salim Turky baada ya kumaliza Mkutano hapa, pia niwatakie Pasaka njema na wale watakaosafiri basi msafiri salama.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo ninaahirisha shughuli za Bunge hadi siku ya Jumanne, tarehe 11 Aprili, 2023 saa 3.00 asubuhi. *(Makofi)*

*(Saa 12.00 Jioni Bunge Liliahirishwa hadi Siku ya Jumanne, Tarehe 11 Aprili, 2023 Saa Tatu Asubuhi)*